# Nipashe

Jumatatu Machi 2, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580168

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




UKURASA 13



RIPOTI MAALUMU

## Madhila shule ya wanafunzi wasomao chini ya mti haya

UKURASA 4

# Vyama vya siasa vyamtega Membe

UKURASA 2



## YALIYOMO

UKURASA WA 5

**MBUNGE SUGU ADAI POLISI KUVAMIA MKUTANO WAKE**

HALI ya sintofahamu ilijitokeza jana kwenye mkutano wa hadhara wa...

UKURASA WA 8

**SAFARI YA TRENI YA KISASA MORO -DAR WAKATI WOWOTE**

SERIKALI imesema ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), umefikia zaidi ya...

## PM ataka vigogo kurejesha nyumba, mashamba

UKURASA 5

TAHADHARI CORONA




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na viongozi wa mkoa wa Tanga kwa ishara alipowasili kwenye uwanja wa ndege jana, kutekeleza maelekezo ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (kulia), ya Watanzania kutosalimiana kwa kushikana mikono au kukumbatiana ikiwa ni tahadhari dhidi ya ugonjwa wa corona. Kushoto ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga, Henry Shekifu na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela (wa pili kushoto). **PICHA: OWM**

# Askofu atoa tahadhari kuelekea uchaguzi mkuu

• **Asema** kuna umuhimu wa kufanya jitihada kabla ili kuondoa...*Endelea ukurasa 2*



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

**MICHEZO** TZ U-17 KIDEDEA KUFUZU KOMBE LA DUNIA UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6



Mchuuzi wa viatu ambaye jina lake halikupatikana, akifanya biashara katika mazingira yasiyo rafiki kama alivyokutwa katika moja ya mitaa ya Haydom Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Askofu atoa tahadhari kuelekea uchaguzi mkuu

**Na Daniel Limbe,** CHATO

ASKOFU wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Biharamulo, Vithalis Yusuph, amesema kuna umuhimu wa kufanya jitihada kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu, ili kuondoa upungufu uliojitokeza kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, uliofanyika mwaka jana.

Kadhalika, amevishauri vyama vya siasa kutosusia uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu, badala yake wawahamasishe wafuasi wao kujitokeza kwa wingi kutimiza takwa la kikatiba.

Askofu Yusuph, aliyasema hayo hivi karibuni wakati wa uzinduzi wa kituo cha maendeleo, malezi na makuzi ya mtoto kinachosimamiwa na Kanisa la Anglikana Parishi ya Chato, kwa ufadhili wa Shirika la kimataifa la Compassion tawi la Tanzania.

"Kwa kuwa Tanzania ni nchi yenye mfumo wa vyama vingi na kwa kuwa ni ya kidemokrasia hatuna budi kuona uchaguzi unakuwa huru na haki ili wananchi waweze kuwachagua viongozi wanaowataka... haitapendeza kuona nchi ingia kwenye sintofahamu kama ilivyojitokeza kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika mwaka jana," alisema.

Vile vile, alisema Kanisa linawajibu wa kuwalea waumini wake kimwili na kiroho ili kumtii Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na dunia ambaye ndiye msimamizi mkuu wa amani iliyopo nchini, na kwamba suala ya uchaguzi wa viongozi wa nchi ni muhimu katika kulinda na kudumisha utulivu wanaojivunia.

Uchaguzi wa serikali za mitaa ulifanyika Novemba 24, mwaka 2019, ambao vyama vya upinzani vilisusia kutokana na kutoridhishwa na taratibu zilizotumika za kuwaengua wagombea wao, ofisi kufungwa na mawakala kukataliwa.

Katika uchaguzi huo, CCM ilishinda kwenye vijiji 12,260 (asilimia 99.9), mitaa 4,262 (asilimia 100), vitongoji 63,970 (asilimia 99.4), na vyama vya ACT - Wazalendo na Chadema walishinda kwenye maeneo machache. Akiwa kwenye uzinduzi huo, Mkuu wa Wilaya ya Chato mkoani Geita, Charles Kabeho, alionekana kukerwa na ongezeko la watoto wanaolelewa na wazee wasiojiweza baada ya vijana wao kuwatelekeza na kutokomea kusikojulikana.

"Kitendo cha vijana kuwatelekezea wajukuu wazazi wao tena maskini hakipendezi hata kidogo...ndiyo maana baadhi ya wabunge walipendekeza kutungwa sheria ya kuwalazimisha watoto kuwatunza wazazi wao...yaani badala ya kumtunza mzazi ninyi mnawarundikia wajukuu ili waendelee kulea tabia hii haifai kabisa," alisema Kabeho.

Mratibu mradi wa maendeleo ya malezi na makuzi ya mtoto kituo cha Chato, Neema Kaloli, alisema jumla ya watoto wasiojiweza na wanaoishi mazingira magumu 200 wamesajiliwa tangu mwaka 2018 na wanahudumiwa kimwili, kiroho, kiafya na kiuchumi. "Lengo letu ni kuwawezesha watoto kufikia ndoto zao kipindi watakapofikisha miaka 22 na kwa sasa tunawasaidia kupata uchunguzi wa afya na tiba kila mwaka, vifaa vya kusomea na kujifunzia huku baadhi ya familia walizotoka tumewanunulia, mbuzi 80, magodoro, mavazi, pamoja na chakula lishe kwa wazazi wao wanaoishi na Ukimwi," alisema Neema.

Meneja wa Shirika la Compassion Kanda ya Ziwa, Emmanuel Pando, alisema taasisi hiyo inafadhili mradi huo kupitia makanisa takribani 500 nchini, huku mkoa wa Geita ukiwa kwenye makanisa 12 na kati ya hayo 4 yapo Wilaya ya Chato.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI-MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;54/2020

Ombi la MARKO LUCAS HUPA na MARY FIDELIS LYIMO Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu LUCAS JOHN HUPA.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 04/03/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 18/02/2020.

HAKIMU

115651202


# Vyama vya siasa vyamtega Membe

**Na Enock Charles**

SIKU nne baada ya aliyekuwa kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Bernard Membe, kuvuliwa uanachama wake, vyama vya upinzani vimetoa ya moyoni juu ya uwezekano wa kumpokea na kumpa nafasi ya kupeperusha bendera ya chama cha upinzania kwenye nafasi ya urais.

Membe ambaye amedai sababu za kufukuzwa kwenye chama chake alichokitumikia tangu akiwa Kamanda wa Vijana wa Mkoa wa Lindi na baadaye Mjumbe wa Kamati Kuu ya Taifa na Katibu wa Sekretarieti ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, ni kutokana na kuonyesha nia ya kugombea urais kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Duru za kisiasa zilieleza kuwa huenda mwanasiasa huyo, aliyeingia bungeni kwa mara ya kwanza mwaka 2000 kwa kuchaguliwa kuwa mbunge wa Jimbo la Mtama, atahamia kwenye chama kingine cha siasa ili kukamilisha ndoto yake ambaye mara kadhaa amesisistiza kuwa haifi.

Membe amekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa tangu mwaka 2007 hadi 2015.

Viongozi wa vyama vya upinzani waliozungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti jana, kila mmoja alieleza ya moyoni kuhusu mwanasiasa huyo, ambaye ameonekana kutoogopa kusimamia anachokiamini.

**CUF: TUNAMKARIBISHA**

Msemaji wa Chama cha Wananchi (CUF), Mohamed Ngulangwa, alisema chama hakina ubaguzi kwa mtu yeyote anayefikiria kujiunga na chama hicho kwa lengo la kukiongezea nguvu

kwa lengo la kuitoa CCM madarakani kwa kuwa lengo kuu la chama cha siasa ni kushika dola. Kuhusu kugombea urais, alisema ni muhimu iwapo mwanachama anayetaka kugombea akaielewa sera ya utajirisho ya chama hicho.

"Sifa hapa si umaarufu wake, tukiridhika kuwa ameilewa itikadi na sera yetu ya utajirisho si yeye tu hata Magufuli (Rais John Magufuli) akija na akafanikiwa kuwashawishi wanachama, tutampa nafasi," alisema Ngulangwa.

**ACT-WAZALENDO: NI MAPEMA**

Ofisa Habari wa Chama cha ACT-Wazalendo, Suphian Juma, alisema kwa sasa chama hicho hakiwezi kuzungumzia suala la ama atapokelewa au la, hadi baada ya kumalizika kwa kikao cha Halmashauri Kuu ya chama hicho inayotarajiwa kukutana jijini Dar es Salaam leo.

Alisema pamoja na mambo mengine, itajadili kuhusiana na uchaguzi ndani ya chama hicho.

**MBOWE: SIWEZI KUWA MPIGA RAMLI**

Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, alipoulizwa iwapo kada huyo anaweza kupokelewa na chama hicho kama ilivyokuwa kwa Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa aliyepokelewa dakika za mwishoni na chama hicho wakati wa uchaguzi mkuu mwaka 2015, alijibu kwa kifupi kuwa hawezi kuwa mpiga ramli kujua iwapo Membe ana mpango wa kuhamia katika chama hicho.

"Ninaomba nisiwe mpiga ramli katika jambo hilo," alisema Mbowe.

Membe alinukuliwa na chombo kimojawapo cha habari nchini alisema adhabu aliyopewa aliitarajiwa kutokana na nia aliyokuwa nayo ya kugombea urais na kueleza kuwa ndoto huwa haifi, na kwamba hata alipoulizwa na Kamati Ndogo ya Udhibiti ni Nidhamu ya chama hicho aliwajibu kuwa atagombea. "Niliwajibu kwamba ndiyo nitagombea, na nakwambia ningegombea wala nilikuwa sitanii," alisema Membe.

Mwaka 2015 Membe alikuwa miongoni mwa wanachama 42 waliotangaza nia kugombea urais kupitia CCM ambapo yeye pamoja na wenzake wanne akiwamo Rais Magufuli walifanikiwa kuingia tano bora kabla ya hapo. Baadaye yeye na Mbunge wa Bumbuli, Januari Makamba, walikatwa na kubakizwa watia nia watatu ambao walipigiwa kura na Rais Magufuli wakati huokuibuka mshindi na hatimaye kupeperusha bendera ya chama hicho.

Mkuu wa Idara ya Habari na Uenezi wa Chadema, Tumaini Makene, akizungumzia suala hilo, alisema chama hicho hakiwezi kuzuia mtu yeyote kujiunga nacho akikifananisha chama mfano wa bahari, ambayo haiwezi kujaa maji na kwamba hata Membe anaweza kujiunga na chama hicho kwa kuwa lengo la chama hicho ni kushika dola.

"Hatuwezi kumzuia ili mradi akubaliane na misingi ya Chadema, mtu yeyote anaweza akakaribishwa kama ambavyo Membe anaweza akakaribishwa...chama cha siasa chochote kile ambacho dhumuni lake kuu ni kushinda uchaguzi na kushika serikali na kuongoza dola, hakiwezi kujaa wanachama kama ambavyo bahari haiwezi kujaa maji," alisema. Uamuzi wa kumvua uanachama Membe ulifanywa na Kamati Kuu ya CCM na kutangazwa Ijumaa na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Humphrey Polepole.

Wengine ambao walikuwa wakituhumiwa kwa makosa ya kwenda kinyume cha maadili ni makatibu wakuu wastaafu, Yisig Mabamba na Abdulrahman Kinana, ambao nao wakihojiwa na kamati hiyo.

Hata hivyo, Kamati Kuu ilimpa karipio Kinana na kumsamehe Makamba.

TANGAZO


absa
Fungua huduma za kibenki kwa alama za vidole
absa
Pakua Absa Mobile Banking App
GET IT ON Google Play
Download on the App Store
Huo ndio Uafricanacity. Hiyo ndio Absa.
absa.co.tz
Uwezo huu unapatikana kwa baadhi ya simu.
Vigezo na masharti kuzingatiwa
Absa Bank Tanzania Limited (yenye usajili namba 38557) inaongozwa na kanuni za Benki Kuu ya Tanzania.

**RIPOTI MAALUM**

# Shule yenye wanafunzi wasomao chini ya mti

## ■Mvua ikija wachanganyika
## ■Chooni, walimu 'majanga'

**Na Halfan Chusi,** KILOLO

UKIIONA ni shule inayopendeza, ina wanafunzi 309 ambao katika mgawanyo wasichana wako 139 na wavulana 170. Katika lugha chapchapu ni kwamba, taaluma imetimia kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Mgowelo iliyoko Kata ya Nyanzwa wilayani Kilolo mkoani Iringa.

Lakini, ukifungua upande wa pili wa sarafu, kuna picha ya 'majanga', kwa maana wadogo zao kabisa walioko chekechea, darasa lao liko nje, tena chini ya mti. Jumla yao ni 52.

Haitoshi, mvua ikinyesha sura ya majanga ndiyo inazidi kumea zaidi maana inabidi wakimbilie kwa kaka na dada zao wa darasa la kwanza, wachanganyike pamoja.

Hapo napo panaibuka suala lingine la kitaaluma. Swali ni je, haya makundi mawili yana mitaala na miongozo ya mafunzo tofauti, mwalimu atafundishaje na kwa kutumia kigezo, ujuzi na mbinu gani ili kumwezesha kila mtu aelewe chake?

Kwa kifupi, hili nalo ni janga kwa kuwa mwalimu na mwanafunzi, kila mmoja ana mazingira tata kwa nafasi yake.

Hapo ni darasani, twende chooni. Huko nako kuna utata wa kiusalama, maana idadi ya matundu ya vyoo inayohitajika kukidhi huduma ya kiafya kwa wanafunzi hao ni pungufu. Hilo nalo linazaa simulizi za foleni, usafi duni na mwingiliano wa kijinsia mahali hapo.

Kisera, darasa moja linapaswa kuwa na wanafunzi 40, hivyo wanafunzi 309 wa Shule ya Msingi Mgowelo walipaswa kugawanywa katika vyumba vinane vya madarasa, lakini shule hiyo kwa sasa ina vyumba sita tu vya madarasa, hivyo kuwalazimu baadhi ya wanafunzi kusoma chini ya miti.

Vivyo hivyo kwa walimu, sera inaelekeza mwalimu mmoja kwa wanafunzi 40. Shule ya Msingi Mgowelo inatakiwa kuwa na walimu wanane, lakini kwa sasa ina walimu sita tu, huku mmoja akifundisha madarasa yote ya awali, yaani kuanzia chekechea hadi darasa la pili.

Kwa upande wa huduma ya choo, sera inaelekeza wavulana 25 na wasichana 20 kwa tundu moja la choo, lakini shule hiyo ina matundu sita tu, manne kwa ajili ya wasichana na mawili kwa ajili ya wavulana.

Hii ina maana kwamba, wanafunzi wa kike katika shule hiyo wanahitaji matundu saba ya vyoo na wa kiume wanahitaji matundu saba pia, tofauti na uwiano wa sasa uliopo shuleni wa wasichana 35 na wavulana 85 kwa tundu moja la choo.



Hali ya usomaji ilivyo kwa wanafunzi wa madarasa ya awali katika Shule ya Msingi Mgowelo wilayani Kilolo mkoani Iringa. **PICHA: HALFAN CHUSI**

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Omari Mkangama, anakiri kuelemewa na 'majanga' hayo kuanzia madarasani hadi huduma ya kiusalama ambako ananena:

"Shule inakabiliwa na uhaba wa madarasa kwa wanafunzi kama unavyoona hapo nje, chekechea hawana mahali pa kusomea. Shule ina vyumba sita tu vya madarasa, lakini kimsingi ilitakiwa kuwa na vyumba vinane kutatua tatizo lililopo.

"Wanafunzi wa madarasa ya awali wanalazimika kusomea nje huku darasa la kwanza wakisoma kwa kupokezana na wanafunzi wa darasa la pili.

"Msimu wa mvua wanapata tabu sana, mvua ikinyesha tunalazimika kuwachanganya wanafunzi wa awali na darasa la kwanza pamoja ili kuwanusuru wasiloe."

Kwa upande wa vyoo, Mwalimu Mkangama alisema shule yake inakabiliwa na uhaba wa vyoo, akibainisha kuwa hata vichache vilivyopo, baadhi ni chakavu na hivyo kuhatarisha afya za wanafunzi.

Alisema kutokana na uchakavu huo, wanafunzi wanakuwa katika hatari ya kupata magonjwa kama kuhara na maambukizo katika njia ya mkojo (U.T.I).

"Matundu ya vyoo tunayoyategemea zaidi ni mawili ambayo ndiyo yako katika hali nzuri. Mengine (manne) ni chakavu, hivyo tunahitaji matundu mengine walau manne, mawili kwa wasichana na mawili kwa wavulana ili tuwe na matundu 10 yatakayotatua tatizo lililopo," aliomba.

Mwalimu wa Afya, Caroline Mafanya, aliambia Nipashe shuleni hapo kuwa uhaba wa matundu ya vyoo unawaathiri kiafya wanafunzi, hasa wa kike.

"Mara nyingi wanafunzi wanaugua U.T.I. Hii yote ni kwa sababu wanafunzi wengi wanatumia choo kimoja na watoto wadogo kama hawa hawajui kuchukua tahadhari kiafya," alifafanua.

Mwalimu wa Taaluma wa shule hiyo, Laurence Mpolenzo, alisema uhaba wa walimu shuleni umekuwa ukisababisha baadhi ya wanafunzi kushindwa kufikiwa na walimu madarasani.

"Walimu ni wachache, wakati mwingine baadhi ya walimu wanashindwa kufika katika madarasa husika katika vipindi husika. Kama unavyoona hapa, tuna mwalimu mmoja ambaye anatakiwa afundishe chekechea, darasa la kwanza na la pili.

"Sasa mwalimu mmoja anawezaje kujigawa kutoka huduma kwa madarasa yote hayo kwa siku? Hapo lazima mwalimu atashindwa kuwafikia wanafunzi wote kwa mara moja.

"Shule ina wanafunzi 309 lakini walimu tuko sita tu (mwanamke mmoja). Hata ukiangalia uwiano wa wanafunzi na walimu, unabaini kabisa walimu ni wachache," alilalamika.

Mwalimu Mpolenzo aliiomba serikali iongeze walimu hasa wa kike shuleni hapo ili ifanye vizuri kitaaluma, akibainisha kuwa kwa sasa shule hiyo haifanyi vizuri kitaaluma.

Mratibu Elimu Kata, Silvanus Dunda, alikiri kuwa na taarifa za uhaba wa walimu na hali duni ya miundombinu katika shule hilo na kubainisha kuwa alishawasilisha taarifa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo.

"Mpaka sasa, taarifa ziko kwa mkurugenzi, naye anaangalia namna ya kutatua matatizo yaliyopo. Tuna taarifa za mwalimu mmoja kustaafu, tunaangalia pia jinsi ya kuziba pengo lake.

"Hata uhaba wa vyoo ni tatizo ambalo tunalijua katika shule hiyo. Kimsingi shule kama hii inatakiwa kuwa na matundi si chini ya 10 ya vyoo, lakini yaliyopo kwa sasa ni sita tu, na kati ya hayo sita, manne hayako vizuri, yanahitaji marekebisho. "Ndani ya mwaka huu, tuna mpango wa kuongeza vyumba viwili vya madarasa katika shule hiyo. Wakati tunalifanya hilo, tutaangalia na namna ya kuongeza walau matundu manne ya vyoo," aliahidi.

Amidu Kilamba, Diwani wa Nyanzwa, alisema wameshafyatua matofali kwa ajili ya vyumba viwili vya madarasa na matundu manne ya vyoo.

"Tunatarajia msimu wa mavuno, tutachangisha pesa kidogo kwa wanakijiji ili tupate angalau pesa ya kunyanyulia kuta na ikibidi kupaua kabisa," alisema.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji, Antoni Kiwonde, na Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Bakari Mtalula, kwa pamoja walikiri kuwapo kwa vikwazo hivyo vya elimu shuleni hapo wakisema wamekuwa wakiwachangisha wanakijiji ili kupata pesa za kuongeza vyumba vya madarasa na kuboresha miundombinu ya vyoo.

INAENDELEA KESHO

## Sugu adai Polisi kuvamia mkutano wake

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALI ya sintofahamu ilijitokeza jana kwenye mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu,' baada ya Jeshi la Polisi kuzuia mkutano huo uliokuwa unatakiwa kufanyika katika Kata ya Igazo, jijini hapa.

Akizungumza na Nipashe, Sugu alidai Polisi walivamia mkutano huo na kuwalazimisha wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), waliokuwa wamekusanyika watawanyike. Alidai waliwalazimisha vijana waliokuwa kwenye gari la matangazo ambalo alilikodi mwenyewe, wawatangazie wananchi kuwa wanatakiwa kutawanyika kutokana na mkutano huo kuzuiwa usifanyike.

Alidai baada ya vijana hao kukataa, gari hilo lilikamatwa na askari hao pamoja na baadhi ya vijana na kuondoka nao kwenda Kituo Kikuu cha Polisi.

Hata hivyo, alidai alikuwa na kibali cha kufanya mkutano huo ambacho kilitolewa na Jeshi la Polisi siku mbili kabla ya mkutano huo, na kwamba kabla ya hapo alikuwa hajawahi kufanya mkutano mwingine.

"Nilianza muda mrefu kuomba kibali na Katibu wangu alikuwa anashinda muda mrefu Polisi kufuatilia kibali hicho, sasa nilikipata jana (Jumamosi) saa 6:00 mchana na nilitakiwa nifanye mkutano huo saa nane siku hiyo hiyo," alisema Sugu na kuongeza:

"Nilimpigia RPC simu kumweleza hali hiyo na nikamwambia kuwa siwezi kufanya mkutano huo kwa sababu nahitaji kufanya maandalizi, akaniambia yeye alishatoa kibali hicho muda mrefu na akaniuliza ulitaka ufanye lini nikamwambia Jumapili (jana) na akanikubalia," aliongeza.

Aliongeza kuwa baada ya kukubaliwa na RPC kwa simu alimwomba amwandikie barua kwa maelezo kuwa amekuwa akifanyiwa figisu mara nyingi katika mazingira kama hayo, lakini akahakikishiwa kuwa hakuna atakayeangemzuia.

Hata hivyo, alisema baada ya kuzuiliwa kwa mkutano huo alimpigia RPC simu kumweleza hali iliyotokea na akathibitishiwa mkutano huo ulikuwa umezuiliwa, lakini sababu alizoelezwa hazikueleweka. Sugu, alisema kabla ya kuomba kibali Polisi, alishafanya mazungumzo na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola na Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, kuomba aruhusiwe kufanya mikutano.

Alisema viongozi hao walikubali ombi lake. Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema yeye hakumzuia 'Sugu' kufanya mkutano huo na kwamba aliruhusu uendelee.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara NBC Tanzania, Theobald Sabi (kushoto), akipokea tuzo ya utendaji uliotukuka katika uchakataji wa miamala ya VISA mitandaoni kwenye POS na ATM kutoka kwa Mkurugenzi wa Visa nchini, Olive Njoroge, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PM aagiza vigogo kurudisha nyumba

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza kurejeshwa serikalini nyumba 11 zilizochukuliwa na watumishi kwa udanganyifu na mashamba ekari 2,000 ambayo hayajaendelezwa.

Alitoa agizo hilo jana jijini Tanga wakati akizungumza na watumishi wa halmashauri za mkoa huo, viongozi wa taasisi mbalimbali, viongozi wa dini na wadau wa zao la mkonge, baada ya kupokea taarifa ya uchunguzi wa tuhuma za uhujumu wa zao hilo.

Akitoa agizo hilo, alisema nyumba namba 176 iliyopo eneo la Bombo ambayo ilimilikishwa kwa aliyekuwa Mwenyekiti wa Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Salum Shamte, irejeshwe serikalini.

Nyumba nyingine 10 zilizoko ndani ya Jiji la Tanga katika maeneo ya Raskazone, Bombo, Nguvumali na Market street, ambazo zilinunuliwa na watumishi hao kwa udanganyifu, zinapaswa kurejeshwa.

Vile vile, Waziri Mkuu aliagiza wawekezaji ambao wanamiliki mashamba ya mkonge yenye ukubwa wa zaidi ya ekari 2,000 ambao hawajayaendeleza, wayaendeleze na wakishindwa yatachukuliwa na kugawiwa kwa wananchi.

Timu hiyo maalum ya uchunguzi iliundwa na Waziri Mkuu na ilifanya uchunguzi mkoani Tanga kuanzia Novemba 29, mwaka jana hadi Februari 7, mwaka huu. Timu hiyo iliyokuwa na wajumbe 13, ilihusisha maofisa kutoka ofisi mbalimbali za serikali ikihusisha masuala mbalimbali ya tasnia ya zao hilo ambayo ni pamoja na uzalishaji wa mkonge, bei ya zao la mkonge katika soko la ndani na nje ya nchi.

Pia, ilichunguza kuhusu mali za iliyokuwa Mamlaka ya mkonge nchini, ubia kati ya Kampuni ya Katani Limited na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Utendaji kazi wa Kampuni ya Katani Ltd na pia utendaji kazi wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB).

Awali, Mwenyekiti wa timu hiyo, Gerald Kusaya, alisema timu ilibaini kuwa Kampuni ya Katani Ltd tokea mwanzo ilikuwa na mgongano wa kimaslahi na kusababisha kuhujumu uchumi kwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wake Shamte, alikuwa mtumishi wa umma na alishiriki vikao vyote vya ubinafsishaji wa Mamlaka ya Mkonge ilhali akijua kuwa ana maslahi kwenye kampuni inayonunua.

"Kwa kuwa uchunguzi umebaini viongozi na wanahisa wa Katani Ltd waliohusika kuingia mikataba walikuwa watumishi wa Mamlaka ya Mkonge wakati wa mchakato wote wa ubinafsishaji, hivyo walitumia vibaya madaraka yao kuishawishi serikali kuingia mkataba huo usiokuwa na tija kwa serikali bali kwa manufaa yao binafsi. Hivyo, timu imeandaa taratibu kwa ajili ya wahusika kuchukuliwa hatua za kisheria."

Kusaya alisema timu hiyo inapendekeza kuwa serikali itoe fedha kwa ajili ya kazi ya kuyapima upya mashamba matano ya Mwelya, Ngombezi, Hale, Magunga na Magoma, ili wananchi wanaoendelea kutumia mashamba hayo kwa kukodishwa na Bodi ya Mkonge kama ilivyokubalika kwenye Baraza la Mawaziri mwaka 2005 waweze kupewa hati ndogo.

Alisema timu inapendekeza nyumba 30 zilizopo eneo la Muheza, ambazo baadhi zilitolewa kwa wananchi waliokuwa watumishi wa Mamlaka ya Mkonge na baadhi kuachwa kwa ajili ya makazi, ziendelee kuwa mali ya wananchi hao kwa kuwa eneo hilo kwa sasa lipo chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

"Nyumba 22 zilizoko ndani ya mashamba ya mkonge na maeneo ya kiwanda cha TANCORD, ziendelee kubaki mali ya serikali na nyumba iliyoko katika kiwanja Na. 176 irejeshwe serikalini kwa njia ya urekebishaji wa Daftari la Msajili wa Hati."


**NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kampuni ya **WAUNGWANA AUCTION MART, ADILI AUCTION COMPANY NA KOTI BROTHERS,** kwa niaba ya AccessBank Tanzania Limited watauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba, Magari na Viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili, Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | KAMPUNI INAYO HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | LUMUMBA | WAUNGWANA AUCTION MART | MLAY/E,PRINCESS | PRINCESS ELIAS MLAY | TOYOTA RAV 4 T759BTV | TABATA | 19/03/2020 SAA 4:00 ASUBHI |
| 2 | LUMUMBA | ADILI AUCTION COMPANY | MLELA/C,JULIETH | NYENGA/JOHN,GEOFREY | NYUMBA | KIJICHI | 19/03/2020 SAA 4:00 ASUBHI |
| 3 | LUMUMBA | WAUNGWANA AUCTION MART | MUNGUTWA/MAJID,ABDUL | MUNGUTWA/MAJID,ABDUL | NYUMBA | KIJICHI | 19/03/2020 SAA 4:00 ASUBHI |
| 4 | LUMUMBA | RIMBO AUCTION MART | MWANGOBOLA/AMOS,SHABA | MWANGOBOLA/AMOS,SHABA | NYUMBA | TABATA | 15/03/2020 SAA 4:00 ASUUHI |
| 5 | PAMBA | WAUNGWANA AUCTION MART | ALOYCE/S,DEUS | ALOYCE/S,DEUS | KIWANJA | NYAMADOKE BUSWELU | 16/03/2020 SAA 4:00 ASUBHI |
| 6 | LUMUMBA | WAUNGWANA AUCTION MART | TWEVE/J,SILVER | TWEVE/J,SILVER | KIWANJA | MKURANGA | 14/03/2020 SAA 4:00 ASUBHI |
| 7 | PAMBA | WAUNGWANA AUCTION MART | ALOYCE/S,DEUS | ALOYCE/S,DEUS | KIWANJA | NYAMADOKE BUSWELU | 16/03/2020 SAA 4:00 ASUBHI |
| 8 | PAMBA | WAUNGWANA AUCTION MART | ALOYCE/S,DEUS | ALOYCE/S,DEUS | KIWANJA | NYAMADOKE BUSWELU | 19/03/2020 SAA 4:00 ASUBHI |
| 9 | KIJITONYAMA | KOTI BROTHERS | HISAYA/JASON,GASPER | HISAYA/JASON,GASPER | FINISHED HOUSE | SALASALA | 17/03/2020 SAA 4:00 ASUBHI |
| 10 | KIJITONYAMA | KOTI BROTHERS | NKOLONA/ALLY,HASHIMU | NKOLONA/ALLY,HASHIMU | FINISHED HOUSE | MBEZI MWISHO | 16/03/2020 SAA 4:00 ASUBHI |
| 11 | KIJITONYAMA | ADILI AUCTION | MARANDU/F,ERASMI | MARANDU/F,ERASMI | FINISHED HOUSE | KIBWEGERE | 18/03/2020 SAA 4:00 ASUBHI |
| 12 | KIJITONYAMA | KOTI BROTHERS | SILEMU/EVODI,LINA | SILEMU/EVODI,LINA | FINISHED HOUSE | KIHARAKA BAGAMOYO | 19/03/2020 SAA 4:00 ASUBHI |
| 13 | KIJITONYAMA | ADILI AUCTION | NGWAITO/M,WILLIAM | NGWAITO/M,WILLIAM | UNFINISHED HOUSE | UDINDIVU BAGAMOYO | 21/03/2020 SAA 4:00 ASUBHI |
| 14 | KIJITONYAMA | ADILI AUCTION | KUNDI/D,VICTORIA | KUNDI/D,VICTORIA | FINISHED HOUSE | MBAGALA | 14/03/2020 SAA 4:00 ASUBHI |
| 15 | KIJITONYAMA | KOTI BROTHERS | HISAYA/JASON,GASPER | HISAYA/JASON,GASPER | FINISHED HOUSE | SALASALA | 14/03/2020 SAA 6:00 MCHANA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. UKAGUZI UNARUHUSIWA MARA USOMAPO TANGAZO HILI.
2. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA MALIPO YA 25% YA FEDHA TASLIMU PAPO HAPO NA 75% BAADA YA SIKU 14 TOKA SIKU YA MNADA KUFANYIKA NA UKISHINDWA KULIPA MALIPO YALIYOBAKI MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZO LIPA HAZITARUDISHWA
3. GHARAMA ZA KUBADILISHA UMILIKI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE, KUMBUKA VIGEZO NA MASHARTI KUZINGATIWA.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI**
**WAUNGWANA AUCTION MART 0713077474**
**KOTI BROTHERS 0713836150**
**ADILI AUCTION MART 0716651103**

**WOTE MNAKARIBISHWA.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mchakato uboreshaji viwanja uende na darasa kwa wamiliki

**SHIRIKISHO** la Soka nchini (TFF), limeeleza kwamba lipo katika mazungumzo ya kuingia mkataba na kampuni moja ya nje kwa ajili ya uboreshaji na usimamizi wa viwanja vya soka nchini.

Makamu wa Rais wa TFF, Athumani Nyamlani, alinukuliwa mwishoni mwa wiki akielezea hatua ya mchakato huo ambao unalenga kuona soka likichezwa katika mazingira salama na rafiki kwa afya za wachezaji.

Katika hilo, Nipashe tunaamini kama tunataka kuona soka la nchi hii likipiga hatua, hatuna budi kuhakikisha tunakuwa na viwanja bora na rafiki kwa mchezo huo unaoongoza kwa kupendwa zaidi duniani.

Aidha, ni ukweli usiopingika kwamba uwapo wa viwanja bora, utavutia mashabiki wengi kwenda uwanjani hivyo kuziingizia klabu husika, TFF na serikali kwa ujumla kipato kikubwa.

Si hivyo, bali pia tunatambua mashabiki wengi nje na ndani ya nchi watavutiwa kuifuatilia ligi yetu kwa njia ya luninga jambo ambalo litaongeza matangazo mengi na klabu kuzidi kunufaika kimapato.

Tunatambua hakuna njia mbadala kama kweli tunataka kupiga hatua kwenye soka, ni lazima TFF, serikali na hata wadau kuwa kitu kimoja katika kuhakikisha kunapatikana viwanja bora na vinatunzwa kwa kiwango cha juu.

Lakini tunatambua zaidi ya asilimia 90 ya viwanja vya soka nchini vinamilikiwa na chama tawala, CCM, hivyo serikali ni lazima kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha uboreshwaji huo unaokwenda kufanyika vigezo na masharti vinazingatiwa.

Tunasema hivyo kutokana na ukweli kwamba mara nyingi wamiliki wa viwanja hivyo wamekuwa mstari wa mbele katika kuviharibu kwa kuvifanyia ama kuvikodisha kwa matumizi tofauti na soka.

Mara nyingi tumeshuhudia viwanja hivyo vikikodishwa kwa shughuli xs matamasha ya muziki na mikutano mbalimbali ambayo husababisha uharibifu mkubwa katika eneo la kuchezea ('pitch').

Hivyo, kama hapatakuwa na ushirikiano wa kutosha katika hilo, mchakato huu wa uboreshaji ambao TFF inakwenda kufanya, hautakuwa na maana yoyote katika viwanja hivyo na soka letu kwa ujumla.


Viongozi wa CCM Mkoa, ambao ndio wanaobeba dhamana ya kuvisimamia na kuvilinda viwanja hivyo, wengi wao hawavijali na wamekuwa wakitanguliza maslahi mbele kuliko kuvitunza kwa faida ya soka letu.

Mfano mzuri ni tamasha la Krismas la msanii wa muziki wa kizazi kipya, Diamond Platinum, lililofanyika katika uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya na kuuharibu vibaya, hivyo mechi za Tanzania Prisons na Mbeya City kulazimika kuhamishiwa viwanja vingine.

Nipashe hatukuona sababu ya tamasha hilo ambalo pia lilihudhiriwa na waziri mwenye dhamana ya Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungamo wa Tanzania, Dk. Tulia Akson, kufanyika uwanjani hapo wakati lilikuwa la bure, bila kiingilio.

Ni ukweli usiopingika kuwa, nchini vipo viwanja vingi vya wazi, lakini pia matamasha ya muziki hufanyika katika kumbi za starehe, hivyo kuelekea uboreshwaji huo tunaiomba serikali sasa ipige marufu shughuli zozote kinyume cha soka zinazoweza kuharibu eneo la kucheza kutofanyika viwanja vya soka. Hakutakuwa na maana yoyote kama TFF itaingia makubaliano hayo na kampuni ya kuviboresha viwanja huku wamiliki wakiwa mstari wa mbele katika kuvikodisha kwa matumizi kinyume cha soka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kipigo Liverpool somo mashabiki Simba, Yanga

Na Adam Fungamwango

**WATFORD,** timu kibonde kwenye Ligi Kuu ya England imetibua rekodi ya Liverpool kushinda mechi mfululizo kwenye ligi hiyo, baada ya kuitandika mabao 3-0 Jumamosi iliyopita.

Si mashabiki wengi wa soka duniani waliotegemea timu kama Liverpool inaweza kufunga na timu kama hiyo. Inawezekana wengi waliamini Liverpool haiwezi kutwaa ubingwa wa England bila kufungwa, lakini si kwa timu kama hiyo kuifunga.

Watford wakahitimisha mechi 44 za Liverpool kucheza bila kufungwa kwa mabao ya Ismaila Sarr aliyefunga mawili, lakini pia Troy Deeney naye akashindilia msumari wa mwisho kwenye jeneza la wapinzani wao.

Pamoja na kufungwa, bado Liverpool wana asilimia kubwa ya kutwaa ubingwa huo, huku Watford, ikijipapatua kwenye timu zenye hati hati ya kushuka daraja.

Liverpool imebaki kwenye nafasi yake ya kwanza kwa pointi 79, wakati Watford ikifikisha pointi 27, ikiwa kwenye nafasi ya 17.

Sipati picha kama timu za Tanzania, Simba ama Yanga zingefungwa na timu kibonde kama hiyo wakati zikiwa kwenye nafasi ya kutwaa ubingwa.Walahi, kusingekalika wanachama na mashabiki wa timu hizo saa hizi 'povu' lingekuwa linawatoka.

Tungesikia kocha afukuzwe. Kocha ameshindwa kupanga kikosi kizuri. Kocha haelewani na msaidizi wake. Kwa nini mchezaji fulani hajapangwa. Pia tungesikia wengine wakisema kuwa Shirikisho la Soka nchini (TFF) viongozi wake wote ni timu fulani.

Waamuzi wanaibeba timu fulani ndiyo maana tumefungwa. Tunafungwa kwa sababu tunapuliziwa dawa kwenye vyumba na ndiyo maana wachezaji wetu wanachoka kipindi cha pili.

Bongo ndiyo nchi pekee ambayo Simba na Yanga zikifungwa basi hazifungwi kwa haki. Hazikuzidiwa ufundi na timu pinzani wala uwezo, ila kuna tatizo tu nje ya uwanja ndilo limesababisha.

Unaweza ukasikia hata mtu akisema hatufanyi vema kwa sababu hatulindi uwanja, sasa tuanze kulinda uwanja ili wapinzani wasiufanyie vitendo vya kishirikina.

Mifano ipo. Simba ilifungwa na Mwadui kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza, lakini pia ilifungwa na JKT Tanzania kwenye mechi ya mzunguko wa pili.

Yanga ilichapwa mabao 3-0 dhidi ya Kagera Sugar, baadaye ikafungwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC.

Kama haitoshi hapo kati, ilitoka sare mfululizo ya bao 1-1 dhidi ya Mbeya City na Polisi Tanzania, lakini suluhu ya bila kufungana dhidi ya Prisons na Coastal Union.

Wanachama na mashabiki wa klabu hizo walikuja juu na maneno ambayo yanaonyesha kama timu hizo hazina haki ya kufungwa, ila kushinda peke yake.

Wanashindwa kutambua kuwa timu yoyote ambayo iko Ligi Kuu ina haki na uwezo wa kushinda kama nyingine yoyote.

Liverpool inayoongoza Ligi Kuu kwa muda mrefu na ndiyo timu inayotarajiwa kutwaa ubingwa msimu huu kwa dalili zote, imefungwa na timu ambayo huenda ikashuka hata daraja kama haikukaza kwenye mechi zilizobaki, lakini hutowasikia mashabiki wa timu hiyo wakimlaumu yeyote yule.

Wamezidiwa, yamekwisha, wanaangalia mechi ijayo. Hili ndilo soka. Kama Liverpool inafungwa na timu kibonde, Simba au Yanga ni nani?

Wanachama na mashabiki wa klabu hizo kongwe waache kulalamika sana timu yao inapofungwa kwa sababu hata timu zinazocheza nazo zinatafuta ushindi. Halafu nazo huwa zinaumia pia zinapofungwa kama wenyewe wanavyoumia timu zao zinapopoteza mechi.

Kipigo cha Liverpool nadhani litakuwa ni somo kuwa hakuna timu yoyote duniani ina hatimiliki ya kushinda tu mechi zote, au kufungwa. Hata inaposhinda vipi, ipo siku itapata mbabe wake itafungwa. Hakuna uchawi, hujuma, refa, wala anayebebwa. Soka ndivyo lilivyo, Simba, Yanga mjifunze kwa hilo.

BARUA & MJADALA

# Umeamua vizuri DC Bagamoyo

**Mhariri,**

*MWISHONI mwa wiki iliyopita, kupitia vyombo vya habari ikiwamo chombo chako gazeti la Nipashe, tulisikia kuchukuliwa uamuzi mgumu kupigwa marufuku muziki wa vigodoro wilayani Bagamoyo.*

*Nalazimika kuutaja ni uamuzi mgumu, kwani nia ya muziki huo uliozoeleka sana katika staili ya kukesha kuuzuiwa ni maumivu makubwa, kuwakosesha wakazi husika burudani yao.*

*Kwa maana hiyo, uamuzi kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, itakuwa jambo gumu kwa waumini wake, lakini hakuna namna ya kuamua vinginevyo, zaidi ya kutekekeza maelekezo ya kiserikali, wakitakiwa kuelekeza nguvu zaidi katika matakwa ya kiserikali.*

*Sababu iko wazi kwamba ni katika nia nzuri, kuwasukuma wakazi wa Bagamoyo wawe na mazingira bora ya kuwajibika kimaendeleo, wakianza kusahau na kuweka kando starehe hiyo ya kiutamaduni.*

*Niseme, kwanza ndugu zangu wa Bagamoyo na kwingine kote kwenye maagizo yanayofanana, mabadiliko ya namna hiyo wanapaswa kukubaliana nayo, kuwezesha azma ya kiutawala kusukuma maendeleo ya kitaifa katika eneo lao.*

*Wanasema, kila penye maendeleo hapakosi hasara yake, kwa maana wanayotumia wachumi kwamba, ili kupata maendeleo kunapaswa kuwapo upungufu kwa wakati fulani kusamehe jambo mlilo nalo au tarajiwa katika nafasi ya mbadala.*


*Wenyewe wasomi wa uchumi kitaalamu huiita 'opportunity cost.' Ndiyo hasa, starehe ya muziki wa vigodoro huko Bagamoyo inawekwa kando, kwa mbadala ya uchapaji kazi kwa ajili ya maendeleo.*

**Manspeer Magaupi,**
**Kibaha**

WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Daraja la Kwanza mbona vurugu kama mchangani?




**Na Adam Fungamwango**

NAKUMBUKA wakati huo nikiwa mdogo, nikianza kupenda soka na kwenda kwenye mechi mbalimbali za mchangani.

Kwa wale waliozaliwa au kukulia Dar es Salaam wanakumbuka sehemu ambazo watoto na mashabiki wengi wa soka walikuwa wanakwenda kuangalia mechi kama vile Uwanja wa Barafu Magomeni, Bonde Mwananyamala, Kinesi Ubungo, UFI Ubungo, Mabibo, Kigogo, Makurumla Magomeni, CCM Magunia Msasani, Shule ya Msingi Mwananyamala, Garden Kinondoni na vingine vingi.

Ilikuwa ni nadra sana mechi hizo kumalizika salama kwa dakika zote 90, kutokana na mazingira yenyewe.

Kwanza mechi zenyewe zilikosa ulinzi wa uhakika, lakini timu nyingi zilikuwa na baadhi ya mashabiki wababe na wenye vurugu. Baadhi ya mashabiki walikuwa wanaona fahari kuanzisha ugomvi mpirani, hata kama hakuna sababu yoyote ya msingi.

Mashabiki wanaweza kukaa nyuma ya goli la timu pinzani na kumtishia kipa kuwa watampiga au kumfanyia kitu kibaya iwapo hatoruhusu bao.

Wakati mwingine kumwagia hata maji ya baridi, au michanga, ili mradi tu kumwondoa mchezoni ili afungwe goli kirahisi.

Ndiyo maana baadhi ya timu zinakuja na mashabiki wake ambao baadhi wanakaa nyuma ya goli la kipa wao kuhakikisha tu hasumbuliwi na wa timu pinzani.

Kupigwa marefa ilikuwa ni jambo la kawaida, labda tu refa huyo awe mbabe, au amekuja na mabaunsa wake, au anachezesha akiwa na silaha. Wachezaji nao walikuwa wakicheza kwenye mazingira magumu kwani mara kwa mara mashabiki wanavamia uwanja kupinga maamuzi ya marefa, au kuwaondoa mchezoni wachezaji wa timu pinzani.

Lakini kwa sasa kuna maendeleo kidogo, mambo hayo kwenye mechi za uswahilini au mchangani yamepungua sana.

Majuzi nimesikia Kamati ya Usimamizi na Uendeshaji wa Ligi, pamoja na mambo mengine ikitoa adhabu kwa baadhi ya timu zinazocheza Ligi Daraja la Kwanza, nikajiuliza kama yale mambo ya vurugu kwenye michezo ya mchangani enzi hizo yamehamia kwenye ligi hiyo!

Klabu ya Stand ilitozwa faini ya Sh. 500,000 kwa kosa la mashabiki wake kufanya vurugu kubwa kwa kurusha mawe kwenye benchi la ufundi la Gwambina FC, lakini pia kuwapiga waamuzi waliosimamia mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga na timu hizo kutoka sare ya bao 1-1.

Lakini klabu ya Gwambina FC, ambayo viongozi wake walishambuliwa na mashabiki wa Stand United, nayo ikatozwa faini kama hiyo ya Sh. 500,000 baada ya mashabiki wake nao kuwashambulia mara kadhaa mashabiki wa Geita FC.

Hapa inaonekana kuwa Ligi Daraja la Kwanza hakuna usimamizi mzuri, na hasa suala la ulinzi, kwani inaonekana timu nyingi zikiwa nyumbani, mashabiki wao wanakuwa watemi kwa kuwapiga wageni. Hii inasababisha nao kujipanga kufanya fujo kwenye mechi ya marudiano.

Kwa maana hiyo huko tunakokwenda kama Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Bodi ya Ligi (TPLB) haitokuwa makini tunaweza kushuhudia maafa kwenye mechi hizo ambazo zinaonekana kabisa usimamizi wake ni mdogo kuliko Ligi Kuu.

Kwenye Ligi Kuu ukiangalia hata adhabu zake zinatofautiana sana na Ligi Daraja la Kwanza.

Utasikia tu, timu haikuingia kwenye vyumba vya kuvalia, kuchelewa kufika na makosa mengine yanayofanana na hayo, lakini ni nadra sana kusikia mashabiki wa timu fulani wamewavamia wa timu nyingine au kuwafanyia vurugu waamuzi.

Ligi Daraja la Kwanza ilipofikia ni pagumu, timu nyingi zinatofautiana kidogo pointi, hivyo zinahitaji kupanda Ligi Kuu, hivyo tutarajie vituko vingi na vurugu kama Bodi ya Ligi haitokuwa makini.

Kwa sasa inabidi iongeze ulinzi, pamoja na waamuzi kuwa makini, pia kuzionya timu zinazofanya fujo uwanjani na ikithibitika zipokonywe tu ushindi.

Hii itasababisha mashabiki wao kuwa makini, na wapo watakaokuwa wanawatuliza wenzao wasifanye fujo kwa sababu wakifanya hivyo tu, basi timu yao inaweza kuzikosa pointi tatu na uwezekano wa kupanda Ligi Kuu usiwepo kabisa.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# 'Treni ya umeme Moro - Dar wakati wowote'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), umefikia zaidi ya asilimia 75 kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro na Watanzania watarajie kuanza kuonja matunda yake wakati wowote mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambaye pia ni Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbasi, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu maendeleo ya SGR.

Alisema serikali inaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya nchi ikiwamo SGR licha ya kelele mbalimbali, ujenzi wake unakwenda kwa kasi.

"Kwa kipande cha Morogoro hadi Makutupora Singida, ujenzi wa reli umefikia zaidi ya asilimia 28 ikijumuisha uwekaji wa nguzo na nyaya za umeme," alisema.

Alisema hadi sasa kiasi cha Sh. trilioni 2.957 kati ya Sh. trilioni saba zimetumika kwenye ujenzi huo na ni fedha za Watanzania.

"Reli tunatekeleza kwasasa vipande viwili licha ya mvua kusumbua kidogo, lakini tunakwenda vizuri, ile ahadi ya serikali kwa Watanzania kupanda treni ya umeme wakati wowote itaanza kukamilika kwa kipande cha Morogoro hadi Dar es Salaam," alisema.

"Kuna watu wamesikia juzi tunachukua mkopo wameanza maneno kwamba mradi umewashinda... brother tulia, usikurupukie hadi sasa tumetumia Sh. trilioni 2.957 fedha za Watanzania."

Dk. Abbasi alisema fedha za mkopo bado hazijafika na endapo zikiingia zitatumika kwenye maeneo yaliyosalia.

"Mwaka huu ile ahadi kwa Watanzania kuonja treni ya umeme baada ya kuziona sana kwenye filamu mbalimbali itakamilika na kila mtu atafurahia walau kuanzia Dar es Salaam hadi Morogoro, kadiri tutakapokamilisha vipande vya mbele ndivyo mtakavyofurahi zaidi," alisema.

Kuhusu kipande cha Mwanza hadi Isaka, Katibu Mkuu huyo alisema miezi mitatu iliyopita Rais John Magufuli aliagiza kipande hicho kimkakati kijengwe ili kuunganisha Rwanda, Kongo na nchi zingine zilizopo kwenye ukanda huo.

"Zabuni itatangazwa wakati wowote ili kumpata mkandarasi atakayejenga SGR, kwa kifupi hakuna kilichosimama, kilichoyumba wala tashititi yoyote kwenye mradi huu," alisema.

Kadhalika, alisema kuanzia leo kutakuwa na ziara muhimu ya siku mbili ya Makatibu Wakuu wa Wizara zote kutembelea utekelezaji wa mradi huo.

"Ziara itaanzia Dodoma kuangalia utekelezaji wa mradi huu wataenda Dodoma hadi Morogoro, na siku ya pili Morogoro hadi Dar es Salaam,"alisema.

Kuhusu mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere, Dk. Abbasi alisema kazi ya kuchoronga handaki la kupitisha maji ya mto, imekamilika kwa asilimia 100.

"Kuweka zege la kuimarisha handaki imefikia asilimia 10 ya ujenzi na hadi Januari 2020, fedha iliyotumika kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere ni Sh. trilioni 1.275 kati ya Sh. trilioni sita," alisema.



Mbunge wa Musoma Vijijini mkoani Mara, Prof. Sospeter Muhongo (kulia), akizungumza juzi na wakazi wa Kata ya Busambara, kwenye hafla ya kuweka jiwe la msingi la Busambara Sekondari iliopo jimboni mwake. **PICHA MPIGA PICHA WETU**

## Vijana hatarini ajali bodoboda, bajaji

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

VIJANA wengi nchini wako kwenye hatari ya kupata ajali za barabarani zinazochangiwa na uendeshaji wa bodaboda na bajaji.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), watoto kuanzia miaka mitano hadi 29, wako katika hatari zaidi kutokana na vijana kujikita katika uendeshaji wa bodaboda na bajaji.

Pia takwimu za WHO zinaonyesha chanzo cha vifo namba nane duniani kinatokana na ajali za barabarani.

Balozi wa usalama barabarani, ambaye pia ni Mkurugenzi wa Shirika la Road Safety Ambassador (RSA), Augustus Fungo, alisema hayo mjini Kibaha, mkoani Pwani wakati wa kuhitimisha sehemu ya mradi wa elimu ya usalama barabarani, kwa shule za msingi na sekondari 12 za mkoani humo.

Alisema mradi huo wa miezi nane ulianza Novemba mwaka 2019 na ulikuwa ukitekelezwa katika mikoa ya Pwani na Kilimanjaro.

Alisema takwimu za WHO zinaonyesha watu 1,350,000 wanapoteza maisha huku zaidi ya milioni 50 wakiachwa na ulemavu wa kudumu duniani. "Kutokana na hali hii tumeanza kutoa elimu na tutaendelea kufanya hivi kuwanusuru vijana ambao wengi wao ni madereva wa bodaboda na bajaji," alisema.

Alisema wanatarajia kutoa elimu hiyo kwa watu wenye ulemavu ili nao watambue sheria za barabarani na kuepuka ajali.

Naye, Kaimu Mkuu wa Usalama Barabarani Mkoa wa Pwani, ASP Africanus Sulle, alisema mafunzo hayo yatasaidia kupunguza ajali hasa kwa wanafunzi ambao wanatumia barabara kuu kuvuka kwenda shuleni.

Alitoa wito kwa wazazi kuwasaidia kuwavusha watoto barabarani badala ya kuwaacha wavuke peke yao.

Alitaja maeneo ambayo alama za zebra zimefutika watashiriki na wakala wa barabara zichorwe upya ili kuepusha wanafunzi na watu wengine kugongwa wanapovuka barabara. Mwanafunzi wa Shule ya Msingi Kongowe, Nyambura Marwa, alisema elimu hiyo imewasaidia kwa kuwa kwa sasa wanaitumia kuvusha wengine na wamefanikiwa kupunguza ajali ambazo zilikuwa zikitokea awali.

# Wawili wafariki dunia kwa kuangukiwa ukuta

**Na Said Hamdani, LINDI**

WATU wawili wamefariki dunia katika mtaa wa Likong'o, Kata ya Mbanja, mkoani hapa kwa kuangukiwa na ukuta wa nyumba walimokuwa wakiishi kufuatia mvua iliyoambatana na upepo mkali.

Watu hao wametambuliwa kuwa ni Rashidi Chande na Hoja Yusufu.

Mvua hiyo pia imeharibu nyumba saba na kusababisha baadhi ya wakazi kukosa mahali pa kuishi.

Taarifa za mashuhuda wa tukio hilo na kuthibitishwa na uongozi wa serikali ya mtaa huo, zinaeleza kuwa limetokea Februari 28, saa 2 usiku. Hamisi Mustafa, Daudi Juma na Omari Yasini, walioshuhudia tukio hilo, wameliambia gazeti hili kuwa mvua iliyonyesha siku hiyo, ikiambatana na radi na upepo mkali, iliezua nyumba saba ikiwamo walimokuwa wanaishi marehemu hao.

Walisema siku ya tu tikio wakazi hao Chande na Yusufu wakiwa ndani ya nyumba hiyo, waliangukiwa na ukuta huo baada ya mvua kunyesha kwa muda wa saa moja, kuezua paa na kubomoa ukuta wa nyumba yao uliowaangukia na kupoteza uhai wao.

"Mvua ilipokuwa inanyesha na upepo mkali waliamua kutoka nje na kuketi barazani, ukuta ukawaangukia na kupoteza maisha yao," alisema mmoja wa mashuhuda hao.

Mwenyekiti wa Mtaa huo wa Likong'o, Rashidi Mikidadi, alithibitisha kutokea kwa vifo vya wakazi hao, na kueleza miili ya marehemu hao imezikwa jana.

Saidi Juma, Diwani wa Kata ya Mbanja, aliyethibitisha kuwapo wa vifo hivyo na kueleza mvua hiyo imeleta hasara ya kuharibu makazi ya watu.

# Kairuki aonyesha viwanda vya kuwekeza

**Na Mwandishi Wetu,**
MWANZA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki, amewataka wawekezaji na wafanyabiashara mkoa wa Mwanza kuchangamkia fursa ya uhaba wa vyakula vya mifugo na mafuta ya kula kujenga viwanda vya kuchakata bidhaa hizo.

Kairuki amesema kwa kufanya hivyo wataondokana na uagizaji wa bidhaa hizo nje ya nchi.

Akihitimisha Mkutano wa Majadiliano kati ya serikali, wawekezaji na wafanyabiashara mkoani Mwanza kujadili changamoto na mapendekezo yanayolenga kuboresha mazingira ya biashara na kuvutia uwekezaji, Waziri Kairuki alisema uwekezaji zaidi unahitajika katika eneo la chakula cha kuku na mafuta ya kula.

"Kuna uhitaji mkubwa wa viwanda vya kuzalisha chakula cha mifugo hasa kwa ukanda wa ziwa ambako kwenye idadi kubwa ya mifugo na uhitaji wake ni mkubwa, hivyo hii ni fursa kwenu kuichangamkia," alisema Waziri Kairuki.

Alisema wizara yake kupitia Kituo cha Uwekezaji (TIC) wamejipanga katika kuziainisha na kuzitambua fursa zote zilizopo ili zitangazwe kuwavutia wawekezaji wenye mitaji kuja kuwekeza ikiwamo kwenye viwanda vya chakula cha mifugo.

"Tupo katika kutekeleza azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025, kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ni sehemu ya kufanikisha azma hiyo," alisema Kairuki.

Alieleza kuwa serikali itaendelea kuwalinda wawekezaji, na wafanyabiashara wa ndani kwa kuhakikisha soko la ndani la bidhaa zinazozalishwa hapa nchini linahimarika na kuchochea ukuaji wa uchumi= kwa kasi inayostahili.

"Lengo letu ni kuachana na uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi jambo ambalo litaongeza ari ya uwekezaji katika viwanda vya kuzalisha bidhaa mbalimbali hapa nchini na kupunguza usafirishaji wa malighafi nje," alisema na kuongeza kuwa ajira zitaongezeka pia.

Aidha, Waziri Kairuki alisema Mkoa wa Mwanza ni moja ya mikoa ya kimkakati, hivyo wizara yake itatoa ushirikiano kwa wawekezaji na wafanyabiashara kwa kuondolea kero zinakwamisha ukuaji na maendeleo ya uwekezaji kwa kuweka mazingira rafiki na wezeshi kwa biashara.

Mwenyekiti wa TCCIA Mkoa wa Mwanza, Leopard Lema, alipongeza majadiliano katika mkutano huu kwa kusema ulikuwa na maana kubwa kwa wawekezaji na wafanyabiashara kwani uliainisha changamoto zote na wahusika ambao ni serikali walitolea majibu au kufanyiwa kazi.

"Tunaimani mapendekezo yetu na changamoto tulizowasilisha kwa viongozi wa serikali zitafanyiwa kazi kwa haraka ili kutoa nafasi kwa

mfanyabiashara na mwekezaji kunufaika na biashara yake na kuongeza hamasa ya kuanzisha viwanda zaidi," alisema Lema.



Naibu Waziri wa Ujenzi ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Elias Kwandikwa, jana, akizungumza na wananchi wa Kitongoji cha Bukindwasali, Kijiji cha Nyamtengela Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga kwenye mkutano wa hadhara kabla ya diwani wa kata ya Idahina, Yuda Majonjos, kusoma taarifa ya utekelezaji wa ilani. **PICHA: SHABAN NJIA**

# TBS yatakiwa kufungua maabara Kanda

**Na Felix Andrew**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limetakiwa kufungua maabara za kanda kwa ajili ya kupima ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini na hatimaye kwenda sambamba na mahitaji ya viwanda.

Wito huo ulitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya wazalishaji wa mafuta ya alizeti na wauzaji wa bidhaa za vyakula na vipodozi jijini hapa.

Alisema TBS inafanya kazi nzuri, lakini inahitaji maboresho zaidi katika utendaji wake ikiwa ni pamoja na kujenga maabara za kanda ambazo zitasaidia kuondoa kero ya ucheleweshaji wa majibu ya sampuli hali inayotokana na ongezeko la mahitaji ya viwanda.

Alisema kwa mkoa wa Dodoma pekee vipo viwanda zaidi ya 3,000 vilivyofunguliwa vinavyohitaji kuhudumiwa na shirika hilo hivyo kuna umuhimu kwenda sambamba na ongezeko la viwanda vinavyoanzishwa hapa nchini, kwa kuzingatia kwamba serikali imejikita katika ujenzi wa viwanda.

Dk. Mahenge alisema shirika linapaswa kuwa na dirisha maalumu la kuwahudumia wawekezaji wakubwa ili kuweka mazingira mazuri na rafiki ya kutoa huduma na kuepuka ucheleweshaji wa aina yoyote.

"Dodoma imejipanga kuweka mazingira yatakayovutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, hivyo TBS ina wajibu wa kuhakikisha kuwa inakidhi matakwa ya viwanda na wawekezaji kwa ujumla," alisisitiza.

Dk. Mahenge alisema mada mbalimbali watakazopatiwa washiriki zitawasaidia kuboresha bidhaa wanazozalisha na kuwa na uhakika wa soko.

Meneja wa Utafiti na Mafunzo, Hamisi Sudi, akimkaribisha mkuu wa Mkoa kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Athuman Ngenya, alisema Shirika limejikita katika kutoa mafunzo kwa wazalishaji wa dogo na wa kati lengo likiwa ni kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu masuala ya viwango na uthibitishwaji ubora wa bidhaa.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2019/2020, shirika limetoa mafunzo katika Kanda ya Magharibi, kanda ya Ziwa na sasa Kanda ya Kati ambapo katika kanda ya kati wilaya zilizonufaika na mafunzo haya ni Iramba, Kondoa,Manyoni, Singida,Kongwa na Dodoma.

Alisema mwitikio wa washiriki katika mafunzo haya umekuwa ni mzuri kwani katika wilaya sita zilizopata mafunzo wadau 489 walishiriki kwa ukamilifu. Shirika linatarajia kuendesha mafunzo kama haya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kaskazini hadi kufikia mwezi Juni mwaka huu.

Katika mafunzo yanayotolewa na TBS kuhusu masuala ya viwango pia hushirikisha wadau kutoka Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), maofisa Afya, Biashara na Maendeleo ya Jamii kutoka katika wilaya husika.

# Ulega atoa neno Sheria ya Uvuvi

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, ameeleza kuwa Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya Mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2009 ipo kwenye hatua ya mwisho ya marekebisho makubwa ili kuendana na wakati kwa kulinda rasilimali za uvuvi, kuzitunza na kuzivuna.

Ulega alisema hayo jijini Mwanza wakati akizungumza kwenye mkutano wa mashauriano kati ya Serikali, wafanyabiashara na wawekezaji wa Mkoa wa Mwanza, na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwemo mawaziri, wataalamu wa sekta mbalimbali pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella.

Alisema moja ya mkakati ni kuona wavuvi wanapata kipato huku ziwa linaendelea na kufanya uvunaji wa rasilimali zake unakuwa endelevu ambapo katika mchakato wa kukusanya maoni uliofanyika mwaka 2019, wavuvi walishirikishwa sana katika kuhakikisha kwamba wanatoa mchango wao wa mawazo ili jambo la uboreshaji wa sheria hiyo iwe nzuri.

"Tupo katika hatua nzuri ndio maana nimewapa matumaini wadau wetu kwa sababu hivi sasa tupo kwenye hatua za mwishoni za marekebisho makubwa ya sheria yetu ya uvuvi na kanuni zake, hivyo mwaka jana tulifanya maboresho ya kanuni, lakini hii tunaifanyia marekebisho makubwa," alisema Ulega.

Akitoa ufafanuzi kuhusu maombi ya wavuvi kuomba kupunguziwa masharti wakati wa kuanzisha na kusajili ushirika wa wavuvi likiwamo la milioni 5, Ulega alisema ushirika ni kwa mujibu wa sheria ambapo jambo la usajili wa ushirika lipo kwa Wizara ya Kilimo, lakini kwa vile wao ni serikali moja wamekuwa wakijadiliana ili kufanya marekebisho ya msingi kabisa ya eneo hilo la vyama vya ushirika hasa vya wavuvi kwa sababu vinaathirika sana na sheria za namna hiyo.

# Brela sasa kunoa maofisa biashara

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

ILI kwenda sambamba na hatua zinazochukuliwa na serikali za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, Wakala wa Usajili wa Majina ya Biashara na Leseni (Brela) imeandaa mafunzo maalum kwa maofisa biashara na viongozi wa chemba za biashara nchi nzima ili kuwajengea uwezo wa kutumia mfumo katika urasimisha wa biashara.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Brela, Godfrey Nyasia, aliwaambia washiriki wa mkutano wa majadiliano kati ya serikali, wawekezaji na wafanyabiashara jijini hapa mwishoni mwa wiki kuwa mafunzo kwa maofisa biashara na viongozi wa chemba za biashara itasaidia kuchochea kasi ya urasimishaji wa biashara nchi nzima.

"Brela kama mdau muhimu katika kufanikisha uboreshaji wa mazingira ya kufanya biashara na kuvutia uwekezaji nchini, tumejipanga mwaka ujao wa fedha kutoa mafunzo maalum kwa maofisa biashara na viongozi wa chemba za biashara mikoa yote ili kuwajengea uwezo wa kuwasaidia wananchi kurasimisha biashara zao," alisema Nyasia.

Nyasia ambaye alikuwa akijibu hoja mbalimbali za wananchi zilizoelekezwa taasisi yake, alisema Brela imeshatoa semina mbalimbali kwa wajasiriamali kuhusu umuhimu wa kurasimisha majina ya biashara zao na kilichobaki sasa ni kuwajengea uwezo zaidi maofisa biashara.

"Tumejipanga kuhakikisha kuwa zoezi la urasimishaji biashara linakuwa endelevu na Brela itaendelea kuhamasisha wajasiriamali kurasimisha shughuli zao," alisema Nyasia na kupongeza mwamko mkubwa wa wafanyabishara kusajili biashara zao.

Pia alisema wakala imeshafanya maboresho makubwa katika utoaji wa huduma zake kwani sasa usajili wa kampuni na majina ya biashara hauhitaji tena mtu kwenda Dar es Salaam ambapo kila kitu kinafanyika kwa njia ya mtandao.

Alisema Brela inafunga mtambo maalum wa mawasiliano ambao utakuwa unatoa msaada kwa mteja kwa muda unaotakiwa tofauti na awali ili kumwondolea mteja changamoto na usumbufu usio wa lazima. "Tumejitahidi kusogeza huduma zetu mikoani na kuendelea kufungua na kuimarisha ofisi zetu za kanda ili kurahisisha zoezi la urasimishaji wa biashara," alisema Nyasia.

Washiriki wa mkutano huo ambao uliongizwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, aliyeambatana na manaibu waziri saba, walipongeza Brela kwa kujipambanua na kuondoa urasimu katika utoaji wa huduma zake.

# Utitiri kodi watawala mkutano wafanyabiashara, wawekezaji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

UTITIRI wa kulipa kodi kwa wafanyabiashara na wawekezaji mkoani Shinyanga, umedaiwa kuwa kero kwao na kusababisha kupata mapato kidogo.

Wengine wamedai kuzifunga baadhi ya biashara na kushuka kiuchumi kutokana na kushindwa kulipa kodi hizo.

Hayo yalibainishwa na Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wa Viwanda, na Kilimo Tanzania (TCCIA), Mkoa wa Shinyanga, Meshack Kulwa, wakati akisoma taarifa kwenye mkutano wa mashauriano kati ya serikali, wafanyabiashara na wawekezaji.

Alisema kero kubwa ambayo wanakabiliana nayo wafanyabiashara na wawekezaji, ni utitiri wa kulipa kodi ambao unasababisha baadhi yao kushindwa kuzimudu kulipa, huku wengine wakifunga na kufungiwa baadhi ya biashara zao sababu ya kushindwa kulipa kodi hizo.

"Kero kubwa ambayo tunayo wafanyabiashara na wawekezaji mkoani Shinyanga, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Anjellah Kairuki), ni kuwapo utitiri wa kodi, hivyo tunachokiomba kwa serikali ni kutuondolea zile kodi ambazo ni kero, ili na sisi tuendelee kufanya biashara tukue kiuchumi na kulipa kodi," alisema Kulwa.

"Pia tunaomba pale kunapotokea mgogoro wa ulipaji kodi, serikali itafutwe suluhu na hata kupitia kwenye chama chetu, na siyo kwenda tu kufunga biashara au kiwanda kisha kutuchafua kwenye vyombo vya habari," aliongeza.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alisema serikali itaendelea kuzifuta kodi, tozo na ushuru ambazo ni kero kwa wafanyabiashara, ili zibaki zile ambazo zinaweza kulipika, na kwamba serikali haiwezi kupata mapato bila kuwapo wafanyabiashara na wawekezaji.

Alisema kwa kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais John Magufuli, wamefuta kodi, tozo na ushuru 168 ambazo zilikuwa kero kwa wafanyabiashara, lakini cha ajabu mapato yamezidi kuongezeka, tofauti na hapo awali kwa sababu walipakodi walikuwa wachache kutokana na ukwepaji uliosababishwa na utitiri huo.

Naye Waziri Kairuki alisema serikali itazishughulikia kero zote ambazo zimetolewa na wafanyabiashara hao likiwamo suala la utitiri wa kodi na tozo mbalimbali, huku akiwataka viongozi wa serikali kufuata taratibu za ufungaji wa biashara, na wafanyabiashara nao walipe kodi kwa hiari.

Pia alitoa wito kwa wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi kwenda kuwekeza mkoani Shinyanga, ambapo kuna fursa nyingi ya viwanda vya nguo, na ngozi, huku akipongeza utengwaji wa maeneo mengi kwa ajili ya uwekezaji.




Ofisa Elimu Sayansikimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Prisca Masenga, akimkabidhi mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Munghaa, Rehema John, taulo za kike zilizotolewa na halmashauri hiyo kwa ajili ya kuwawezesha kujistiri na kuhudhuria darasani salama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chifu wa Wangoni ahimiza utamaduni

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

CHIFU wa kabila la Wangoni Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma, Emmanuel Zuru Gama, amewataka watu wa kabila hilo kuendelea kuenzi tamaduni zilizoanzishwa na mababu zao ili kudumisha mila na desturi ambazo zipo hatarini kutoweka.

Wito huo aliutoa wakati akizungumza kwenye sherehe za kumbukizi za vita ya Majimaji iliyohusisha Wajerumani na wakazi wa maeneo ya Kusini wakiwamo Wangoni mwaka 1905 hadi 1907.

Mashujaa 67 wa Kingoni walinyongwa na 66 kuzikwa kwenye kaburi moja 66, huku Chifu Songea Mbano alizikwa kaburi la pekee yake baada ya kitanzi kudaiwa kukatika mara tatu. Chifu Gama alisema kuwa kumekuwapo na changamoto kwa kizazi cha sasa kuacha tamaduni za makabila yao ambazo zilikuwa zikitumiwa na mababu, jambo ambalo linasababisha kupotea kwa tamaduni hizo na kusananisha kufutika kwa mila na desturi.

Gama alisema vita ya Majimaji ilionyesha uzalendo mkubwa katika Taifa lao, hivyo ni vema watu wakawa wanazitunza kumbukumbu hizo kwa kuzienzi na kuzifuata ili kuendelea kulinda asili ya makabila yao.

Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololet Mgema, ambaye alikuwa mgeni rasmi, alisema huwezi kuitamka Tanzania bila kuwakumbuka mashujaa wa vita ya Majimaji ambao walipoteza uhai wao kwa kulitetea Taifa lao.

Mgema ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, alisema makumbusho hayo yaendelee kuimarisha umoja na mshikamano wa kuendelea kulipenda Taifa.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa, Dk. Noel Luoga, awali akitoa mahudhui ya kumbukizi za vita ya Majimaji, alisema serikali iko tayari kuendelea kufanya utafiti mbalimbali wa kihistoria ikiwamo wa vita ya Majimaji.

Sherehe hizo zilihudhuliwa na machifu kutoka nchi za Malawi na Zambia, walitoa salamu za kuwapongeza mashujaa waliyonyongwa kwa ajili ya kutetea Taifa lao.



# Miradi ujenzi, ukarabati shule yatekelezwa

**Na Allan Isack,** ARUMERU

SERIKALI kupitia miradi ya lipa kutokana na matokeo 'Education Payment for Result' (EP4R), imejenga na kuboresha miundombinu kwenye shule mbalimbali za msingi na sekondari katika Halmashauri ya Arusha DC, wilayani Arumeru mkoani hapa, ili kuboresha miundombinu ya shule.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, Ofisa Habari wa Halmashauri ya Arusha DC, Elinipa Lupembe, alisema kwa kipindi cha miaka minne serikali imejenga na kuboresha miundombinu ya shule za msingi na sekondari. Alisema katika Shule ya Sekondari ya Mlangarini, serikali imejenga madarasa mapya, mabweni ya wanafunzi wa kike na wa kiume, maabara ya masomo ya sayansi pamoja na kukarabati baadhi ya madarasa.

Pia imeipandisha hadhi shule hiyo kuwa miongoni mwa shule za mchepuo wa kidato cha tano na cha sita wilayani humo.

Kadhalika imetoa mamilioni ya fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule hiyo ili iwe na hadhi ya shule za kidato cha tano na sita.

Mwaka wa fedha wa 2016/2017, serikali ilitoa Sh. milioni 250, ambazo zilijenga bweni la wasichana 80, vyumba sita vya madarasa, ukarabati wa maabara tatu za masomo sayansi pamoja na ujenzi wa vyoo vya wanafunzi. Matokeo mazuri ya kidato cha pili na cha nne ya shule hiyo, mwaka wa fedha 2018/19, serikali ilitoa Sh. milioni 110, kwa ajili ya ujenzi wa maktaba na ukarabati wa bwalo la chakula ambalo limekamilika.

Elinipa alisema mpango mkakati wa serikali ni kupandisha kiwango cha taaluma shuleni hapo kwa kuweka mazingira bora ya kujifunzia kwa wanafunzi na ya kufundishia kwa walimu ili kuleta matokeo chanya kwa shule za msingi na sekondari.

Uongozi wa Halmashauri ya Arusha DC, umewataka wananchi na wadau wa elimu, kuunga mkono juhudi za serikali chini ya Rais John Magufuli na serikali ya kuchangia ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya shule za serikali, ili wanafunzi wapate elimu katika mazingira bora na rafiki.



Mbunge wa Viti Maalumu, Catherine Magige, akiongea na wanawake wa Umoja wa Wanawake wa CCM Wilaya ya Arumeru wakati alipofanya ziara ya kutembelea Hifadhi ya Arusha National Park kuhamasisha utalii wa ndani. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wananchi 50,000 kunufaika maji

**Na Allan Isack,** ARUMERU

ZAIDI ya wananchi 50,000 wa vijiji vitano katika Halmashauri ya Arusha DC, wilayani Arumeru mkoani hapa, watarajia kupata huduma ya majisafi na salama, baada ya kukamilika kwa mradi wa maji wa vijiji vitano. Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Ofisa Habari wa Halmashauri hiyo, Elinipa Lupembe, alisema kukamilika kwa mradi huo katika vijiji vitano, utasaidia kutoa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi zaidi ya 50,000 kwenye vijiji vya halmashauri hiyo. Alisema serikali kwa kushirikiana na Idara ya Maendeleo nchini Uingereza (DFID), inatekeleza mradi wa maji wa vijiji vitano kwa lengo la kupeleka huduma ya majisafi na salama.

Vile vile, alisema mradi huo utahudumia wananchi wa vijiji vya Olkokola, Lengijave na vitongoji vya Ngaramtoni, Seuri na Ekenywa katika Mamlaka ya Mji mdogo Ngaramtoni.

Alisema mradi huo, umegharimu kiasi cha Sh. bilioni 8.4, na umesanifiwa kwa kutumia teknolojia ya kuchuja maji, kwa kutumia mitambo ya kuondoa uchafu na kupunguza ongezeko la madini ya Fluoride kwenye maji. Alisema kwa kiasi kikubwa wananchi wa eneo hilo, wameathirika kwa kutumia maji yenye madini ya fluoride.

Pia, alisema kukamilika kwa mradi huo, kutawapunguzia adha wananchi wa vijiji hivyo kutumia maji yenye madini hayo. Mradi huo, unatumia teknolojia ya malipo kabla ya kupata huduma (pre-paid).

Teknolojia hiyo, inatekelezwa na Shirika la eWater ambalo linatarajiwa kutoa huduma kwa zaidi miaka 20. Mradi huo umekamilika kwa asilimia 95 na baadhi ya maeneo, wananchi wameanza kupata huduma ya

# Shirika mradi wa usafi mazingira lapongezwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SHIRIKA la Maendeleo la Uholanzi (SNV), limepongezwa na serikali kutokana na mradi wa maji na usafi wa mazingira, kwa kugawa vifaa vya Sh. milioni 4.8 kwenye kampuni 35 zinazojihusisha na shughuli za usafi wa mazingira katika Jiji la Arusha.

Akizungumza jana jijini hapa, wakati akigawa vifaa hivyo, kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, Katibu Tawala wa Wilaya ya Arusha, David Mwakiposa, alitaja vifaa vilivyotolewa kuwa ni kofia ngumu, mabuti, max, makoti maalum ya kuvaa wakati wa usafi na gloves.

Alisema lengo kubwa la kutoa vifaa hivyo ni wafanyakazi wao hasa wanaojihusisha na unyonyaji wa majitaka kujikinga na maradhi pamoja na kuhifadhi mazingira.

"Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Dk. Maulid Madeni na viongozi wa kampuni hizi, mhakikishe kila atakayepatiwa vifaa hivi, avitumie wakati wa kufanya kazi zao na tutafanya ukaguzi atakayekutwa hajavaa tutamtoza faini ya Sh. 50,000," alisema.

Aliagiza kampuni hizo kuhakikisha anajisajili Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (Nemc) ili ziweze kufanya kazi nchi nzima badala ya Arusha pekee.

Mwakiposa aliomba mradi huo, usaidie jiji hilo, kukarabati vyoo vya umma na kujenga vya mfano ili kuimarisha usafi zaidi kwenye maeneo hayo, ambayo serikali inatamani kuyaimarisha, lakini fedha ni chache kulingana na mahitaji.

Meneja wa mradi huo, Olivier Germain, alisema wametoa vifaa hivyo, wakiamini usafi wa mazingira unapaswa kuanzia kwenye vyoo na wanyonyaji wa majitaka ni wadau muhimu katika kuimarisha usafi wa mazingira na afya za watu.

"Tumegawa vifaa hivi ili watoa huduma watoe huduma yenye viwango kwa kuhakikisha wanaponyonya majitaka hawachafui mazingira kwa kudondosha majitaka ovyo, au wafanyakazi kushika mabomba ya kunyonya majitaka bila kujikinga na chochote," alisema.

Mshauri wa mradi wa maji na usafi wa mazingira kutoka SNV, Saul Mandosya, alisema kuna umuhimu Watanzania wakabadilika kwa kutambua muhimu kuboresha vyoo vyao kwa kusakafia na kunawa mikono baada ya kutoka chooni.

"Tufahamu uhifadhi salama wa takangumu ikiwamo taulo za kike kwa kuepuka kutupa ovyo katika shimo la choo, badala yake zihifadhiwe kwenye vyombo maalum vya taka vyenye mifuniko na unyonyaji salama wa tope kinyesi kabla ya choo kufurika," alisema.





## Udhibiti uuzaji petroli waanza

**Na Ashton Balaigwa**, SAME

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Kanda ya Kaskazini (Uwura), imeanza kutekeleza mkakati wake wa kupunguza na kudhibiti matukio ya moto yanayosababishwa na uuzaji holela wa mafuta ya petroli kwenye mapipa na madumu ya plastiki.

Kibano hicho kinawahusu zaidi wafanyabiashara wa maeneo ya vijijini ambako hakuna vituo vya mafuta.

Meneja wa Ewura, Kanda ya Kaskazini inayojumuisha mikoa ya Arusha, Manyara, Tanga na Kilimanjaro, Mhandisi Lorivil Long'idu, alisema kabla ya kuwabana kisheria wafanyabiashara wa mikoa hiyo wameanza kutoa elimu vijijini. Long'idu alikuwa akizungumza mwishoni mwa wiki katika Wilaya ya Same na wafanyabiashara pamoja na baadhi ya wananchi.

"Chini ya mkakati huu, Ewura Kanda ya Kaskazini, imeanza kutoa elimu kwa wafanyabiashara wa mafuta ya petroli wenye mitaji midogo na wasio na uelewa wa kutosha. Kimsingi tumeanza kutoa elimu na ushauri wa kuwapo kwa ujenzi wa vituo rafiki na vya gharama nafuu katika maeneo ya vijijini.

Alisema kuwa ujenzi wa vituo hivyo unagharimu Sh. milioni 55 ikijumuisha pamoja na mambo mengine ujenzi na vifaa vya kutolewa huduma hiyo.

"Gharama hizo ni ujenzi wa kituo, pampu moja yenye uwezo wa kuuza aina mbili za mafuta, konopi, matangi mawili, kujenga ofisi na choo ambayo inategemea na thamani ya kiwanja katika eneo husika," alisema.

Alisema wameamua kuhamasisha ujenzi huo wa vituo vya gharama nafuu kutokana na mahitaji ya mafuta ya petroli na dizeli kuongezeka hasa maeneo ya vijiji kutokana na kushamiri kwa shughuli za kiuchumi ikiwa pamoja na usafiri wa pikipiki maarufu kama bodaboda. Alisema kutokana na ongezeko la mahitaji ya mafuta maeneo mengi ya vijijini yamebaki kutokuwa na vituo vya mafuta kutokana na wafanyabiashara wa mafuta hasa ya petroli wenye mitaji mikubwa kusita kujenga vituo hivyo vijijini kwa kuona hakuna biashara ya kutosha na hivyo wameamua kuhamasisha sasa wenye mitaji midogo waliopo vijijini.

Naye Ofisa Mwandamizi wa Huduma kwa Wateja wa Ewura, Kanda ya Kaskazini, Evelyne Shundi, akitoa elimu kwa wafanyabiashara wa mafuta pamoja na wananchi, alisema uhifadhi wa mafuta ya petroli kwenye madumu ya plastiki majumbani na kuyauza katika vibanda kwa kutumia chupa na wafanyabiashara hao umekuwa ni hatari kwa afya na usalama wa mazingira kutokana na kuzuka kwa moto.

Alisema yamejitokeza matukio mengi ya moto na kugharimu maisha ya watu na kuharibu mali na kuhatarisha wafanyabiashara hao kuwa katika hatari ya kupata magonjwa ya kansa ya ngozi kutokana na kushika mafuta wakati wa kutoa huduma.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alipongeza Ewura kwa kusaidia kutoa elimu hiyo kwa wananchi pamoja na wafanyabiashara akieleza itasaidia kupunguza matukio ya moto yanayotokana na kuhifadhi mafuta ya petrol majumbani hasa katika maeneo ya vijijini.

# KKKT kudhamini wanafunzi masomo

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fedrick Shoo, amebariki uamuzi wa Dayosisi ya Kaskazini ya kanisa hilo kutoa ufadhili wa masomo ya chuo kikuu kwa kila wanafunzi watatu kutoka kwenye sharika zake kuanzia mwaka wa masomo 2020/21.

Taarifa iliyothibitishwa na Katibu Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini ya kanisa hilo, Arthur Shoo, inaeleza kuwa wanafunzi hao watagharamiwa ada ya masomo katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Stephano Moshi (SMMUCo) katika ngazi ya cheti na stashahada.

Kozi zilizopata ufadhili huo ni fani za Maendeleo ya Jamii, Uhasibu, Uandishi wa Habari na Usimamizi wa Biashara.

Kwa mujibu wa barua ya Katibu Mkuu huyo iliyoandikwa Februari 25, mwaka huu kwenda kwa wachungaji viongozi wa sharika zote za KKKT, Dayosisi ya Kaskazini, uamuzi huo unatokana na chuo hicho kukidhi masharti yote ya Tume ya Vyuo Vikuu nchini (TCU) tangu mwaka jana.

Barua hiyo imeeleza kuwa kukidhi vigezo vya TCU, ni hatua kubwa kwa kanisa hilo na Dayosisi ya Kaskazini. Januari 2, mwaka huu, wazawa wa Moshi takribani 900 wakiwamo wafanyabiashara maarufu wanaoishi ndani na nje ya nchi, walipitisha maazimio 17 watakayoyapigia chapuo mwaka huu ili kuifanya Kilimanjaro kuwa Dubai ya Tanzania.

Maazimio hayo ya kuibadili Moshi, yalipitishwa na wazawa hao wakati wa kikao cha waumini wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini kilichoongozwa na Mkuu wa kanisa hilo nchini, Askofu Dk. Fedrick Shoo.

Moja ya maazimio hayo ni pamoja na suala la kukitangaza Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Askofu Stefano Moshi (SMMUCo) kwa nguvu zaidi na kanisa kuwekeza katika rasilimali watu watakaoweza kuendesha vyuo vyao.




Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Yohana Sintoo (wa pili kulia) na Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Upendo Wella (wa tatu kulia), wakiwa wameshika mfano wa hundi ya zaidi ya Sh. milioni 53 kwa ajili ya kukabidhi vikundi 11 vya makundi maalumu ya jamii juzi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# DED Hai ashtukia mikopo kumtumbua

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Yohana Sintoo, ameruka 'kihunzi' cha kwanza cha Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, kuhusu utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa makundi maalumu.

Akizungumza mwishoni mwa wiki, wakati wa hafla fupi ya kukabidhi hawala (hundi) kwa vikundi 11 vya wanawake, vijana na walemavu, Sintoo alisema hayuko tayari kwa sasa kutumbuliwa kutokana na kushindwa kutekeleza Sheria ya Bunge iliyoanza kutekelezwa rasmi Julai Mosi, 2019.

"Mimi ambaye ni msimamizi wa mapato ya halmashauri, kutokutoa mikopo kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo ni makosa makubwa, kutumbuliwa... ni halali kwa Mkurugenzi. Najinasibu kabisa kwamba ni lazima nitoe mikopo kwa asilimia 100 kwa kile kinachopatikana ili nisitumbuliwe. Sisi hatutaki kelelekelele za kuanza kunyooshewa kidole.

Zaidi alisema: "Utoaji wa mikopo kwa sasa hivi ni sheria kamili ambayo tayari tumeanza utekelezaji wake kuanzia Julai mosi 2019 kwa mwaka wa fedha 2019/20. Kwa hiyo ni takwa la kisheria ambayo imetungwa na Bunge, kwa hiyo ndugu zangu tulewe kwamba sasa hivi tuko kisheria."

Halmashauri hiyo, ilikabidhi mikopo ya Sh. 53,502,904 kwa vikundi 11 ambavyo vimekidhi vigezo na masharti ya kupatiwa mikopo hiyo ya uwezeshaji kiuchumi.

"Kwa upande wa pili ina maana kwamba mkopo huo mwongzo wake utasimamiwa vizuri sana kwa wanaokopeshwa, tukizingatia kwamba mkopo huu haina riba. Ni mkopo ambao umekuwa mlaini sana. Rejesheni mikopo hii haraka iwezekanavyo, kwa mujibu wa mkataba na maelekezo yaliyowekwa ili ukimaliza mkopo wako uwe na uwezo wa kuomba tena," alisema.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, "Ni vizuri kwa mkopo ambao hauna riba kujenga imani kubwa kwa vikundi vyote, naujua uthamani wa pesa hususani kipindi hiki cha Mheshimiwa Rais John Magufuli, ninajua Sh. 10,000, Sh. 20,000 ni pesa nyingi sana. Sh. 10,000 sasa hivi ni mtaji, hata Sh. 5,000 sasa hivi ni mtaji maana inategemea wewe kichwa chako kikoje.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Hai, Upendo Wella, alisema ziko rekodi za makundi hayo za nyuma zinaonyesha baadhi ya wanakikundi wamechukua fedha hizo, lakini hawataki kurejesha.

"Mkifanya hivyo na ninyi maana yake wengine wanaotakiwa kupata matunda haya mnawanyima fursa ya kupata hizi fedha. Kwa hiyo muhimu ni kwamba mkazalishe, mkafanye hizo shughuli za uzalishaji za kiuchumi lakini mwisho wa siku mrejeshe kwa wakati ili na wengine wanufaike kiuchumi," alisisitiza Wella.

Februari 14 mwaka huu, Mghwira aliagiza mamlaka zinazohusika kutomlipa mshahara wa mwezi Februari mwaka huu, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, Zefrin Lubuva, baada ya kushindwa kujibu swali alilomuuliza kuhusu utoaji wa mikopo ya makundi hayo kama sheria hiyo inavyotaka.

NIPASHE JUMATATU MACHI 2, 2020

Nipashe Spotiko




NYOTA 10 WALIOSHINDWA KUTWAA TAJI LA LIGI YA MABINGWA ULAYA UK. 16&17




## ISIKUPITE

BAO alilofunga kinda wa England, Jadon Sancho wakati Borussia Dortmund ikiichapa Freiburg juzi, linamfanya sasa kufunga katika mechi saba mfululizo za nyumbani kwenye Bundesliga, ni Pierre-Emerick Aubameyang (kwa sasa Arsenal), aliyeweza kucheka na nyavu mechi nyingi mfululizo katika klabu hiyo (mechi 11 za nyumbani).

# SIKU YA KUFA NYANI...

Beki wa Liverpool, Virgil van Dijk akimfukuzia winga wa Watford, Ismaila Sarr, kabla ya kuifungia timu yake bao la pili wakati miamba hiyo ya Anfield ikilala kwa mabao 3-0 ugenini, hicho kikiwa kichapo cha kwanza msimu huu kwenye Ligi Kuu England. **HABARI UK. 29**

# SABABU 3 SOUTHGATE ATAMUITA SAKA EURO




**LONDON,** England

HUKU ikiwa imebakia miezi michache kuanza kwa michuano ya Mataifa ya Ulaya, Euro 2020 na si zaidi ya mwezi mmoja kabla ya Gareth Southgate kutangaza kikosi kwa ajili ya mechi za kirafiki dhidi ya Italia na Denmark, joto la ushindani la kuwania namba kwenye kikosi cha England maarufu kama 'Simba Watatu' ni kubwa. Wachezaji kama Jordan Henderson, Raheem Sterling na Harry Maguire wanaonekana kama wasio na shaka na nafasi zao, huku wengine kama Harry Winks na Jadon Sancho wakiwa wameshathibitishiwa nafasi zao baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia msimu huu.

Lakini bado kuna ushindani mkubwa wa namba kwenye kikosi hicho baada ya nyota wangine kuchomoza kwa kasi msimu huu na kinda la Arsenal, Bukayo Saka mwenye umri wa miaka 18, anaonekana kuwa mmoja wao. Hili ni zao la akademi ya vijana ya 'Washikabunduki' hao. Saka amejiimarisha yeye mwenye kama beki mzuri zaidi wa kushoto na amekuwa na kiwango cha kuvutia akifunga mabao mawili na kutoa pasi za mwisho nane katika mashindano yote msimu huu.

Lakini je, Gareth Southgate atatakiwa kumuita mchezaji huyu ambaye ana nafasi ya kuichezea timu ya Taifa ya Nigeria - kucheza kwenye Euro 2020? Hapa tunaangalia sababu tatu kwa nini anatakiwa kumuita kikosini...

**1. ENGLAND INAHITAJI ZAIDI BEKI WA KUSHOTO**

Gareth Southgate ni kocha wa England mwenye bahati ya kuwa na wachezaji wengi wenye vipaji na hivyo kujikuta akiwa na uwanja mpana wa kuchagua wachezaji katika nafasi zote. Lakini pengine nafasi dhaifu zaidi kwa kikosi cha England kwa sasa ni beki ya kushoto. Nyota wa Leicester City, Ben Chilwell amekuwa ndio chaguo la kwanza kwa England katika mechi za hivi karibuni, lakini bado inaonekana anahitaji mtu wa kumsaidia.

Ashley Young - ambaye alikuwa chaguo la kwanza wakati wa Kombe la Dunia mwaka 2018 - amestaafu kucheza soka la kimataifa, huku Danny Rose na Luke Shaw hawajawa kwenye viwango vyao katika misimu ya hivi karibuni. Ryan Bertrand anaonekana kabisa hayupo kwenye rada za Southgate, na hii inamaana kwamba, hakuna msaidizi wa maana wa Chilwell.

Nyota wa Manchester United, Brandon Williams mwenye umri wa miaka 19, anaonekana kujiimarisha msimu huu chini ya kocha, Ole Gunnar Solskjaer, lakini hajawa kwenye kiwango cha kuvutia kama Saka pale Arsenal na kwa kiasi fulani kiwango chake hakimfikii nyota huyo wa Washikabunduki.

Kwa uhakika kabisa Chilwell atakuwa chaguo la kwanza la Southgate kwenye mashindano hayo, maana yake ni kwamba Saka ndiye anayefaa kuwa msaidizi wake kuliko Rose.

**2. KIRAKA**

Kitu cha kufurahisha zaidi kuhusu Saka ni uwezo wake wa kucheza beki ya kushoto kwa ustadi mkubwa wa kupanda na kushuka kwa kasi, lakini hiyo siyo nafasi pekee anayoweza kucheza. Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 18, alitengeneza jina lake kwenye akademi ya Arsenal kama winga wa kushoto 'anayepaa' nafasi ambayo pia alianza kucheza chini ya kocha, Unai Emery msimu wa 2018-19 na pia anacheza kama mshambuliaji. Ni katika mechi za hivi karibuni tu ndio anatumika zaidi kama beki wa kushoto sehemu ambayo nayo ameonyesha kiwango bora kabisa.

Hii maana yake ni kwamba, hili ni chaguo sahihi kwa Southgate katika kikosi cha England kwa uwezo wake wa kucheza nafasi nyingi tofauti. Kwa kumchukua Saka, hatakuwa tu msaidizi wa Ben Chilwell nafasi ya beki wa kushoto, lakini anaweza kumtumia kama mshambuliaji pamoja na wachezaji kama Jadon Sancho na Raheem Sterling pale itakapohitajika.

Ukichukulia hali ya sasa ya majeruhi ya Marcus Rashford na kukosa kupata mechi nyingi za kucheza kwa Callum Hudson-Odoi wa Chelsea - itaweza kumfanya kocha kuwa na nafasi nzuri ya kumchezesha nafasi ya Sterling au Sancho kama wakipata majeruhi au adhabu ya kutocheza.

**3. MBUNIFU WA PASI ZA MWISHO**

Eneo moja ambalo kikosi cha England chini ya Southgate limekuwa likishutumiwa zaidi ni kukosekana kwa ubunifu, hasa, nafasi ya kiungo. Southgate amewajaribu wachezaji kadhaa wa kutengeneza ubunifu kwenye nafasi ya kiungo - Ross Barkley, Dele Alli, Jesse Lingard na Mason Mount - lakini hakuna mmoja kati yao aliyefanikiwa. Na bado England inafunga mabao ya kuvutia hasa wakati wa mashindano ya kufuzu Euro 2020.

Mabao hayo yamekuwa yanakuja kutoka sehemu tofauti hasa kwa juhudi zao washambuliaji kama Marcus Rashford, Raheem Sterling na Jadon Sancho.

Sasa uwapo wa Saka kikosini hapo kunaifanya nafasi ya kiungo kupokea mipira mingi ya kutoka beki ya kushoto na kusukumiza mashambulizi mbele kwa uharaka.

Saka amekuwa akicheza kwa ubunifu mkubwa kama alivyoonyesha kwenye mechi mbili zilizopita za Arsenal kwenye Ligi Kuu. Alicheza vizuri kumzidi maarifa Valentino Lazaro wa Newcastle na kutengeza bao kwa Nicolas Pepe na pia alitengeneza pasi nzuri zaidi kwa Eddie Nketiah aliyefunga dhidi ya Everton.

**JE, WAJUA?**

TANGU kuanza kwa msimu uliopita, ni beki wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold mwenye (pasi za mwisho 24) pekee kwenye Ligi Kuu zaidi ya winga wa Bournemouth, Ryan Fraser (18).



MICHEZO



Ditram Nchimbi (kushoto) wa Yanga akipambana na mmoja wa mabeki visiki nchini, Juma Nyosso wa Kagera Sugar kwenye moja kati ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

# NCHIMBI ANAVYOSOMEKA NDANI YA YANGA, ALLIANCE

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Straika wa Yanga aliyesajiliwa kipindi cha dirisha dogo akitokea Polisi Tanzania, Ditram Nchimbi, ameifungia timu yake hiyo mpya mabao mawili tangu ajiunge nayo.

**Mabao mawili aliyofunga Jumamosi iliyopita dhidi ya Alliance ya Mwanza, yaliiwezesha timu yake hiyo kushinda 2-0, baada ya mechi nne mfululizo za matokao ya sare.**

Nchimbi, alifunga bao lake la kwanza Yanga dakika ya 47 na lingine dakika ya 78 na kufikisha jumla ya mabao sita kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

Straika huyo anayeichezea pia timu ya Taifa, Taifa Stars, alikuwa akiichezea Polisi Tanzania kwa mkopo akitokea Azam FC.

Rekodi zinaonyesha kuwa mabao yote hayo sita aliyoyafunga Nchimbi yana nasaba na timu zilizocheza Jumamosi za Yanga na Alliance...

**MABAO MATATU ALIIFUNGA YANGA**

Kati ya mabao hayo, matatu aliifunga timu yake ya sasa, Yanga, wakati akiichezea Polisi Tanzania, mechi iliyoisha kwa sare ya 3-3 kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Ilikuwa ni mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara Oktoba 3, mwaka jana, Yanga ikitoka sare na Polisi Tanzania kwa mabao 3-3, Nchimbi akipiga 'hat-trick' ya kwanza kwenye ligi msimu huu.

Aliyafunga dakika ya 33, 55 na 57, huku David Molinga akifunga mawili, Mrisho Ngassa moja kwa upande wa Yanga.

**ALIIFUNGA ALLIANCE AKIWA POLISI**

Akiwa bado anaichezea Polisi Tanzania, kabla ya kufunguliwa kwa dirisha dogo la usajili, Nchimbi alifunga bao la tatu kwenye Uwanja wa Ushirika mjini Moshi, akiifunga Alliance FC kwenye mechi ambayo iliisha kwa Maafande hao kutoka uwanjani na ushindi wa bao 1-0, Novemba 2, mwaka jana.

Bao hilo alilifunga dakika ya 59 na kuwa ni la mwisho kwa timu yake ya zamani ya Polisi Tanzania, kabla ya kutimkia Yanga.

**KAIFUNGA TENA ALLIANCE AKIWA YANGa**

Mara ya mwisho Nchimbi kufunga bao kwenye Ligi Kuu, ilikuwa ni mechi ya mzunguko wa kwanza timu yake ya Polisi Tanzania ikicheza dhidi ya Alliance, lakini sasa ameifunga tena Alliance akiwa na Yanga, ikiwa ni mabao yake ya kwanza tangu ajiunge na timu hiyo.

Kwa maana hiyo mabao yote sita ya Nchimbi, matatu ameifunga timu yake ya zamani Yanga, na matatu amefunga Alliance FC. Amezifunga timu mbili tu kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

**NCHIMBI NI NANI?**

Ni straika mzoefu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, akiwa amezichezea klabu mbalimbali ikiwamo Njombe Mji, Majimaji ya Songea, Mwadui FC, Azam, Polisi Tanzania na hatimaye Yanga.

Msimu uliopita alifunga mabao manne akiwa na klabu ya Mwadui FC, msimu wa 2017/18 akimaliza msimu akiwa na jumla ya mabao mawili, akiichezea Njombe Mji, msimu wa 2016/17 alimaliza na mabao manne akiwa na klabu ya Mbeya City.

Msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2015/16 alifunga mabao matatu, akiifungia bao moja Majimaji, kabla ya kusajiliwa kupindi cha dirisha dogo kuelekea Mbeya City ambako alimaliza akiwa na mabao mawili.

Kwa maana hiyo ana mabao 19 mpaka sasa tangu mwaka 2015, alipoanza kuchezea Ligi Kuu akiwa na klabu ya Majimaji ya Songea.

Ni mmoja wa wachezaji walioifungia timu ya taifa bao dhidi ya Sudan lililoifanya Tanzania kufuzu kwenye michuano ya fainali za Afrika kwa Wachezaji Wanaocheza Ligi ya Ndani (CHAN) inayotarajiwa kuchezwa mwezi ujao nchini Cameroon.

**NJE YA UWANJA**

KIPIGO cha mabao 2-1 Arsenal ilichokipata dhidi ya Olympiakos wiki iliyopita, kinaifanya kupoteza nyumbani mfululizo kwenye michuano hiyo ya Ulaya kwa mara ya kwanza tangu Februari/Septemba 2015 kwenye Ligi ya Mabingwa.



# NYOTA 10 WALIOSHINDWA KUTWAA TAJI LA LIGI YA MABINGWA ULAYA


IBRAHIMOVIC

**LONDON,** England

MICHUANO ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hukutanisha wachezaji wakali na huacha kumbukumbu isiyofutika.

**Michuano hiyo inatoa nafasi ya kushuhudiwa wachezaji kutoka sehemu mbalimbali duniani wakipambana kuwania taji hilo kubwa zaidi kwa ngazi ya Klabu barani Ulaya.**

Winga wa zamani wa Real Madrid, Paco Gento aliweza kutwaa taji hilo mara sita wakati wa kipindi chake cha uchezaji akiwa na miamba hao wa soka la Hispania kati ya mwaka 1962 na 1971. Wachezaji Cristiano Ronaldo, Paolo Maldini na gwiji Alfredo di Stefano wametwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tano kwa kipindi chao cha uchezaji (huku Ronaldo bado akiendelea kucheza). Hapa tunawaangalia wachezaji 10 bora ambao hawajawahi kamwe kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya...

### 1. LAURENT BLANC
Amecheza kwa kipindi cha miaka 20, mlinzi Laurent Blanc ametwaa mataji mengi kwa kipindi chake cha uchezaji kwenye ngazi ya klabu na timu ya Taifa ya Ufaransa.

Akiwa na timu ya Ufaransa amewahi kutwaa Kombe la Dunia mwaka 1998 pamoja na lile la Mataifa ya Ulaya mwaka 2000. Lakini kamwe hakuweza kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Blanc aliweza kushinda taji la Washindi Ulaya (sasa Ligi ya Europa) akiwa na Barcelona mwaka 1997, lakini alikaribia kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2001/02 akiwa na Manchester United. Ndoto yake ya kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya chini ya kocha, Sir Alex Ferguson iliishia nusu fanali wakati wakitolewa na Bayer Leverkusen.

### 2. RUUD VAN NISTELROOY
Ruud van Nistelrooy alikuwa mmoja wa wafungaji bora zaidi kwenye mchezo huo wakati wake wa uchezaji.

Akiwa ameanza kucheza soka kwenye Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie, akahamia Manchester United mwaka 2001 akicheza chini ya Sir Alex Ferguson. Kama ilivyo kwa Laurent Blanc, van Nistelrooy hakuweza kutwaa taji hilo akiishia kwenye nusu fainali waliyotolewa na Bayer Leverkusen mwaka 2002.

Baada ya miaka mitano ya kukaa pale Old Trafford, akaenda kujiunga na Real Madrid, lakini hakuweza kubeba taji hilo licha ya kuwahi kuibuka mfungaji bora katika misimu mitatu tofauti.

### 3. PAVEL NEDVED
Nafasi ya Pavel Nedved kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya ilikuja msimu wa 2002/03.

Kiungo huyo alikuwa na Juventus wakati walipokutana na AC Milan kwenye fainali pale kwenye Uwanja wa Old Trafford. Baada ya sare ya bila kufungana mchezo ukaenda kipindi cha dakika za nyongeza na baadaye mikwaju ya penalti na Juventus ikafungwa 3-2.

Msimu huo ulimalizika kwa Nedved kushinda tuzo ya Ballon d'Or, ambayo angalau ilipunguza machungu ya kukosa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

### 4. GIANLUIGI BUFFON
Bila shaka yoyote Gianluigi Buffon ni mmoja wa makipa bora zaidi kuwahi kutokea kwenye mchezo wa soka, lakini kwa kipindi chake chote hicho hadi sasa hajaweza kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mshindi huyu wa Kombe la Dunia na timu ya Taifa ya Italia mwaka 2006, amecheza fainali tatu tofauti za Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini hajawahi kutwaa taji hilo.

Mwaka 2003, akiwa na Juventus alifungwa kwenye fainali dhidi ya AC Milan na mwaka 2015 akafungwa na Barcelona. Huku mwaka 2017 akifungwa na Real Madrid.

### 5. MICHAEL BALLACK
Michael Ballack amecheza Ligi ya Mabingwa Ulaya na klabu tatu tofauti. Raia huyo wa Ujerumani ametinga fainali na klabu mbili tofauti, Bayer Leverkusen mwaka 2002 na Chelsea mwaka 2008, na zote walifungwa kwenye fainali na hakuweza kulibeba taji hilo hadi anastaafu kucheza soka.

### 6. ZLATAN IBRAHIMOVIC
Zlatan Ibrahimovic anachukuliwa kama mmoja wa wafungaji bora zaidi kwenye mchezo huu. Hata hivyo, katika kipindi chake cha uchezaji hajawahi kulitwaa taji hilo.

Raia huyo wa Sweden amecheza katika klabu tatu kubwa za Italia; Juventus, AC Milan na Inter Milan, lakini katika zote hizo hakuwahi kulibeba taji hilo.

### 7. FRANCESCO TOTTI
Fowadi wa Italia Francesco Totti amecheza soka kuanzia mwaka 1992 hadi alipostaafu mwaka 2017 na mara zote atakumbukwa kama mchezaji ambaye aliamua kutumia kipindi chake chote cha maisha ya kucheza soka akiwa na AS Roma.

Totti alipata kila kitu akiwa pale Roma, lakini hakuweza kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

### 8. ROBERTO BAGGIO
Roberto Baggio alikuwa mmoja wa viungo washambuliaji waliozawadiwa kipaji cha ukweli katika mchezo huu wa soka.

Licha ya kutawala kwenye timu za Ligi Kuu ya Italia na kimataifa kwa miaka mingi, lakini hakuweza kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Baggio alifunga mabao 27 katika mechi 57 timu ya taifa ya Italia na alitwaa taji la Uefa (sasa Ligi ya Europa) akiwa na Juventus mwaka 1993.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Italia, alishinda taji la Ligi Kuu ya Italia, Serie A, mara moja na alishinda Kombe la Dunia mwaka 2006 akiwa na Italia, lakini ameikosa medali moja tu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

### 9. LOTHAR MATTHAUS
Lothar Matthaus alikuwa kiungo aliyebarikiwa kipaji na mchezaji bora zaidi kwa kizazi chake, akishinda mataji saba ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, na manne ya DFB-Pokal (Kombe la Ujerumani) akiwa na Bayern Munich. Matthäus alikuwa kwenye kikosi cha Ujerumani kilichotwaa taji la Ulaya mwaka 1980 na miaka kumi baadaye aliongeza taji la Dunia.

Lakini kwa kipindi chake chote cha uchezaji, hakufanikiwa kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

### 10. RONALDO
Mmoja wa washambuliaji bora zaidi kwenye historia ya mchezo wa soka. Ronaldo aliweza kubeba mataji mengi likiwamo Kombe la Dunia, lakini kamwe hajawahi kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku akilishuhudia tu kwenye televisheni.

Katika msimu wa 1996/97, wakati anaichezea Barcelona, Ronaldo alishinda Kombe la Washindi Ulaya (sasa Ligi ya Europa) wakati timu yake ilipoifunga Paris Saint Germain 1-0 na yeye ndiye akiwa mfungaji wa bao hilo dakika ya 38.

Baada ya msimu mmoja pale Nou Camp, alihamia kwa miamba wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Inter Milan. Katika msimu wake wa kwanza kwenye soka la Italia, alishinda Kombe la Uefa akifunga moja ya mabao kwenye fainali wakati wakiibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Lazio.

Ronaldo alikaribia kulishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati aliposaini kuichezea Real Madrid mwaka 2002.

Lakini walitolewa na Juventus kwenye nusu fainali, huku mchezo wa kwanza wakishinda 2-1 pale kwenye dimba la Bernabeu na wa marudiano kule Turin wakachezea kichapo cha mabao 3-1.

## Nukuu

"Nadhani Liverpool inayo wachezaji sita wa daraja la juu duniani. Nadhani wanaye kipa Alisson, Trent Alexander-Arnold, Virgil van Dijk, Sadio Mane, Roberto Firmino na Salah. Nadhani kama ukiwauliza mashabiki wa Liverpool endapo watachukua kiasi kikubwa cha fedha kwa wengine watano, wote watasema hapana, haijalishi ni kiasi gani cha fedha. Lakini kama utawapa ofa ya pauni milioni 130 kwa Salah, wanaweza kulifikiria hilo," **Nguli wa zamani wa Liverpool, Jamie Carragher**



"Miguu yangu haikuwa na nguvu kuanzia mwanzo wa pigano, na katika raundi ya tatu miguu yangu ilikosa nguvu katika kipindi chote," **Bondia wa Marekani, Deontay Wilder (pichani) akilaumu vazi alilovaa na kuingia nalo ndani ya ulingo kama sababu iliyomfanya kupoteza taji lake la WBC katika uzani mzito zaidi duniani dhidi ya Muingereza Tyson Fury.**



"Kama hatutashinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, kila mtu atasema tumefeli katika muda wetu tuliotamba. Kwa sababu hicho ndicho kitu ambacho bado hatujakibeba," **Kiungo wa Manchester City, Kevin de Bruyne akiwaambia wachezaji wenzake.**



# MAKOCHA WA KIRUNDI WANAVYOITEKA LIGI KUU BARA



NDAYIRAGIJE

Na Adam Fungamwango

MIAKA mingi iliyopita, Tanzania ikuwa ikipokea makocha wanaofundisha mpira wa miguu kutoka nchi mbalimbali duniani, lakini kwa kiasi kikubwa wengi walitokea Ulaya ya Mashariki. Hii ilitokana na siasa za wakati huo ambazo ni za Kijamaa.

**Simba iliwahi kufundishwa na makocha kama Dimitar Samsarov kutoka Burgaria miaka ya '80 ambaye baadaye alikwenda kuifundisha Majimaji, Dragan Popadic ambaye wakati huo nchi yake iliitwa Yugoslavia, lakini sasa ni Serbia na wengine wengi.**

Yanga pia ilishawahi kufundishwa na makocha Rudi Gutendorf kutoka Ujerumani Mashariki na wengine wengi. Hata miaka ya 2000, makocha wengi wa kigeni waliokuja ni kutoka Serbia na nchi nyingine zinazofanana na hizo.

Kwa miaka ya hivi karibuni kunaonekana kumekuwa na mageuzi makubwa ya makocha nchini Tanzania. Makocha wengi wa Kiafrika kwenye nchini Tanzania walikuwa wakitoka Uganda, Kenya na DR Congo, lakini kwa sasa nchi ya Burundi imeonekana kuteka soko la makocha nchini.

Taarifa zinaeleza kuwa ni kutokana na sera na nchi ambayo kwa sasa inachukua wachezaji wanaostaafu soka na wengine na kuwapeleka nchini Ufaransa kuwasomesha kwa makubaliano ya nchi hizo mbili.

Burundi kwa sasa inaonekana kuvuna makocha wengi ambao wamesambaa sehemu mbalimbali Afrika na si Tanzania tu pekee.

Nchini Sudan Kusini, Sudan, Eritrea, Somalia na hata Ethiopia kuna idadi kubwa ya makocha wa Burundi ambao wanakwenda kutafuta maisha na kutengeneza wasifu wao wa nchi yao.

Nchini Tanzania, tayari makocha wa Burundi wameshaanza kuaminika na klabu nyingi sasa pamoja na timu ya Taifa, Taifa Stars imekuwa na makocha kutoka nchini humo.

Inawezekana kabisa msimu ujao wakaongezeka tena, baada ya klabu nyingi licha ya kugundua kuwa ni wazuri kwenye kufundisha, lakini hawana gharama kubwa na wanaweza kufundisha kwenye mazingira yoyote, hata magumu.

Kwenye makala haya, mwandishi ameorodhesha baadhi ya makocha Warundi ambao wamemiminika nchini kufundisha klabu mbalimbali, ikiwamo Taifa Stars...

**1. ETIENNE NDAYIRAGIJE (TAIFA STARS)**

Kwa sasa ndiye Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars. Na huyu ndiye tunaweza kumwita ni baba wa makocha wote wa Kirundi hapa Bongo kwa sasa amewafungulia njia.

Ndayiragije ambaye akiwa Burundi amewahi kuifundisha Vital'O, alianza kujulikana Tanzania alipoifundisha timu ya Mbao FC, iliyoingia Ligi Kuu msimu wa 2016/17 na kuwa tishio.

Mwaka 2018, alichukuliwa na klabu ya KMC nayo pia akaifanya timu ngumu kufungika, kabla ya Azam FC kumchukua mwaka jana.

Hata hivyo, hakukaa muda mrefu kabla hajatemwa kutokana na muda mwingi kuutumia akiwa na timu ya Taifa Stars kwa kuazimwa. Azam ilipomtema tu, akalamba mkataba Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kuifundisha rasmi Taifa Stars hadi leo.

**2. MASOUD DJUMA (SIMBA)**

Huyu ni kocha Mrundi aliyetua Simba na kukaa kwa muda mfupi, lakini hadi leo ameendelea kuwa kipenzi cha wanachama na mashabiki wa klabu hiyo.

Mwaka 2018, Simba ilimtambulisha kocha huyo na kwa muda mfupi aliokaa, alifanya mambo makubwa yaliyowakosha Wanasimba.

Hata hivyo, inasemekana hakuwa na maelewano mazuri na mabosi wake, Pierre Lechatre na hata aliyekuja baadaye Patrick Aussems kwa sababu yeye alikuwa msaidizi, ikisemekana kuwa alikuwa akiutaka Ukocha Mkuu.

**3. HITIMANA THIERY (NAMUNGO FC)**

Ni kocha Mrundi ambaye kwa sasa ameanza kuwa maarufu kutokana na kuifanya Namungo FC, klabu iliyopanda msimu huu kuwa ya kuogopwa na wapinzani wake inaokutana nao.

Hitimana ni kocha wa zamani wa Biashara United aliyokuwa akiifundisha mwaka 2018, na kisha kutimkia Namungo FC kabla haijapanda Ligi Kuu kuchukua mikocha ya Mtanzania Fulgence Novatus ambaye kwa sasa anaifundisha Gwambia FC.

Hadi makala haya yanaandaliwa Namungo yenye maskani yake mkoani Lindi ilikuwa kwenye nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**4. RAMADHANI NSANZURWIMO (SINGIDA UNITED)**

Pamoja na kwamba timu yake inakamata nafasi ya mwisho kwenye Ligi Kuu, lakini Ramadhani Nsanzurwimo ni mmoja wa makocha waliootokea kuwa bora nchini Tanzania.

Alishawahi pia kuifundisha Mbeya City na timu kadhaa za Ligi Kuu, hivyo kwa sasa amekuwa mwenyeji na anazunguka kwenye klabu mbalimbali nchini.

Huenda hata msimu ujao, Mrundi huyu anaweza kusikia yupo kwenye klabu nyingine ya Ligi Kuu.

**5. HARUNA HARERIMANA (KMC)**

Ni Mrundi mwingine aliyeingia nchini siku za hivi karibuni na kuifundisha Lipuli ya Iringa.

Ni baada ya Selemani Matola kwenda Polisi Tanzania. Haruna Hererimana akaifanya Lipuli kuendelea kuwa tishio kwenye Ligi Kuu. Kufanya kwake vema kuliwafanya viongozi wa KMC kummezea mate na hatimaye kumchukua kwenye kikosi chao.

Ni baada ya KMC kuonekana maji yamezidi unga kwenye ligi, ingawa bado hajaweza kuiweka timu hiyo kwenye 'reli' inavyotakiwa.

**6. NZEYIMANA MAILO (LIPULI FC)**

Majuzi tu, Lipuli nayo ikaona isiwe tabu. Baada ya kuchukuliwa kocha wao Hererimana, Ikaenda tena nchini Burundi na kumshusha kocha mwingine Nzeyimana Mailo ili kuchukua nafasi yake.

Tayari kocha huyo ameanza kazi yake kwenye timu yake mpya na kufanya idadi ya makocha wa Kirundi kuzidi kutamalaki kwenye ardhi ya Bongo.

**NAJUA WAJUA**

WATFORD FOOTBALL CLUB

WATFORD ni timu ya kwanza kuifunga Liverpool kwenye Ligi Kuu tangu Manchester City ilipofanya hivyo Januari 2019, hivyo kuhitimisha safari yao ya kushinda mfululizo (mechi 18), lakini nafasi ya pili ya kutokupoteza ya (mechi 44) katika historia ya Ligi Kuu England.

SOKA

# KWA NINI NI WAKATI WA UTD KUMUUZA POGBA?




**MANCHESTER,** England

MAJALIWA ya Paul Pogba yanaendelea kutawala vyombo vya habari wakati kiungo huyo akiwa anajaribu kurudi kutoka chumba cha majeruhi. Kuna ripoti kwamba, Mfaransa huyo atarudi dimbani wakati wa mchezo wa 'dabi' kwa timu za jiji moja, Manchester United dhidi ya Manchester City, Machi 8 mwaka huu, lakini tayari mashabiki wa United wamegawanyika kuhusu majaliwa ya Pogba. Wengine wanaamini kwamba Mfaransa huyo anaondoka hapo Old Trafford.

**Huku mashabiki wengine wakiona kwamba Pogba ndiye kiungo mwenye kipaji zaidi hapo Old Trafford kwa sasa, kocha Ole Gunnar Solskjaer anaonekana kuwa kwenye mkanganyiko juu ya hatima ya mchezaji huyo.**

Kwa upande mwingine, wakala wa mchezaji huyo, Mino Raiola anaonyesha nia ya wazi kwamba mchezaji huyo anaondoka. Kauli zake za hivi karibuni kwamba Juventus ni kama "nyumbani" kwa Pogba kunafanya mkanganyiko kuwa mkubwa zaidi.

Makala haya yanachambua sababu tatu kwa nini Manchester United ni bora ikamuuza Pogba kipindi kinachokuja cha majira ya joto...

**3. POGBA HANA MORALI KUICHEZEA UNITED**

Wakati wa kipindi cha majira ya joto kilichopita, Pogba alisababisha taharuki, wakati alipobainisha mpango wake wa kutaka changamoto mpya. Ilitarajiwa kwamba, Mfaransa huyo alikuwa tayari kuondoka kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili, huku Real Madrid na Zinedine Zidane wakionyesha wazi kabisa kumtaka.

Pogba pia alionyesha nia yake ya kucheza chini ya kocha huyo wa Real Madrid, lakini uhamisho huo haukufanikiwa na Pogba akaendelea kuwa mchezaji wa United.

Tangu hapo, Mfaransa huyo amecheza mechi nane tu kwa 'Mashetani Wekundu' hao ambapo sita kazi ya hizo akianza. Pogba hatarajii kurudi uwanjani hadi Machi na kuna ishara kadhaa zinaonyesha kuwa mchezaji huyo hana hamasa wala morali ya kuichezea Manchester United.

**2. MKATABA UNAISHA 2021**

Mfaransa huyu atatimiza umri wa miaka 27 mwezi huu, na sasa anakaribia kuingia mwaka wake wa mwisho kwenye mkataba wake. Mkataba wa Pogba na United unamalizika kipindi cha majira ya joto 2021, lakini Mashetani Wekundu hao wana kipengele cha kumwongeza mwaka mmoja. Na hali ilivyo kwa sasa hakuna ishara kama Pogba atakuwa tayari kuongeza mkataba wake na United, maana yake ni kwamba, United wanatakiwa kumuuza.

Ukweli ni kwamba, Man United watapata kiasi kikubwa cha fedha kama wakimuuza Pogba ambaye bado anawaniwa na Real Madrid pamoja na klabu yake ya zamani ya Juventus.

Pogba asipouzwa sasa kuna hatari Mashetani Wekundu hao kumpoteza kwa kuondoka akiwa mchezaji huru mara tu mkataba wake utakapomalizika.

**1. MAUZO YAKE YATASAIDIA USAJILI**

Msimu huu umekuwa wa kufungua macho kwa Manchester United.




Huku kiungo wake huyo akiwa bado majeruhi kwa zaidi ya nusu ya msimu, Solskjaer amekuwa akihaha kutafuta matokeo mazuri uwanjani.

Ni wazi kwamba, Manchester United itahitaji kufanya usajili wa wachezaji wakati wa kipindi cha majira ya joto kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake. Tayari wamemsajili Bruno Fernandes ambaye ameshathibitisha ubora wake.

Hivyo, kama Man United wakimuuza Pogba itawasaidia kupata fedha za usajili wakati wa kipindi cha majira ya joto kijacho, hasa ikizingatiwa kwamba, hatauzwa kwa bei ndogo, hivyo kiasi cha fedha watakachopata kitawapa nafasi nzuri ya kufanya usajili wa wachezaji wakubwa.

Pogba ambaye alitua hapo Man United kwa ada iliyoweka rekodi ya duniani, mwenyewe tayari ana nia ya kutaka kuondoka, hivyo ni nafasi nzuri zaidi kwa Man United kujipanga na kuhakikisha wanapata faida kwa mauzo yake

USHINDI wa Watford wa mabao 3-0 dhidi ya Liverpool ndio mkubwa zaidi kwa timu iliyopo kileleni mwa Ligi Kuu England kufungwa na timu iliyopo ukanda wa kushuka daraja, tangu Leicester ilipoichapa Manchester United 3-0 Novemba 23, mwaka 1985.



NDANI YA 18



MICHUANO ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hukutanisha wachezaji wakali na huacha kumbukumbu isiyofutika. Michuano hiyo inatoa nafasi ya kushuhudiwa wachezaji...

Uk. 16&17



# MAMBO YATAKAYOAMUA KINARA BALLON D'OR 2020

**GENEVA,** Uswisi

TUZO ya Ballon d'Or ni moja ya zawadi bora zaidi kwa wachezaji na kila mwanasoka ana ndoto ya kuibeba siku moja. Lionel Messi na Cristiano Ronaldo wametawala tuzo hiyo kwa kupokezana kuitwaa kwa kipindi cha muongo mmoja, na kwa jumla yake wakitwaa mara 11.

Hata hivyo, mwaka huu, wawili hao wanakabiliwa na ushindani mkubwa zaidi msimu huu kutokana na viwango vya timu zao za Barcelona na Juventus kweye mashindano ya Ulaya.

Tofauti na misimu iliyopita tuzo hiyo ilikuwa inaamuliwa na kiwango cha Messi na Ronaldo, lakini msimu huu mambo ni magumu kwao kwani wachezaji wengi wameibuka na wanaonekana wako fiti na wana 'njaa' kweli ya kuitwaa tuzo hiyo.

Makala haya yanakuchambulia mambo matatu yatakayoamua mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or msimu huu...

**3. KIWANGO CHA RONALDO, MESSI**

Tuzo ya Ballon d'Or kwa kipindi cha miaka 12 iliyopita ilikuwa chini ya Messi na Ronaldo. Na sasa ni rahisi kusema kwamba, kiwango cha wachezaji hao msimu huu na klabu zao kwenye mashindano ya Ulaya kitakuwa na matokeo makubwa zaidi kwenye upigaji kura kwa washindi.

Mwaka huu Ronaldo na Messi wameachwa nyuma kwenye mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu kwa ufungaji bora katika ligi tano kubwa Ulaya, huku kwa sasa wakiwa nafasi ya tatu na sita kwenye orodha. Pia kiwango watakachoonyesha kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, nacho kina nafasi kubwa zaidi kuamua mshindi wa tuzo hizo.

**2. KIATU CHA DHAHABU ULAYA**

Tuzo ya mshindi wa Ballon d'Or huwa pia inaangalia kiwango cha mchezaji husika dhidi ya wachezaji wengine na mabao aliyoyafunga. Mchezaji ambaye atafunga mabao mengi katika timu yake na kuibuka mfungaji kwenye ligi ya nchi anayocheza anajiweka kwenye nafasi nzuri zaidi.

Kama historia inavyoonyesha, tuzo hii inawapa nafasi kubwa zaidi washambuliaji dhidi ya walinzi.

Kiatu cha Dhahabu Ulaya ni tuzo inayotolewa kwa mfungaji bora katika ligi tano kubwa Ulaya, na tuzo hiyo inampa nafasi kubwa zaidi mchezaji kuwa kwenye nafasi ya kutwaa Ballon d'Or.

Messi alishinda Ballon d'Or na Kiatu cha Dhahabu Ulaya mwaka huo huo mara tatu, wakati Ronaldo alishinda hivyo mara mbili. Ingawa kuibuka mfungaji bora si kigezo cha kutwaa Ballon d'Or, lakini inamuweka mchezaji kwenye nafasi nzuri zaidi.

Kwa sasa mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu Ulaya zipo kati ya Ciro Immobile wa Lazio na Lewandowski wa Bayern Munich ambao wanaongoza kwa kufunga mabao katika ligi tano kubwa Ulaya. Maana yeke mwisho wa msimu kutakuwa na ushindani mkubwa katika kuwani tuzo ya Ballon d'Or.

**1. MICHUANO YA KIMATAIFA - EURO 2020, COPA AMERICA 2020**

Kila mchezaji ana ndoto ya kushinda taji kwenye mashindano ya kimataifa. Mafanikio ya mchezaji mmoja mmoja kwenye timu zao za taifa kunampa nafasi kubwa ya kuwa kwenye mbio za kutwaa Ballon d'Or.

Mwaka huu kutakuwa na mashindano makubwa mawili ya kimataifa kipindi cha majira ya joto. Kombe la Mataifa ya Ulaya, Euro 2020 na mashindano ya mataifa ya Amerika Kusini, Copa America- ambapo itashuhudiwa wachezaji wakubwa wakiwakilisha mataifa yao.

Ukiacha Ronaldo na Messi, pia tutawashuhudia wachezaji kama Kylian Mbappe, Lewandowski, Neymar na Van Dijk wakizipigania nchi zao katika mashindano hayo. Hivyo, mchezaji atakayeiwezesha timu yake kutwaa mataji hayo atakuwa na nafasi kubwa ya kulibeba taji la Ballon d'Or.

**USILOLIJUA**



TANGU amejiunga na Arsenal Februari 2018, Pierre-Emerick Aubameyang amefunga mabao 61 katika mashindano yote, ni Mohamed Salah (64) pekee anayeweza kumpiku kati ya wachezaji wa Ligi Kuu England.





Baadhi ya madereva na makondakta wa malori yanayosafirisha viazi kutoka Kikondo wilayani Mbeya wakichimba barabara ili kuwezesha magari yao kupita baada ya kunasa kwenye matope kwa zaidi ya wiki moja katika kijiji cha Igoma barabara ya Mbeya - Makete kupitia Isyonje.
**PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wanaobadili fedha za kigeni mitaani Tunduma kukiona

**Na Nebart Msokwa,** TUNDUMA

SERIKALI wilayani Momba, Mkoa wa Songwe imetangaza kuanza kuwachukulia hatua za kisheria wafanyabiashara watakaoendelea kufanya biashara haramu ya kubadili fedha za kigeni mitaani katika mpaka kati ya Tanzania na Zambia, mjini Tunduma.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya ya Momba, Juma Irando, wakati wa uzinduzi rasmi wa urasimishaji wa matumizi ya Shilingi na Kwacha katika miji ya kibiashara ya Tunduma kwa upande wa Tanzania na Nakonde kwa upande wa Zambia.

Urasimishaji wa matumizi ya fedha hizo ulifanywa kwa ushirikiano kati ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na Benki Kuu ya Zambia (BoZ), katika eneo la Kituo cha Pamoja cha Forodha cha Tunduma (One Stop Border Post) na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali za nchi hizo mbili.

Irando alisema baada ya matumizi ya fedha za nchi zote mbili kurasimishwa, hakuna mfanyabiashara anayeruhusiwa kuendelea kufanya biashara hiyo ya kubadili fedha mitaani na badala yake kazi hiyo itafanywa na benki pamoja na maduka ya kubadili fedha yaliyosajiliwa. "Kuanzia sasa tutaanza kuendesha operesheni maalumu ya kuwaondoa wote wanaofanya biashara hii kienyeji, elimu imetolewa ya kutosha maana huu mpango ulianza tangu mwaka jana na sasa atakayekamatwa sheria itachukua mkondo wake," alisema Irando.

Alisema wafanyabiashara wanaotaka kuendelea na biashara hiyo, wanatakiwa kufungua maduka na kuyasajili huku akiwataka wananchi kuacha kuwatumia wahuni wa mitaani kubadili fedha zao. Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Nakonde nchini Zambia, Field Simwinga, alisema Serikali za Tanzania na Zambia ziliamua kurasimisha mfumo huo wa matumizi ya Kwacha na Shilingi kwa pande hizo mbili ili kuboresha sekta ya biashara. Alisema vilevile waliamua kutekeleza utaratibu huo ili kuendana na matakwa ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika (Sadc) ya kuondoa vikwazo vya kibiashara miongoni mwa nchi wanachama.

Alisema ili kuhakikisha mfumo huo unakuwa na faida, Serikali ya Tanzania inatakiwa isaidie kuwaondoa wafanyabiashara ambao wametapakaa mitaani wakifanya biashara hiyo na kuongeza muda wa benki na maduka ya kubadilisha fedha ili wananchi wapate huduma muda wote.

"Hiki tunachokifanya hapa ni kwa faida ya nchi zetu mbili na kitatusaidia hata kuimarisha uhusiano wetu, lakini kitu tunachoomba kiboreshwe ni muda wa benki na maduka kuongezwa na ikiwezekana zifanye kazi usiku kucha maana kituo chetu cha pamoja kinafanya kazi saa 24," alisema Simwinga.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa BoT, tawi la Mbeya, Ibrahimu Malogoi, alisema kurasimisha matumizi ya fedha hizo kutasaidia kuimarisha fedha za nchi zote mbili tofauti na ilivyokuwa awali na wafanyabiashara walikuwa wanahujumu viwango vya ubadilishaji wa fedha. Pia alisema utaratibu huo utasaidia kuepuka kusambaa kwa noti bandia ambazo zilikuwa zinaingia kwenye mzunguko kupitia kwa wafanyabiashara hao ambao baadhi sio waaminifu. Alisema mfumo huo utasaidia serikali kukusanya kodi kupitia biashara hiyo ya ubadilishaji wa fedha za kigeni kwa maelezo kuwa awali ilikuwa vigumu kukusanya kwa wafanyabiashara hao.

# Watakaohujumu wagombea wateule CCM kufukuzwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UONGOZI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wilayani Mbeya Mjini, umetangaza utawafukuza uanachama mtu yeyote wa chama hicho atakayeshiriki njama za kuwahujumu wagombea watakaoteuliwa kukiwakilisha kwenye nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za chama hicho, eneo la Saba Saba, Katibu wa CCM Wilaya ya Mbeya Mjini, Gervas Ndaki, alisema baadhi ya wanachama wamekuwa wakiwahujumu wagombea wao kwa kuwasema vibaya.

Alisema kwa sasa utaratibu wa chama hicho kuwapata wagombea majimbo ni tofauti na miaka iliyopita kwa kuwa kulikuwa na utitiri wa watia nia ambao wanapigiwa kura za maoni, lakini sasa hivi yatakuwa yanapitishwa majina matatu pekee.

Ndaki alisema mwanachama ama kiongozi ambaye ataonyesha kuwasema vibaya wagombea watakaokuwa wameteuliwa, atafukuzwa kupitia vikao vya kamati ya nidhamu na kwamba kwa mujibu wa maelekezo ya chama vikao hivyo vinaweza kuitishwa muda wowote hata kama ni usiku na uamuzi ukatolewa.

"Makundi wakati wa uchaguzi ni kitu cha kawaida, lakini baada ya mgombea kuteuliwa makundi yote yanavunjwa na anaanza kunadiwa mtu huyo mmoja, sasa ikitokea mtu yeyote akawa anamsema vibaya iwe hadharani ama kwa kunong'ona tutamfukuza," alisema Ndaki.

Alisema chama hicho kina uwezo wa kumfukuza uanachama mwanachama yeyote na kutoa mfano viongozi wakubwa akiwamo aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Benard Membe, ambaye alivuliwa uanachama wiki iliyopita.

Katika hatua nyingine, alimjia juu Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu' kutokana na kauli alizozitoa kuhusu Rais Dk. John Magufuli na CCM hivi karibuni alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari.

Katika maelezo yake, Ndaki alisema alimsikia mbunge huyo akisema "Rais Magufuli na chama chake cha CCM hajafanya maendeleo yoyote ndani ya Jiji hilo na badala yake wanaishia kuwanunua madiwani wa Chadema."

Alisema kauli hizo haina mashiko yoyote kwa maelezo kuwa kuna miradi mbalimbali ambayo imefanywa ikiwamo ya elimu, afya na hata miundombinu ya barabara inaendelea kujengwa.

"Hata fedha za Mfuko wa Jimbo ambazo 'Sugu' ni mwenyekiti wake zinapopitishwa na Bunge, Sugu ni miongoni mwa wabunge ambao hawajawahi kuipitisha ila kwenye matumizi yeye anakuwamo," alisema Ndaki.

## Waomba uharaka utoaji vibali michango ya maendeleo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Kata ya Nsalaga katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wameiomba serikali kuharakisha kutoa vibali vya kuwaruhusu wananchi kuchangia maendeleo ya shule hasa ujenzi wa miundombinu.

Walitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki walipokuwa wanapokea msaada wa mifuko 82 ya saruji iliyotolewa na wanafunzi wa Chuo cha Uhasibu nchini (TIA), Tawi la Mbeya kwa ajili ya kusaidia ukarabati wa vyoo na madarasa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu wa Shule ya Msingi Nsalaga.

Mwenyekiti wa Mtaa Majengo Mapya katika Kata hiyo, Fanikiwa Chaula, alisema wananchi wa kata hiyo waliazimia kuchangia Sh. 4,000 kwa ajili ya kukarabati shule hiyo, lakini kibali kina zaidi ya miezi miwili hakijatoka tangu walipoomba.

Alisema waliuomba uongozi wa Halmashauri ya Jiji hilo kutoa kibali hicho ili wakarabati shule hiyo kongwe na kwamba wananchi wana fedha na wako tayari kuchangia lakini kinachowakwamisha ni kibali.

"Shule hii tulijengewa miaka mingi sana na Mzungu aliyekuwa anakaa hapa, sasa imechakaa na haifanani kabisa ndio maana tukaomba tuikarabati, sisi wananchi tuko tayari kufanya maendeleo hivyo tunaomba serikali iwahishe kutoa vibali," alisema Chaula.

Akikabidhi msaada huo, Mwalimu Mlezi wa wanafunzi wa Chuo TIA, Dietrich Mgaya, aliwataka wananchi wa kata hiyo kujitoa kwa moyo kushirikiana na serikali kujenga miundombinu ya elimu badala ya kuiachia serikali.

Alisema kila mmoja anatakiwa ajitolee kuboresha madarasa ya watoto wenye mahitaji maalumu ili wapate elimu katika mazingira mazuri kama ilivyo kwa wanafunzi wengine.

Mgaya alisema endapo mazingira ya vyoo kwenye shule hayatakuwa rafiki kwa watoto, kuna hatari ya magonjwa ya mlipuko kutokea kwenye shule na kusababisha maafa.

"Hawa ni watoto wetu wenyewe kwahiyo tusisubiri watu wengine kuja kutusaidia kuboresha miundombinu, tusisubiri akina mjomba waje watusaidie, sisi wenyewe tujitolee kufanya kazi hii," alisema Mgaya.

Mwalimu Mkuu wa watoto wenye mahitaji maalumu katika Shule ya Msingi Nsalaga, Bosijege Kasokela, aliwashukuru wanafunzi wa chuo hicho kwa msaada waliotoa.



# Mbunifu wa helikopta kupata mamilioni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imesema kiasi cha Sh. milioni 750 kimetolewa kwa ajili ya kuendeleza wabunifu 60 walioshiriki mashindano ya kitaifa ya sayansi, teknolojia na ubunifu (MAKISATU) mwaka jana.

Miongoni mwa wanufaika wa fedha hizo ni pamoja na mbunifu wa helikopta, Adam Kinyekire, ambaye atapatiwa Sh. milioni 99 ili kutengeneza karakana yake na kubuni teknolojia nyingi zaidi.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi wa Idara ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu wa Wizara hiyo, Prof. Maulilio Kipanyula, katika semina ya wanahabari kuhusu mashindano hayo kwa mwaka 2020, yatakayofanyika kuanzia Machi 16-20 jijini Dodoma.

Alisema serikali imedhamiria kuwatambua na kuendeleza ubunifu wao kuanzia ngazi ya chini ili uwe na manufaa kwa Taifa na ziwasaidie kujikwamua kiuchumi.

"Kwa mara ya kwanza mashindano yalifanyika mwaka jana ambapo tulipokea maombi 415 na kupitia makundi mbalimbali walipatikana wabunifu 60 walioshiriki mashindano na 18 kati yao waliibuka washindi, lakini wizara ikaamua washiriki wote bunifu zao ziendelezwe na wengine kwa tulivyowatembelea kila mmoja alikuwa na mahitaji yake," alisema.

Alieleza kuwa mbunifu wa helikopta ambaye yupo wilaya ya Tunduma mkoani Songwe atapata Sh. milioni 99 kwa ajili ya kutengeneza karakana yake ili kubuni vitu vingi.

"Huyu mbunifu Adam baada ya ubunifu wake wa ndege tulimfikia tukaangalia ubunifu wake na kuna hatua kadhaa zimechukuliwa kwanza kumuunganisha na taasisi zinazoendana na kazi anayofanya, tulimuunganisha na Shirika la Nyumbu pale Kibaha ili kuona namna ya kumsaidia na kuangalia kama ubunifu wake utasonga mbele," alisema.

Alisema mbunifu huyo pia hakuishia kwenye ndege bali amebuni pia mashine ya nafaka inayofanya kazi nyingi.


"Alishiriki mashindano mwaka jana na atapata Sh. milioni 99 kwa ajili kusaidia karakana yake iweze kutoa vitu vizuri zaidi, tunataka kumuona anazalisha na anaendelea na ubunifu wake zaidi, tupo naye tunamfuatilia kwa karibu," alisema.

Aliwataka Watanzania kubuni na kugundua teknolojia ambazo zitasaidia nchi kupiga hatua kimaendeleo na kufikia uchumi wa viwanda.

Akizungumzia mashindano ya mwaka 2020, Prof. Kipanyula alisema tayari wamepokea maombi ya wabunifu 583 na taasisi 61 zitashiriki kwenye maonyesho ya Makisatu.

Aliwaomba waandishi wa habari kusaidia jamii kupata uelewa wa mashindano hayo ili kukuza ubunifu na kutambulika kwa umma huku akisema fomu za kushiriki zimekuwa zikitolewa kwenye na Makatibu Tawala wa Mikoa.

"Pia tuhamasishe watafiti wasiishie kusambaza matokeo bali waweke kwenye namna ambayo itawafikia walengwa kwa lugha rahisi," alisisitiza.



Msajili kwa njia ya kielektroniki kutoka kampuni ya Datavision International, Cecilia William, akichukua picha na taarifa za askari wa kampuni ya sekta binafsi ya ulinzi Mkoa wa Dodoma kama alivyokutwa jana, eneo la Polisi Jamii jijini Dodoma, Jeshi la Polisi limeagiza wafanyakazi wote wa kampuni hizo wasajiliwe kwa njia hiyo ili kuwatambua. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Agizo madiwani Mpwapwa kujaza fomu za maadili

**Na Renatha Msungu,** MPWAPWA

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, wametakiwa kujaza fomu za maadili na tamko la mali zao na madeni na kuwasilisha katika Ofisi za Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kabla ya udiwani wao kukoma Julai, mwaka huu.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Ofisa wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, George Shilla, wakati akiwasilisha mada ya tamko la mali na madeni katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo.

Alisema jukumu la kujaza fomu ya maadili ni jukumu la kila kiongozi wa umma na halimhusu mwajiri wake au mkuu wake wa idara na kwamba lipo kwa mujibu wa Sheria ya Maadili namba 13 ya Mwaka 1995 inayomtambua kiongozi wa umma.

Alisema madiwani wana wajibu wa kuwasilisha fomu hizo kwa Kamishna wa Maadili wenyewe na siyo kutegemewa kuwasilishiwa na Mkurugenzi wa Halmashauri kwani Sheria ya Maadili Namba 13 ya Mwaka 1995 inatambua kiongozi wa umma wao binafsi kila mmoja.

Shilla aliwataka madiwani kuijiepusha na mgongano wa maslahi kwa kuwa kina madhara makubwa kwa maendeleo ya taifa na wilaya.

Alisema mgongano huo unadidimiza maendeleo ya nchi na wananchi kukosa imani na viongozi wao.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, George Fuime, aliwaomba ofisi ya sekretarieti ya maadili kuharakisha fomu hizo ili kuzijaza kwa wakati.

Pia aliwaomba sekretarieti ya maadili kufungua ofisi katika wilaya ili kupunguza mrundikano wa watumishi kwenye ofisi za kanda.

# Usajili walinzi kielektroniki kabla Desemba

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAKURUNGENZI wa kampuni za sekta binafsi za ulinzi nchini (TSIA), wametakiwa kusajili wafanyakazi wao kwa njia ya kielektroniki kabla ya Desemba mwaka huu ili kudhibiti vitendo vya kihalifu wanavyofanya walinzi.

Kauli hiyo ilitolewa na Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Narcis Missama kutoka Makao Makuu ya Jeshi hilo, katika mkutano wake na wakurungenzi hao jijini hapa. Missama alisema lengo la usajili huo ni kuwatambua askari wote wa makampuni hayo.

Alitaja sababu nyingine ni kuwabaini askari wenye tabia za wizi ambao wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya kihalifu na kukimbilia mikoa mingine na kuajiriwa huko.

"Usajili huu utakuwa na uwezo wa kumtambua askari yeyote aliyewahi kufanya kazi kwenye kampuni nyingine hapa nchini hata kama utahama mkoa aliyosajiliwa," alisisitiza.

Aliwataka wakurugenzi hao kuhakikisha askari wa kampuni zao wanapewa mafunzo ya mbinu za kiulinzi yanayotolewa na jeshi hilo kwa kushirikiana na wakufunzi kutoka vyombo mbalimbali vya ulizi na usalama.

Alisema mafunzo hayo yalianza kwa baadhi ya mikoa, lakini yataendelea hadi wahakikishe askari hao wanapewa mafunzo hayo kwa nia ya kuwajengea uwezo wa kazi.

"Hatuwezi kuwa tunawalalamika kuwa askari wetu hawana ujuzi wa kiulinzi wakati wengine hawajawezeshwa, hivyo hakikisheni kila askari anapata mafunzo hata kama aliwahi kupitia majeshi mengine ya ulinzi," alisema.

Alisema kila askari atakayepata mafunzo hayo atakabidhiwa cheti maalumu kumtambua na ambacho kitakuwa ni sehemu ya kigezo mmoja wapo cha kupata ajira na vitakuwa katika mfumo wa kitaifa.

Naye Mkurugenzi wa Miradi wa Kampuni ya Datavision International, Macmillan George, alisema kampuni hiyo kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi walibuni mfumo huo ili kuisaidia sekta ya ulinzi binafsi na kuna kampuni 60 za sekta hiyo.

Mwenyekiti wa Kampuni za Sekta Binafsi za Ulinzi Kanda ya Kati, Lukanus Kayombo, alisema kanda hiyo ilitoa mafunzo kwa askari wake kwa awamu ambapo awamu ya pili ya mafunzo hayo inatarajiwa kuanza mwezi huu.



# Mhadhiri aomba usimamizi rasilimali bahari

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MHADHIRI wa Chuo Kikuu Cha Taifa Zanzibar (SUZA), Dk. Ali Makame Ussi, amesema kuwa kunahitaji usimamizi endelevu wa rasilimali za bahari ili kutoa tija kwa kizazi kijacho.

Hayo aliyasema jana alipokuwa akiwasilisha mada kuhusu hali halisi ya mazalio ya samaki matumbawe ya baharini katika mafunzo ya waandishi wa habari kuhusu mradi wa uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFISH), uliofanyika Mjini Zanzibar.

Alisema kuna ongezeko kubwa la wavuvi wadogo kila siku hali inayoashiria kupungua au kukosekana kabisa rasilimali hizo kutokana na mahitaji kuongezeka. Alisema lazima kuwe na usimamizi mzuri ili kuhakikisha waliopo wanafaidika na kuja kufaidika wajao.

Ili kufikia hayo, alisema wanahitaji taarifa sahihi na uwapo wa ufuatiliaji wa karibu wa zao hilo la bahari ili kujua hali yake halisi.

"Hali sio mbaya sana, lakini tunahitaji ufatiliaji wa karibu ili kujua kinachoendelea," alisema.

Kwa upande wake, Mratibu wa mradi huo, Hashim Muumini, alisema lengo la kuwapo kwa mradi huo ni kuangalia tija inayopatikana na usimamizi wa wavuvi hususan wadogo.

"Tunapozungumzia uvuvi wa Zanzibar mara nyingi ni ule uvuvi wa wavuvi wadogo ambao wanatumia dhana za kiasilia kama vile mtumbwi, ngalawa na madau," alisema.

Alisema wavuvi hao wanachangia asilimia sita na mpaka sasa wapo 34, 571 na kwamba wakazi wa Zanzibar wanakula kwa wingi viumbe vya baharini (samaki) kuliko nyama na kutaja kwa mwezi wanakula kilo 22.5 ikiwa ni ongezeko kubwa la matarajio ya duniani ambao kwa mwezi ni kilo 16.

Zaidi ya asilimia 90 ya wavuvi wa Zanzibar wanatumia uvuvi katika mwambao wa Matumbawe kwa mujibu wa utafiti uliofanywa mwaka 2002 ambayo yapo kwa asilia 35 mpaka 2016.



Mratibu wa Taasisi ya Mwambao, Ali Thani, akiwasilisha mada wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusiana na masuala ya uvuvi, hafla iliofanyika ukumbi wa Wizara ya Kilimo Maruhubi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Jamii yatakiwa kushiriki kutokomeza kipindupindu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI Mtendaji Kamisheni ya kukabiliana na maafa Zanzibar, Makame Khatibu Makame, ameitaka jamii kushiriki kikamilifu Mpango Shirikishi wa Taifa wa kutokomeza maradhi ya kipindupindu.

Alisema njia rahisi ya kuelekea kuwa na taifa lisilokuwa na kipindupindu ni wananchi kubadilika na kuelewa umuhimu wa kutumia vyoo, kunywa maji yaliyo salama na kusafisha mazingira yaliyowazunguka.

Mkurugenzi Makame alieleza hayo jana alipokuwa akifunga mafunzo ya siku sita ya wawezeshaji wa Mpango Shirikishi wa kutokomeza kipindupindu ngazi ya wilaya na taifa yaliyofanyika Mwanakwerekwe. Alisema kipindupindu ni moja kati ya maradhi mabaya ya mlipuko, ni rahisi kujikinga nayo iwapo kila mtu atafuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa Wizara ya Afya. Aliwataka wawezeshaji waliopatiwa mafunzo hayo kuyatumia kuwaelimisha wananchi njia sahihi za kujikinga kwa kuwa Zanzibar bila kipindupindu inawezekana.

Mkufunzi wa mafunzo hayo, Mhandisi Mazingira kutoka Taasisi ya Uhandisi na Uhifadhi wa Mazingira (EEPCO) John Ngemo, alisema ili kutokomeza kipindupindu ni wananchi kuacha tabia ya kujisaidia ovyo, kutibu maji kabla ya kunywa na kuhakikisha chakula hakiingii kinyesi. Alisema Shirika la EEPCO kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (Unicef), limetoa mafunzo kwa wawezeshaji kutoka vitengo mbali mbali kuunga mkono juhudi za serikali za kutokomeza maradhi hayo.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Afya kutoka Wizara ya Afya, Forogo Mtande, alisema Serikali ya Zanzibar imeandaa mkakati wa kumaliza kipindupindu na mafunzo yaliyotolewa kwa wawezeshaji kutoka wilaya tano ni moja ya mikakati iliyopangwa kwa ajili ya mpango huo.

Alisema Wizara ya Afya imejipanga kutekeleza mpango huo kwa vitendo na amewashauri wananchi na taasisi nyingine kushiriki kikamilifu kwa kuwa vita hivyo vinahitaji nguvu ya pamoja ili kufanikiwa.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Seif Hamad Swaleh, ambaye ni Ofisa Lishe Wilaya ya Mjini, alimtaka kila mwananchi kuchukua tahadhari mwenyewe kwa kuwa kosa la mtu mmoja linaweza kuathiri wananchi wengi kwa wakati mmoja.

Alisema kila mtu anapaswa kujisimamia mwenyewe na kuhakikisha kuwa hafanyi kosa litakalosababisha kipindupindu hasa kipindi cha mvua za masika kinachotarajiwa kuanza wiki chache zijazo.

Mafunzo ya kuwajengea uwezo wawezeshaji wa mkakati wa kutokomeza kipindupindu Zanzibar yalitolewa kwa maofisa wa Elimu ya Afya, Lishe na Maafa kutoka Wilaya ya Mjini, Wilaya ya Magharibi 'A' na Magharibi 'B' kwa Unguja na Pemba ni Micheweni na Wete.

## Dk. Shein ahakiki taarifa zake daftari wapigakura

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKATI zoezi la uandikishaji na uhakiki wa taarifa za wapigakura likiwa linaendelea Visiwani Zanzibar, juzi Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, alihakiki taarifa zake katika daftari hilo kwenye kituo cha Shule ya Bungi Mkoa wa Kusini Unguja.

Dk. Shein alifuatana na mke wake Mama Mwanamwema Shein kituoni hapo na kufuata taratibu zote za uandikishwaji ikiwamo kupanga foleni kama wananchi wengine kwa ajili ya kuhakiki taarifa zao katika daftari hilo.

Akizungumza na vyombo vya habari baada ya kuhakikiwa Dk. Shein alikiri kuwa zoezi la uandikishaji na uhakiki wa taarifa za wapigakura linaenda vizuri kutokana na utaratibu mzuri na mfumo wa uandikishaji ulioandaliwa na Tume ya Uchaguzi ambao unawapatia huduma wananchi kwa haraka zaidi.

Alisema kitambulisho cha Mzanzibar Mkaazi ni haki ya kila mtu hivyo aliwatoa hofu wananchi ambao hawajapata vitambulisho vipya vya Mzanzibar Mkaazi na kuwaomba kuendelea kufiatilia kutokana na umuhimu wake kwa matumizi mbalimbali.

Alisema Serikali ya Zanzibar imejiandaa kuendesha uchaguzi ulio huru na haki kutokana na kuandaliwa misingi bora ambayo itawawezesha wananchi kupata haki yao ya kupigakura na kuwa na ridhaa ya kuchagua viongozi wanaowataka kwa maslahi yao na taifa kwa jumla.

Akizungumzia suala la amani na utulivu nchini kuelekea uchaguzi mkuu, alisema serikali haitokuwa tayari kuona baadhi ya watu wanajaribu kuvuruga amani iliyopo na itaendelea kuwadhibiti na kuwachukulia hatua wale watakaofanya hivyo.

Katika hatua nyingine, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Jaji Mkuu mstaafu Hamid Mahmoud Hamid, alitembelea vituo katika kisiwa cha Uzi ikiwa ni miongoni mwa hatua ya Tume hiyo kuendelea na taratibu za kufuatilia zoezi hilo na kujionea baadhi ya changamoto zinazojitokeza.

Katika ziara hiyo, Mwenyekiti Hamid alisema lengo la Tume ya Uchaguzi ni kuandikisha idadi kubwa ya wananchi wenye sifa hivyo, itahakikisha inazipatia ufumbuzi changamoto hizo.

Zoezi la uandikishaji na uhakiki wa taarifa za wapigakura kwa Wilaya ya Magharibi " B' na Jimbo la Tunguu kwa Wilaya ya Kati, limemalizika juzi na limendelea jana katika majimbo ya Wilaya ya Kati na yote ya Wilaya ya Kusini na kutarajiwa kukamilika Machi 5.

# Waondokana na changamoto ya maji

Na Neema Emmanuel, MWANZA

WAKAZI wa maeneo ya Nyegezi Majengo Mapya, Mkoloani na Buhongwa wameanza kunufaika na maji baada ya tangi la Nyegezi Majengo Mapya kukamilika na maji kufunguliwa.

Hayo yalibainishwa na Meneja Uhusiano wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira jijini Mwanza (Mwauwasa), Mohamed Saif, wakati akizungumza na Nipashe, na kueleza kuwa tangi hilo limekamilika na maji yamefunguliwa, hivyo ni fursa kwa wananchi wa maeneo hayo kuyatumia.

"Napenda kuwafahamisha wananchi wa maeneo ya Nyegezi Majengo Mapya, Mkolani na Buhongwa kuwa maji yameanza kutoka na kwa wale ambao hawajaanza kupata huduma ya maji walio katika maeneo haya watupatie taarifa mapema ili tuweze kufika na kubaini tatizo," alisema Saif. Aliwataka wananchi wa maeneo hayo ambao ni wanufaika kupitia tangi hilo watoe taarifa za uvujaji wa mabomba ili waweze kuzifikia kwa haraka na kuzuia upotevu wa maji.

Alisema tangi hilo lina uwezo wa kuhifadhi lita milioni 1.2 za maji ambalo litahudumia wakazi wote wa maeneo hayo kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwenye maeneo hayo yenye changamoto.

Hivi karibuni, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mwauwasa, Mhandisi Leonard Msenyele, alieeleza kuwa ujenzi wa tangi hilo umekamilika, hivyo wananchi watarajie kupata huduma ya maji kwa uhakika.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, akisalimiana na Kaimu Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa, kwenye tamasha la mamalishe Wilaya ya Kisarawe jana. NMB wamedhamini tamasha hilo ili kuwainua wajasiriamali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanahabari waombwa vita ya ufisadi

Na Neema Emmanuel, MWANZA

WAANDISHI wa habari nchini wameshauriwa kuunga mkono jitihada zinazofanywa na serikali katika mapambano dhidi ya rushwa.

Rai hiyo ilitolewa na Mkurugenzi wa Mipango wa Ofisi ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali, Florian Bombo, kwenye mafunzo ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa kuandika habari za ubadhirifu na viashiria vya rushwa zinazotokana na taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG).

Alisema waandishi wa habari wanapaswa kutoa taarifa kwa wananchi kuhusu ubadhirifu na viashiria vya rushwa vitakavyokuwa vikitolewa na ofisi ya CAG.

"Sisi sote tunatambua athari kubwa zitokanazo na rushwa, hivyo basi wajibu wetu sote ni kuhakikisha kuwa tunaunga mkono juhudi za serikali katika jitihada zake za kupambana na rushwa," alisema Bombo.

Alisema ofisi ya CAG inatekeleza mradi wa kujenga mfumo endelevu wa kupambana na rushwa nchini (BSAAT) na kuzinufaisha taasisi mbalimbali, na kuwa lengo la programu hiyo ni kupunguza rushwa nchini ambayo imekuwa ni changamoto kubwa katika kupambana na umaskini nchini.

Naye Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kanda ya Ziwa, Anna Masanja, akizungumzia juu ya umuhimu wa mafunzo kwa waandishi wa habari, alisema wanaimani na waandishi wa habari wakielewa vizuri, watawasaidia kuwaelimisha wadau na wananchi juu ya kusimamia rasilimali na fedha kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

"Kupitia vyombo vyenu mtasaidia sana katika kuchambua kwa ufasaha kwa kutumia lugha nyepesi ambayo kila mwananchi anaweza kuelewa vizuri na kufanya maamuzi sahihi ya kusimamia matumizi mazuri ya rasilimali za taifa," alisema Masanja.

# Mamalishe watakiwa kuchangamkia fursa

Na Mwandishi Wetu

WAJASIRIAMALI wa kike na mama lishe walioshiriki Tamasha la Vyakula na Ujasiriamali wilayani Kisarawe, wametakiwa kuchangamkia fursa ya kukuza mitaji yao.

Fursa hizo zitokanazo na Akunti ya Fanikiwa ya Benki ya NMB, ambayo ina gharama nafuu za uendeshaji kulinganisha na akaunti nyingine, ili kuharakisha kukua kwa mitaji yao.

Tamasha hilo lililotambulika kama Kisarawe Mamalishe Festival 2020, lilidhaminiwa na Benki ya NMB, ambayo iliinadi Fanikiwa Akaunti, ambayo huwezesha wafanyabiashara wadogo kuweka amana zao benki, huku pia ikiwapa fursa ya kupata mikopo nafuu kwa ustawi wa biashara zao.

Kisarawe Mamalishe Festival 2020, lililenga kutoa elimu ya nidhamu ya fedha, kuwaongezea ujuzi, kuzipa thamani bidhaa na kubadilishana mawazo kwa washiriki, ambalo limefanyika na kufana wikiendi hii, chini ya uratibu wa Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo na kudhaminiwa na NMB.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa tamasha hilo, Ofisa Mkuu wa Fedha wa NMB, Benedicto Baragomwa, alisema Fanikiwa Akaunti ni kimbilio sahihi la wajasiriamali na mamalishe, ambako hadi sasa NMB imefungua akaunti 80,750 nchi nzima.

"Tayari tumetoa mikopo 1,963 yenye thamani ya Sh. bilioni 5.3 kupitia Fanikiwa Akaunti, lakini tunayo Pamoja Akaunti, ambayo ni maalumu kwa vikundi vilivyorasimishwa ili kuviwezesha kusimamia makusanyo na matumizi fedha kulingana na maamuzi na shughuli za wana kikundi," alisema.

Aidha, Baragomwa alisema NMB inajisikia fahari kuwa wafanikishaji wa tukio hilo, walilolitumia kuthibitisha ukaribu wa benki hiyo kwa jamii ya Kitanzania, hususani wafanyabiashara na wajasiriamali wa kada zote.

Aliipongeza serikali kwa kutoa kipaumbele kikubwa katika kuweka mazingira wezeshi kwa wajasiriamali, hasa wadogo wadogo kwa lengo la kukuza biashara zao, hivyo kuchanga ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja, nchi na kukuza pato la taifa.

Baragomwa alitambia kiasi cha Sh. bilioni 640 ambacho NMB imetumia kuwezesha Biashara Ndogo na za Kati (CSME's) na Kilimo, huku ikitoa zaidi ya Sh. bilioni 600 kwa wawekezaji wakubwa, pamoja na Sh. trilioni 2.2 walizokopesha wateja binafsi wa benki hiyo.

Kisarawe Mamalishe Festival 2020, tamasha hilo lililokutanisha vikundi 17 vya mamalishe na wajasiriamali (kimoja kutoka kila kata wilayani humo), lilihudhiriwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo.

Waziri Jafo, ambaye ni Mbunge wa Kisarawe, aliwataka wajasiriamali wa kike wilayani humo kutumia elimu waliyopata, huku akiipongeza NMB kwa kudhamini, lakini kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Jokate Mwegelo kwa wazo chanya lililozaa tamasha hilo.

"Tamasha hili linaunga mkono sera ya serikali ya kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Tamasha hili ni maono yanayopaswa kuigwa na kujifunzia kupitia kwao. Pongezi kwa NMB kukubali kudhamini tamasha hili," alisema Waziri Jafo.

Aliitaja Wilaya ya Kisarawe kuwa ni kinara wa utekelezaji na matumizi sahihi ya fedha za makundi maalum ya kijamii (wanawake, vijana na walemavu), na kwamba serikali iliitengea wilaya hiyo zaidi ya Sh. bilioni 90, ambazo zimetumika vema, huku akimpongeza Mkurugenzi wa Wilaya hiyo.

Naye Jokate Mwegelo, Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, alisema maendeleo ya Wilaya ya Kisarawe yanahitaji nguvu za wana Kisarawe na wadau wa maendeleo kama NMB na kwamba mahudhurio makubwa ya mamalishe ni dalili njema za kufana kwa mchakato wa mabadiliko kuelekea Siku ya Wanawake Machi 8.

## HABARI KIMATAIFA

# Corona yaingia Marekani, mmoja afariki

**WASHINGTON,** Marekani

MAREKANI imethibitisha kutokea kwa tukio la kwanza la mgonjwa mwenye virusi vya corona katika Jimbo la Washington.

Maofisa wa Marekani wamesema kwamba mgonjwa huyo mwenye miaka 50 alikuwa mwanaume ambaye hali yake ya afya haikuwa nzuri.

Rais Donald Trump alisema kwamba vifo vingi zaidi vinatarajiwa kutokea na akaongeza kuwa nchi hiyo imejitayarisha kwa lolote litakalo tokea.

Jana, nchi za Australia na Thailand pia zimerekodi kifo cha kwanza cha virusi vya corona.

**Rais Donald Trump alisema vifo vingi zaidi vinatarajiwa kutokea na nchi imejitayarisha kwa lolote litakalo tokea.**

Mwanamume wa miaka 78 wa Australia alifariki dunia baada ya kuambukizwa ugonjwa huo katika meli ya Diamond Princess nchini Japan mwezi uliopita. Thailand ambayo imethibitisha kutokea kwa vifo 42 vya corona imesema mwanaume wa miaka 35, aliyekufa pia alikuwa anaugua homa ya dengue.

Zaidi ya matukio 85,000 ya ugonjwa wa corona vimethibitishwa katika nchi 57 kote duniani huku vifo 3,000 vikithibitishwa, kulingana na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Idadi kubwa ya vifo hivyo ni kutoka China na kwamba virusi hivyo vilianzia mwishoni mwa mwaka jana.

Maofisa wa afya wa eneo wamethibitisha kwamba mwanaume huyo alikufa katika Jimbo la Washington. Na kuongeza kwamba hakuwa amesafiri katika maeneo yalio kwenye hatari ya kupata ugonjwa huo.

Gavana wa Jimbo la Washington, Jay Inslee, alitangaza hali ya hatari kama hatua alioichukua baada ya kutokea kwa kisa hicho kipya katika jimbo lake.

Hilo linatokea wakati maofisa katika pwani ya magharibi ya Marekani - California, Oregon na Washington - wakiwa na wasiwasi kuhusu vifo vinavyowatokea wagonjwa ambao hawakuwa wametembelea eneo lenye mlipuko ama kutangamana na yeyote aliyekuwa na ugonjwa huo.

Maofisa wa Jimbo la Washington Jumamosi walisema wanachunguza uwezekano wa kutokea kwa mlipuko wa corona katika makao ya kuwatunza wazee.

Ofisa wa Afya eneo la Seattle, Dk. Jeffrey Duchin, alisema kuna matukio mawili yenye kuhusishwa na makao ya kuwatunza wazee, mhudumu mmoja wa afya na mkazi mwenye umri wa miaka 70. Dk. Duchin alisema kuwa wakazi 27 na wahudumu 25 katika kituo hicho walionyesha dalili kama hizo. Aidha maofisa walisema matukio zaidi ya corona yanatarajiwa kutokea.

Hadi kufikia jana, WHO ilisema matukio 62 yameripotiwa nchini Marekani. **BBC**



Mjumbe wa kutafuta amani wa Marekani, Zalmay Khalilzad (kushoto), na Mullah Abdul Ghani Baradar, kiongozi wa kisiasa wa ngazi ya juu wa kikundi cha Taliban wakisaini mkataba wa amani kati ya Taliban na maofisa wa Marekani, Doha. **PICHA: AP**

## Marekani, Taliban wafikia makubaliano ya amani

**DOHA,** Qatar

MAREKANI na kikundi cha Taliban wamesaini makubaliano mjini Doha, Qatar, wakiandaa mazingira kumaliza vita vilivyodumu kwa takriban miaka 19 nchini Afghanistan na hivyo Marekani kurejesha vikosi vyake vilivyoko nchini huko.

Msimamizi Mkuu wa mazungumzo hayo, Zalmay Khalilzad na Mullah Abdul Ghani Baradar, Naibu Mkuu wa Taliban katika masuala ya kisiasa, alitia Saini makubaliano hayo wakati wa tafrija fupi katika hoteli moja mjini Qatar ambako Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo na mawaziri wa mambo ya nje wengine kutoka nchi kadhaa walihudhuria.

Katika tamko lililotolewa baada ya makubaliano hayo kusainiwa na kikundi cha Taliban, White House ilisisitiza kuwa Rais Donald Trump anatekeleza ahadi yake ya kurejesha vikosi vya Marekani nyumbani kutoka maeneo yenye vita visivyomalizika nje ya nchi na kusimamia kupatikana amani Afghanistan.

"Makubaliano yamefikiwa na kikundi cha Taliban ambao unaleta makubaliano muhimu ambayo ni ya dharura kuweza kumaliza vita nchini Afghanistan.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Mike Pompeo alitoa wito kwa kikundi cha Taliban kuheshimu makubaliano hayo na kuacha mahusiano na vikundi vyenye itikadi kali.

Chini ya makubaliano hayo Marekani itaanza kuwaondoa wanajeshi wake kwa sharti ya kuwa Taliban wazuie mashambulizi ya kigaidi dhidi ya serikali ya Afghanistan.

Wakati kundi la Taliban likitimiza masharti ya mkataba huo Marekani nayo itaondoa wanajeshi wake wote ndani ya muda wa miezi 14 ijayo. **VOA**

## Mkuu idara ya ujajusi afariki dunia

**KINSHASA,** DRC

NAIBU Mkuu wa majeshi ya FARDC, nchini DRC na Mkuu wa Idara ya Ujasusi katika jeshi, Jenerali Delphin Kahimbi amekutwa amefariki dunia nyumbani kwake jijini Kinshasa.

Taarifa za kifo cha Jenerali Kahimbi ilitolewa na mkewe pamoja na washirika wenzake kadhaa wa karibu. Hata hivyo, uchunguzi unaendelea, ofisa mmoja wa jeshi amebaini.

Jenerali Delphin Kahimbi aliitwa mara kadhaa katika siku za hivi karibuni kujibu tuhuma zinazomkabili (uhusiano na makundi yenye silaha na kujaribu kuhatarisha usalama).

Kulingana na vyanzo kutoka Ikulu ya Rais, Jenerali Delphin Kahimbi alikuwa amesimamishwa kazi.

Msemaji wa jeshi amekiri kwamba uchunguzi umeanzishwa ili kubaini sababu za kifo chake. Kifo chake kimetokea baada ya kusimamishwa kazi tu.

Mwishoni mwa wiki kulikuwapo na taarifa zilizozagaa zikieleza kuwa, Jenerali Delphin Kahimbi, amefariki dunia katika Hospitali ya Cinquantaire jijini Kinshasa.

Jenerali Delphin Kahimbi, ambaye alikuwa anakabiliwa na vikwazo vya Ulaya na Marekani tangu mwaka 2016, anatuhumiwa makosa ya ukiukwaji wa haki za binadamu nchini DRC. **RFI**

## Rais Condé ahairisha mchakato katiba mpya

**CONAKRY,** Guinea

RAIS wa Guinea, Alpha Condé ameahirisha kura ya maoni yenye utata iliyokuwa ifanyike jana kuhusu kubadilishwa kwa katiba.

Mabadiliko hayo endapo yatapita huenda ikamruhusu kuwania tena urais kwa awamu ya tatu.

Condé, (81), alisema aliamua kuahirisha kwa muda kura hiyo kwasababu upinzani ulidai kuwa maofisa wameingilia usajili wa wapigakura.

Tangazo hilo limetolewa huku wasiwasi ukiendelea kuongezeka kuhusu suala la kura hiyo kufanyika kwa haki.

Maandamanao yenye ghasia yamekuwa yakishuhudiwa katika miezi ya hivi karibuni kupinga kura hiyo. Karibia watu 30 wameuawa katika maandamano ambayo yamekuwa yakifanyika tangu Oktoba.

Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS), wamesema kwamba hawatatuma waangalizi wao kwa uchaguzi huo.

Inakadiriwa kuwa raia milioni 7.7 waliosajiliwa kupiga kura pia watapiga kura kuchagua wabunge.

Mapema wiki hii, Shirika la Kimataifa la Wazungumzaji wa Kifaransa lilisema kwamba kuna tatizo la kutambua majina karibia milioni 2.5 katika usajili ya wapigakura.

Kulingana na Rais Condé, kura hiyo lazima itafanyika, na kulingana na barua iliyotumwa na Condé kwa Ecowas kuhusu kuahirishwa kwa uchaguzi huo.

"Huku hakumaanishi kwamba ni kulegeza msimamo au kurudi nyuma. Raia wa Guinea watamchagua wanayempenda kwa uhuru katika kura ya maoni," alisema Rais Condé katika runinga inayomilikiwa na serikali Ijumaa jioni.

Muungano wa upinzani uliokuwa unapinga katiba mpya, FNDC, ulitoa wito wa kususia kura hiyo ya maoni na kuongeza uwezekano wa wale wanaoiunga mkono kuibuka na ushindi kwa urahisi. **BBC**

# Wazazi wanaoweka watoto kuomba sasa kukamatwa

**Na Beatrice Shayo**

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, ameagiza kuchukuliwa hatua wazazi wanaowaweka watoto wao barabarani kwa ajili ya kuomba na wanaowapa fedha wakamatwe.

Dk. Ndugulile ameyasema hayo mwishoni mwa wiki baada ya kutembelea kijiji cha watoto kilichopo chini ya shirika la kuhudumia watoto waliopoteza au walio kwenye hatari ya kupoteza malezi ya wazazi.

Alisema sheria zimewekwa bayana kuwa mtoto ana haki ya kulindwa kuishi, kushirikishwa, ana haki ya kutokutumikishwa kazi.

Dk. Ndugulile alisema hivi karibuni kuna wimbi kubwa la watoto kutumikishwa kazi katika barabara na wazazi ambao wanawatumia watoto kwa ajili ya kuomba fedha.

"Nitumie fursa hii kuipongeza Halmashauri ya Ilala kwa kutoa tangazo la kutoza faini wale wote ambao watabainika kutoa fedha kwa ombaomba, vilevile ninawata waende mbali kuanza kuwachukulia hatua wazazi wanao waweka watoto wao barabarani badala ya kuwapeleka shule," alionya Dk. Ndugulile.

Alitoa rai kwa halmashauri nyingine za mijini ambazo zina wimbi kubwa la watoto ombaomba barabarani kuhakikisha wanawachukulia hatua wazazi pamoja na wanaotoa fedha.

"Tunataka kukomesha tatizo la ombaomba barabarani kwa sababu wazazi wao wengi ni watu ambao wakimilifu hawana tatizo la upungufu wowote wa kimwili, wanatakiwa kutimiza majukumu yao ya msingi ya kuhakikisha kwamba wanatafuta riziki kwa ajili ya kulea watoto wao na sio watoto kuwatafutia riziki," alisema na kusisitiza:

"Halmashauri nyingine za mijini zihakikishe zinachukua hatua za haraka za kuwaondoa ombaomba na kuwatoza faini wanaofanya kazi hiyo barabarani," alisema.

Kadhalika, alisema watoto 17,000 wamefanyiwa vitendo vyake ukatili wa kijinsia kwa mwaka 2017 na waliohusika ni ndugi au jamaa wa karibu.

Naye Mkurugenzi SOS Tanzania, David Mulongo, alisema wanajishughulisha na mipango ya utetezi na kulinda haki za watoto kwa kuwajengea mfumo imara wa ulinzi kwa mtoto.

Alisema kupitia programu hiyo ya vijiji vya watoto kuanzia mwaka 2015, wamefanikiwa kuwafikia watoto na vijana 34,418 kwa kuwapatia huduma za elimu, afya na kuboresha pato la familia ili kuziwezesha kumudu mahitaji ya msingi.

Alisema kijiji hicho kina jumla ya watoto 120 kati ya hao wasichana 54. Sita wapo chini ya umri wa kwanza shule, 14 shule ya awali, 56 shule ya msingi na 50 sekondari.

Mulongo alisema ili kufanikisha uendeshaji wa miradi ya kuhudumia watoto wa kitanzania rasilimali fedha ni muhimu.

"Kwa mwaka 2019 matumizi halisi kwa miradi yetu yote ilikuwa in pesa za kitanzania 12, 591,185,118. Michango ya ndani ya nchi ilikuwa kukusanya sh 233,160,000 lakini hadi mwisho wa mwaka zilipatikana Sh. 71,529,233 kwa hiyo utegemezi wa wahisani wa nje umeendelea kuwa mkubwa," alisema Mulongo.



Ofisa Uhusiano Mwandamizi Wateja Wadogo wa Benki ya CRDB, Seuri Meijo, akimwelezea Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo (wa pili kulia), huduma mbalimbali zinazotolewa na benki ya CRDB kusaidia wakinamama wajasiriamali wakati wa kongamano la mamalishe lililofanyika mwishoni mwa wiki. Kulia ni msanii wa muziki wa kizazi kipya Shilole ambaye ni mjasiriamali mamalishe. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Tanroad Lindi yakusanya mil. 350/- faini

**Na Said Hamdani,** LINDI

OFISI ya Wakala wa Barabara (Tanroads) mkoani Lindi, imekusanya maduhuri yenye thamani ya Sh. 351,945,890 zikiwa ni faini za magari makubwa yaliyokiuka sheria za barabara, ikiwamo uzidishaji wa mizigo kwa kipindi cha miezi sita iliyopita.

Meneja wa Tanroads mkoani Lindi, Issack Mwanawima, alisema hayo, alipokuwa akiwasilisha taarifa ya utekelezaji kwenye kikao cha Bodi ya Barabara kilichofanyika mjini hapa.

Mwanawima alisema makusanyo ya maduhuri hayo ni ya kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2019 hadi Januari 31, mwaka huu, magari makubwa 168,743 yalipimwa uzito kupitia mizani ya Kijiji cha Nangurukuru, Wilaya ya Kilwa na Mingoyo, Lindi.

Mwanawima alisema kati ya magari hayo 60,118 yalibainika kuzidisha uzito, wakati 2,490 yalizidisha zaidi ya asilimia tano inayoruhusiwa kisheria na kutozwa faini ya Sh. 351,945,890.

Alisema takwimu hizo zinaonyesha kupungua kwa idadi ya magari yaliyopimwa mwezi Novemba na Desemba, 2019 na Januari 2020, huku akitaja sababu kuwa ni kuharibika mara kwa mara kwa mizani iliyopo Kijiji cha Nangunguru.

Alisema wastani wa kuzidisha uzito kwa asilimia 35.61 katika mkoa upo juu kwa asilimia 1.85 ikilinganishwa na wastani wa kitaifa wa asilimia 33.76, huku akielezea sababu za kuzidisha uzito katika mkoa kuwa juu ya wastani wa kitaifa ni ongezeko la magari.

Aliyataja magari hayo kuwa ni pamoja na yaliyokuwa yakibeba korosho kutoka mkoani Ruvuma, Lindi na kupeleka Bandari ya Mtwara hadi Dar es Salaam na magari ya kubeba makaa ya mawe kutoka Mbinga, Songea na mawe aina ya gypsum kutokea Kilanjelanje na Hoteli Tatu, Kilwa.

# Programu mafunzo mahali pa kazi yaja

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI inatarajia kuzindua Programu ya Taifa ya Mafunzo kwa vitendo mahala pa kazi kwa vijana, baada ya kubaini asilimia 79.9 ya nguvu kazi ya taifa ambao ni vijana wana ujuzi wa chini katika ufanisi wa kazi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akielezea maandalizi ya Mkutano wa Mawaziri wa Sekta ya Kazi na Ajira wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi Kusini mwa Afrika (Sadc) unaotarajia kufanyika nchini kwa siku tano.

Mhagama alisema idadi ya vijana wenye uwezo wa kufanya kazi nchini ni milioni 15.7, lakini asilimia 79.9 kati yao wana ujuzi mdogo wa kufanya kazi.

"Mkutano huo wa Sadc utaanza Machi 2 hadi 6, na miongoni wa shughuli zitakazofanyika ni serikali kuzindua Programu ya Taifa ya Mafunzo kwa Vitendo mahala pa kazi kwa vijana," alisema Mhagama na kuongeza:

"Programu hii ni mahsusi kwa vijana wa Kitanzania waliohitimu vyuo mbalimbali ili kujifunza na kupata uzoefu, ujuzi, maadili ya kazi na namna bora ya kuhudumia wateja katika sehemu zao za kazi watakazoajiriwa ndani na nje ya nchi au kujiajiri wenyewe," alisema Mhagama.

Alisema programu hiyo itazinduliwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan na itaendeshwa na kugharamiwa na serikali kwa kushirikiana na waajiri.

Pia, muda wa mafunzo ni kati ya miezi sita hadi 12 na itawawezesha vijana kuoanisha ujuzi walioupata kwenye taasisi za elimu na mafunzo pamoja na mahitaji hali ya ujuzi kwa waajiri.

Itawawezesha vijana kujifunza maadili, mtazamo chanya kuhusu kazi pamoja na tamaduni za kuishi mahali pa kazi, vijana kupata uzoefu wa kazi unohitajika na waajiri kama sifa ya kuajiri.

Mhagama alisema washiriki wa mkutano huo wa Sadc ni Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wataalamu wa Sekta ya Kazi na Ajira kutoka nchi 16 zinazounda jumuiya hiyo.

"Vilevile utahudhuriwa na viongozi wakuu wa shirikisho ya vyama vya wafanyakazi na waajiri kutoka nchi hizo, kaulimbiu ni kukuza ajira na mahusiano mema sehemu za kazi kwa maendeleo endelevu," alisema Mhagama.

Alisema hadi sasa serikali imeshapokea maombi 14,000 ya vijana wanaotaka kujiunga na programu hiyo na kati yao 5,000 wameshafikiwa, 1,000 wameshapata kazi.

HABARI KITAIFA

# Jafo akerwa halmashauri kuwanyima mikopo vijana

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameziagiza halmashauri kutoa mikopo kwa vijana na wakishindwa atakwenda kuwashtaki ifikapo Juni, mwaka huu.

Waziri Jafo aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam katika kongamano la vijana kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kufanya shughuli za kujitafutia kipato na kuboresha maisha.

Alisema halmashauri ambazo hazitekelezi kanuni zilizopo za kutenga asilimia 10 ya mapato kwa ajili ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ni kuwanyima fursa makundi hayo. Jafo alisema utekelezaji usipofanyika asilaumiwe kwa hatua atakazozichukua, atapeleka majina ya halmashauri zilizoshindwa kutekeleza agizo hilo.

Alisema taifa lolote duniani liweze kuendelea linategemea vijana kwa kuwa ndio nguvu kazi, vinginevyo taifa hilo linaweza kuangamia lisipowekeza katika kundi hilo.

Alisema ni vizuri vijana hao wakapewa kipaumbele kwa kuwa serikali imetenga fedha katika halmashauri japo hawazitoi.

Waziri Jafo alitoa angalizo kwa vijana kuwa licha ya kuwapo kwa changamoto za kiuchumi, ajira kwa vijana wajihadhari kutumika hasa katika kipindi cha kuelekea uchaguzi.

Alisema katika nchi ambazo amani imetoweka baadhi ya sababu ni watu kufuata mkumbo au kushawishiwa na wasio na mapenzi mema na mataifa yao na kusababisha amani kutoweka. Alisema vijana wana nafasi kubwa katika uchaguzi jambo la msingi ni kuhakikisha wanawachagua viongozi wazuri wenye kufanya mabadiliko.

Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la Babawatoto, Mgunga Mwamnyenyelwa, alisema lengo la mradi wa kuwawezesha vijana mwaka huu, ni kuwapa elimu kuhusu ushiriki wao katika shughuli za kijamii, kubadili tabia na kuacha matumizi ya dawa za kulevya.

"Mabadiliko ya kifikra, uwajibikaji na utendaji katika jamii yataleta mafanikio ya kiuchumi nchini, iwapo vijana watahamasika na kuonyesha nia," alisema Mwamnyenyelwa.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Foundation for Civil Society (FCS), Francis Kiwanga, alisema wamewekeza kwa vijana zaidi hivi sasa kwa kuwawezesha katika miradi mbalimbali.

"Sasa hivi tunafadhili vijana zaidi kwa kuwa wana changamoto hasa za kiuchumi, hata hivyo tunaipongeza serikali kwa kusimamia upatikanaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa makundi maalumu, yaani wanawake asilimia nne, vijana pia asilimia nne na watu wenye ulemavu asilimia mbili. Utoaji wa mikopo kuanzia mwaka 2015 umeongezeka ikilinganishwa na hapo awali," alisema Kiwanga.

# Taasisi za fedha zaonywa kushikilia kadi za watumishi

**Na Happy Severine,** ITILIMA

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, amepiga marufuku taasisi ndogo za kifedha ambazo huwakopesha watumishi wa umma wakiwamo walimu, kuacha utaratibu wa kushikilia kadi zao za benki kama dhamana wanapowakopesha.

Mtaka alisema taasisi ambayo itabainika au kukutwa na kadi hizo, haitaruhusiwa tena kufanya kazi hiyo katika mkoa wake.

Alitoa onyo hilo juzi wakati wa hafla ya kuwapongeza walimu, wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wilaya ya Itilima waliofanya vizuri mitihani ya kitaifa mwaka jana.

Mtaka ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo iliyofanyika mjini Lagangabilili, aliwataka wamiliki wa taasisi hizo kuacha mara moja utaratibu huo kwani utawagharimu.

Alieleza kuwa taasisi hizo zimekuwa zikiwapatia mikopo watumishi, wengi wao wakiwa walimu hasa kutoka Wilaya ya Itilima, huku sharti likiwa kuweka rehani kadi zao za benki na nywila (Password).

"Ni marufuku kwa taasisi yoyote ya pesa ambayo imemkopesha mwalimu, kukutwa na kadi ya benki ya mwalimu aliyepewa mkopo... tukikubaini au kukukuta na kadi hizo, hatua kali tutazichukua ikiwamo kukufukuza kufanya kazi Simiyu," alisema Mtaka.

Aidha, aliwataka walimu kutumia elimu waliyonayo kuacha tabia ya kuacha nywila pamoja na kadi zao za benki kwenye taasisi hizo, huku akiwataka kuchukua mikopo kwa malengo, kwani wengi wao wamekimbia madeni.

Mtaka alieleza kusikitishwa na vitendo vya walimu mkoani humo kuendelea kudanganywa na watu ambao hawajasoma kwa kutakiwa kuacha kadi hizo, ikiwamo kutapeliwa fedha zao.

"Ofisini kwangu kuna kesi zaidi ya 40, ambazo walimu wa kike wamewakopea wapenzi wao pesa, kisha kuachwa... wapenzi wao hao wanakimbilia kusikojulikana, hili jambo ni aibu sana kwa walimu ambao wamesoma," alisema Mtaka.

Kadhalika, alisema kuwa baadhi ya walimu wamekuwa wakiweka rehani vyeti vyao vya elimu ili kukopesheka kwenye taasisi hizo ndogo za kifedha, na kuwataka kuacha tabia hiyo.



Mafundi wa ujenzi wa barabara wakimalizia kuweka zege kwenye barabara ya mtaa wa Siwa Mikocheni jijini Dar es Salaam jana. **NA MPIGAPIGA WETU**

# Tanzania ya 21 duniani kwa uboreshaji biashara ndogo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TANZANIA imetajwa kuwa nchi ya 21 duniani kwa kiwango cha biashara ndogo na uboreshaji wa shughuli za machinga.

Sifa hizo zimetolewa katika Ripoti ya Taasisi ya RMB (Rand Merchant Bank) mwaka huu, na kwamba pia Tanzania ni nchi ya nne kwa Afrika na ya kwanza kwa Afrika Mashariki.

Hayo yalielezwa jana na Msemaji Mkuu wa Serikali ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbasi, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu masuala ya kimataifa.

Alisema taasisi hiyo katika ripoti yake 'Niwekeze wapi Afrika ya mwaka 2020' ndio inaonyesha mafanikio hayo kwa Tanzania.

"RMB Where to Invest In Africa 2020, inaitaja Tanzania kuwa nchi ya 21 duniani, ya nne kwa Afrika na ya kwanza Afrika Mashariki kwa kiwango cha biashara ndogo ndogo na uboreshaji wa shughuli za Wamachinga," alisisitiza.

Alisema mafanikio hayo yametokana na hatua mbalimbali zilizofanywa na serikali kwa wamachinga ikiwamo kupewa vitambulisho ili wasisumbuliwe.

Kuhusu haki za binadamu, Dk. Abbasi alisema katika kikao cha 43 Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Taifa, kilichofanyika Februari 25, mwaka huu, Geneva, Uswisi, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, aliwasilisha ripoti ya Tanzania kuhusu masuala ya haki za binadamu.

"Alielezea mafanikio ya serikali ya awamu ya tano katika kulinda na kusimamia haki za binadamu na kutolea ufafanuzi wa swheria tatu zilizotungwa, tumeeleza nchi inavyotekeleza haki za binadamu katika mawanda yote ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kimaendeleo," alisema.

Alisema watu waelewe mawanda hayo kuwa sio siasa pekee bali kuna haki za kiraia na maendeleo kwa mwanadamu kwamba haki zote zitaenziwa.

Vile vile, alisema Ripoti ya Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ya mwaka 2020 imeitaja Tanzania kuwa moja ya nchi yenye mageuzi yanayogusa na kubadili maisha ya watu.

"Pia yaitaja Tanzania kuwa ni miongoni mwa nchi zilizopiga hatua kubwa katika kupunguza umaskini," alisema.

Kadhalika, alisema Shirika la Habari la Kimataifa la CNBC Africa juzi limerusha kwa zaidi ya nchi 100 duniani makala inayoeleza mafanikio ya Tanzania katika sekta mbalimbali iitwayo 'TANZANIA: The Soul of a New Africa'.

# SANE ARUDI DIMBANI, KUONGEZA NGUVU CITY




**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester City, Leroy Sane amesema anahisi anajiamini baada ya kurudi kutoka chumba cha majeruhi na kuichezea timu ya vijana chini ya umri wa miaka 23, akija kuongeza nguvu katika kikosi cha Pep Guardiola.

Sane alikuwa nje ya dimba tangu alipoumia kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Liverpool Agosti mwaka jana, lakini mchezaji huyo aliyekuwa akivumishiwa kwenda Bayern Munich alirudi dimbani Ijumaa.

Winga huyo wa kimataifa wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 24 alicheza kwa dakika 57 wakati City ikiifunga Arsenal 4-2 kwenye mchezo wa timu hizo chini ya umri wa miaka 23 pale Emirates.

"Najihisi kuwa vizuri," alisema akiwaambia waandishi wa habari. "ilikuwa jambo nzuri kwa namna nilivyorudi uwanjani.

"Bado sijawa fiti kwa asilimia 100, lakini ninajiamini sasa naweza kurudi kwenye kikosi nikiwa fiti zaidi.

"Najiamini na sikuwa na tatizo lolote, ninafuraha na namna nilivyorudi na kuweza kucheza. Bilashaka nitakuwa bora zaidi kwa siku chache zijazo."

# Lampard akerwa kwa sare Chelsea

**LONDON,** England

FRANK Lampard amejutia "dakika 10 mbaya" wakati Chelsea ikilazimishwa sare ya kufungana mabao 2-2 na Bournemouth kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England, Jumamosi.

Marcos Alonso alifunga mara mbili kila kipindi kuwawezesha kupata sare hiyo kwenye mchezo uliopigwa pale katika dimba la Vitality, huku mabao ya Bournemouth yakifungwa na Jefferson Lerma na Joshua King.

Lampard aliingia kwenye mchezo huo akitoka kushuhudia Blues hao wakichapwa 3-0 na Bayern Munich kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora.

"Tulitakiwa kushinda, tulikuwa na nafasi nyingi," alisema. "Tulikuwa na dakika 10 mbaya wakati walipofunga na hali ile sikuipenda.

"Hatukuwa mchezoni kwa dakika 10 na kwa hakika kabisa tulishinda kucheza kwa umakini mkubwa.

"Dhidi ya Bayern tuliruhusu mabao ya haraka mara mbili, hii si mara ya kwanza. Tatizo ni kwamba tulikosa utulivu na umakini? Inawezekana kutoka kwa wachezaji."





# *Tuchel awajia juu wanaoishutumu PSG*

**PARIS,** Ufaransa

THOMAS Tuchel amesema Paris Saint-Germain inatakiwa kubaki ikijiamini na kuwa na imani kwamba wana nafasi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya kupata ushindi mnono dhidi ya Dijon.

PSG walikabiliwa na shutuma nyingi baada ya kupoteza 2-1 kwa Borussia Dortmund kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora, lakini wakaifumua Dijon 4-0, Jumamosi.

Tuchel alisema hakukuwa na sababu ya kuitilia shaka timu yake ya PSG, ambayo inaongoza msimamo kwa pointi 13 kileleni mwa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

"Wachezaji wanatakiwa kuthibitisha kwamba, wanaweza kuchukua hatua mbele, shutuma zilikuwa nyingi mno," alisema kocha huyo wa PSG akiwaambia waandishi wa habari.

"Wana msimu mzuri, wakiwa wameshinda mechi nyingi, wakiwa na kiwango bora, kiwango cha kuvutia, kiwango imara. Wanastahili ushindi. Kulikuwa na sare chache na kipigo kimoja.

"Hatuwezi kupoteza ujasiri wetu kwa timu hii, hatuwezi kupoteza ujasiri kwa kundi hili. Kuna mechi mbili (ya kwanza na ya pili). Wachezaji wanataka kucheza mchezo wa pili. Wanataka kuthibitisha nini wanachoweza kukifanya.

"Wameanza kuonyesha uwezo wao kwenye mazoezi wiki hii, wameonyesha kwenye mchezo huu, wataendelea Jumatano (Kwenye nusu fainali ya Kombe la Ufaransa dhidi ya Lyon)."

# De Bruyne anahitaji vichache - Guardiola

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema kuna vitu vichache anavyoweza kuvitoa kwa Kevin De Bruyne ili aimarike zaidi kwani yeye ni mchezaji wa kipekee na mwenye kipaji ambaye anaweza kujipa changamoto yeye mwenyewe kufika mbali zaidi.

De Bruyne amekuwa nguzo muhimu zaidi kwa mafanikio ya Guardiola pale Manchester City tangu alipochukua mikoba ya kuinoa timu hiyo inayotumia Uwanja wa Etihad msimu wa 2016-17.


Kiungo huyo wa kimataifa wa Ubelgiji kwa mara nyingine alionyesha umuhimu wake kwenye kikosi cha City katikati ya wiki iliyopita wakati alipoisaidia kuifunga Real Madrid mabao 2-1 kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora.

Baada ya kutengeneza bao la kwanza, De Bruyne alifunga la ushindi kwa mkwaju wa penalti.

Wakati sifa za wachambuzi zikiendelea kumiminika kwa De Bruyne, Guardiola amesema ana vitu vichache sana vya kumpa ili aweze kuimarika zaidi.

"Kwa ukweli kabisa, aina hii ya wachezaji, changamoto inakuja kutoka kwao wenyewe, ndani yao," alisema Guardiola kabla ya mchezo wa fainali wa jana wa Kombe la EFL dhidi ya Aston Villa.

"Kama unatakiwa kuwasukuma kufikia kitu fulani ni kwa sababu si wakubwa. Sipendi wachezaji ambao wanalalamika kuhusu vitu."







# RONALDO HANA MPANGO WA KUCHEZA MAREKANI

**TURIN,** Italia

CRISTIANO Ronaldo amesisitiza hana nia yakutafuta uhamisho wa kuondoka Juventus licha ya uvumi kumhusisha na mpango wa kwenda katika klabu ya David Beckham, Inter Miami inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani, MLS.

Miami jana Jumapili ilitarajiwa kucheza mchezo wake wa kwanza kwenye Ligi Kuu ya Marekani (MLS), wakati waliposafiri kuifuata timu ya Los Angeles FC, baada ya kukamilika kwa mipango ya umiliki wa Beckham na usajili wa kuingia MLS ulioanza mwaka 2013.

Beckham aliinunua klabu hiyo Februari mwaka uliofuata na Januari 2018 timu yake ilipata leseni ya kushiriki MLS kwa msimu wa 2020.

Akiwa amekijenga kikosi chake kutoka chini, wachezaji wachache wanafikiriwa kujiunga na timu hiyo, lakini Beckham nia yake ni kuwapata wachezaji wenye majina makubwa kutoka ligi za Ulaya.

Beckham aliwataja Lionel Messi na Cristiano Ronaldo, kwamba wana uwezekano wa kutakiwa kujiunga na timu hiyo siku za usoni, lakini Ronaldo ameonekana kutokuwa na mpango huo.

"Nina furaha hapa," alisema Ronaldo akiiambia Sky Sports. "Nipo kwenye klabu bora nchini Italia.

"Nina furaha kucheza pamoja na wachezaji bora, nina furaha tumeshinda mataji msimu uliopita, na mwaka huu natumaini tutashinda pia."

# Klopp: Liver haiwezi kupata kila rekodi

**LIVERPOOL,** England

KOCHA Liverpool, Jurgen Klopp amedai hajaumizwa kwa kushindwa kuvunja rekodi baada ya matumaini yao ya kumaliza msimu wote wa Ligi Kuu ya England bila kufungwa kuzimwa na Watford, Jumamosi.

Wekundu hao walipata kipigo chao cha kwanza kwenye Ligi Kuu msimu huu, wakimaliza mechi 44 bila kupoteza, baada ya kuchapwa 3-0 pale kwenye dimba la Vicarage Road.

Ushindi huo wa Watford pia ulizima ndoto za Liverpool kupata ushindi wa muda mrefu zaidi kwenye Ligi Kuu, wakati walipoingia kwenye mchezo huo wakiwa wameshinda mechi 18 mfululizo.

Hata hivyo, Klopp ameelezea kuwa hakuwa anafikiria kufikia rekodi hiyo na kwamba macho yake yalikuwa yakiangalia zaidi kiwango cha wachezaji wake.

"Vijana tayari wana rekodi nyingine, hivyo hatufikiri kwamba tutamfunga kila mtu," alisema Klopp akiiambia Sky Sports. "Huwezi kupata kila rekodi unayotaka. Utatakiwa kucheza kwa kiwango. Matokeo yanatokana na kiwango chako.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER ATANGAZA RASHFORD KUREJEA

## Anataka kurudi, vipimo vimeonyesha ishara chanya, lakini tutampa muda...

**MANCHESTER,** England

MARCUS Rashford anatarajiwa kurudi dimbani kutoka chumba cha majeruhi ya mgongo baadaye msimu huu kwa ajili ya kuipa nguvu Manchester United, kocha Ole Gunnar Solskjaer amesema.

**Rashford, ambaye amefunga mabao 19 msimu huu, amekuwa nje ya dimba tangu katikati ya Januari mwaka huu kutokana na kuwa majeruhi.**

Lakini wakati kulikuwa na hofu kuwa mshambuliaji huyo kukosa kipindi chote cha msimu huu kilichobaki, Solskjaer amebainisha kwamba, mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 22, anaweza kurudi baadaye msimu huu wa 2019-20.

"Vipimo vimeonyesha ishara chanya," alisema kocha huyo akinukuliwa na magazeti ya Uingereza.

"Lakini tutampa muda anaouhitaji. Anataka sana kurudi uwanjani, bila shaka yoyote, lakini pengine itakuwa miezi mingine kadhaa kabla ya kumuona tena uwanjani. "Hatuwezi kufanya haraka, lakini wakati atakapokuwa fiti atakuwa imara, hivyo wakati atakaporudi uwanjani ataongeza nguvu kubwa kwa upande wetu."

Wakati United wakiwa nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England, jana Jumapili walikuwa ugenini kucheza na Everton, na pia wapo katika raundi ya tano ya Kombe la FA na wametinga hatua ya timu 16-bora kwenye Kombe la Ligi ya Europa.

Solskjaer amesema Rashford alikuwa na nia ya kurudi haraka uwanjani wakati huu United wakisaka angalau taji moja msimu huu.

"Anakaribia kurudi, anakuja vyumbani kabla ya mchezo na hata wakati wa mapumziko. Anawataka vijana kupambana na kufanya kweli, hivyo anaweza kurudi kwenye Ligi ya Europa na fainali ya FA," alisema.

"Anataka kuwa hapa wakati tukikaribia kukamilisha msimu na kuanza mambo upya."

## ZISIKUPITE

### BARCA NA AUBAMEYANG

KLABU ya Barcelona inaendelea kumtolea macho mshambuliaji wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 30, ambaye mkataba wake unamalizika mwisho mwa msimu ujao. ***(Sunday Express)***

### KUMPOTEZEA BECKHAM

NYOTA wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 35, amesema anafurahia kuwapo Juventus, hana mpango wa kujiunga na Inter Miami ya nchini Marekani inayomilikiwa na David Beckham. ***(Sky Sports)***

### GREALISH KUJAZWA NOTI UTD

KLABU ya Manchester United ipo tayari kutoa kiasi cha pauni 150,000 kama mshahara wa wiki kwa nahodha wa Aston Villa, Jack Grealish ili kutua Old Trafford msimu ujao. ***(Sun)***

### NYOTA CANADA LULU EPL

CHELSEA ipo kwenye mbio moja na Liverpool, Manchester United na Tottenham Hotspur kufuatilia maendeleo ya mshambuliaji wa kimataifa wa Canada, Jonathan David, 20, ambaye thamani yake ni pauni milioni 20. Mchezaji huyo ameifungia mabao 23 timu yake ya Genk ya Ubelgiji msimu huu. ***(Sunday Express)***

### LALLANA, SHAQIRI KUONDOKA

LIVERPOOL itakuwa na kibarua cha kuimarisha safu yake ya ushambulia msimu ujao kwa sababu, Adam Lallana mchezaji wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 31, na Xherdan Shaqiri raia wa Uswisi mwenye miaka 28, wote wanatarajiwa kuondoka mwisho mwa msimu huu. ***(Express)***

### OWEN AMVUTA ABDOULAYE

KIUNGO wa kati wa Watford, Abdoulaye Doucoure mwenye umri wa miaka 27, anatakiwa kusajiliwa na Liverpool, kwa mujibu wa mchezaji wa zamani wa timu ya Taifa ya England, Owen Hargreaves. ***(Daily Star)***

### HOLGATE KUIGHARIMU MAN CITY

KLABU ya Manchester City italazimika kulipa kiasi cha pauni milioni 40 ikiwa inataka kumsajili mlinzi wa Everton, Mason Holgate mwenye umri wa miaka 23. ***(Football Insider)***

### HAALAND AWINDWA MADRID

MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland ndiye anayewindwa zaidi na Real Madrid wakati wanapojiandaa kuongeza mshambuliaji mwingine kwa msimu wa tatu mfululizo. Timu hiyo ya Hispania inafahamu itatakiwa kulipa takriban pauni milioni 65 kwa ajili ya kuinasa saini ya mchezaji huyo. ***(Marca)***

### LIVER KUTESEKA KWA WERNER

NYOTA wa Klabu ya RB Leipzig, Timo Werner mwenye umri wa miaka 23, yuko kwenye orodha ya Real Madrid na hiyo inamaanisha kwamba, huenda Liverpool ikapata upinzani mkali wa kumpata mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani anayesemekana kuwa na thamani ya pauni milioni 51. ***(Daily Mail)***

### ARSENAL KUIBOMA SHEFFIELD

KOCHA wa Sheffield United, Chris Wilder amesema kiungo wa kati John Fleck, aliyesaini mkataba mpya wiki iliyopita, alikuwa anawindwa na timu nyingine. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, amehusishwa kutakiwa kule Arsenal. ***(Sheffield Star)***

HABARI MICHEZO

## Daraja la 4 Ilala waitiwa fomu

**Na Shufaa Lyimo**

LIGI Daraja la Nne Wilaya ya Ilala inatarajiwa kuanza Aprili 5, mwaka huu, huku ikishirikisha timu zote zilizosajiliwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Soka Wilaya ya Ilala (DRFA), Daudi Kanuti, alisema tayari fomu zimeanza kutolewa tangu Februari 24 na mwisho wa kurudisha itakuwa Machi 21, mwaka huu.

"Zoezi la kurudisha fomu ni mwezi wa tatu, hatutakuwa na muda wa ziada kwa sababu taarifa tuliitoa mapema," alisema Kanuti.

Kanuti alisema usaili utakuwa Machi 30, mwaka huu, na kwamba mwitikio ni mkubwa kutokana na timu nane mpaka sasa zimejitokeza kuchukua fomu za ushiriki.

Aidha, alisema hakuna vigezo zaidi ya timu iwe imesajiliwa na kuzitaka timu zote zijitokeze kushiriki.

"Ninaomba timu zijitokeze kushiriki kwa sababu itawasaidia wachezaji wao kujulikana pamoja na kuinua vipaji vyao," alisema.

## Azam haijakata tamaa ubingwa

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuambulia pointi nne kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, hatimaye ushindi wa bao 1-0 walioupata Azam FC dhidi ya JKT Tanzania umewafungua mdomo wa mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Bara.

Kabla ya mechi hiyo iliyopigwa kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Dodoma juzi, Azam ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Ndanda katika dimba la Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara na kisha kuchapwa 1-0 dhidi ya Namungo FC ikiwa Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi.

Na licha ya Azam FC kushuka dimbani mara 25 na kuambulia alama 48, ambazo ni 14 nyuma ya vinara Simba kabla ya mechi yao ya jana dhidi ya KMC, bado inaamini inaweza kutwaa taji hilo la Ligi Kuu.

Ofisa Habari wa Azam FC, Jaffary Maganga (pichani), alimwambia mwandishi wetu kuwa ushindi huo umerudisha morali kwa wachezaji wa kuendelea kupambana kufikia malengo waliyojiwekea ya kutwaa taji hilo.

Tayari watani wa jadi wa Simba, Yanga wamenyoosha mikono juu kuhusu mbio za ubingwa wakati huu wakiwa na alama 44 kwenye nafasi ya nne baada ya mechi 23, lakini Azam wenyewe wanaamini katika kupambana hadi kieleweke.



# KOCHA NAMUNGO FC AWEKA USHINDI KANDO

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya timu yake kutoa vipigo Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hitimana Thiery, amesema ligi hiyo ni ngumu na ili kuendelea kupata ushindi wana kazi kubwa ya kulinda uwezo na kiwango chao kwa sasa.

Juzi, Namungo iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 ugenini katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Samora mjini Iringa dhidi ya wenyeji, Lipuli FC.

Matokeo hayo yanaifanya Namungo kufikisha alama 46 katika nafasi ya tatu ikiwa ni pointi mbili nyuma ya washika nafasi ya pili, Azam FC.

**Hata hivyo, Namungo imeshuka dimbani mara 24, mechi moja nyuma ya Azam FC, kwenye msimamo wa ligi hiyo ambayo, Simba ipo kileleni iiwa na alama 62 kabla ya mchezo wao wa jana usiku dhidi ya KMC.**

Akizungumza na mwandishi wetu, Thiery alisema bado kuna mechi nyingi za kucheza kabla ya msimu kumalizika, na kuelekea hatua hii ya lala salama ligi inazidi kuwa na ushindani mkubwa.

"Unajua ligi bado ni ndefu na si ushindi wa mechi moja ama mbili ni lazima kuona namna gani mechi zote unapata matokeo ila kwa hatua ambayo tupo nawapongeza wachezaji wangu," alisema.

Katika mwendelezo wa ligi hiyo, keshokutwa, Jumatano Namungo FC itashuka katika Uwanja wa Gairo mkoani Morogoro kuwavaa wenyeji wao, Mtibwa Sugar waliopo katika nafasi ya 14 na pointi zao 27 baada ya kushuka dimbani mara 25.

NIMEMALIZA...




Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Mark Ocitti, akikimbia na kufanikiwa kumaliza mbio za kilomita 21 za Kilimanjaro Marathon 2020 zilizofanyika mjini Moshi jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Alliance FC yajivunia kiwango Yanga*

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Alliance FC, Mathias Wandiba, amekunwa na kiwango walichokionyesha dhidi ya Yanga juzi, huku akisema hawawezi kuwalaumu wachezaji wao zaidi ya kujipanga ili kupata matokeo mazuri katika mechi zilizobaki na kujiweka kwenye nafasi nzuri katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kauli hiyo imekuja baada ya juzi kukubali kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Yanga kwenye mechi ya ligi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Matokeo hayo yanaifanya Alliance kukalia nafasi ya 13 katika msimamo wa Ligi Kuu baada ya kujikusanyia pointi 29 kibindoni zilizotokana na mechi 25.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Wandiba alisema hawako katika nafasi nzuri kulingana na aliyekuwa chini yao akipata ushindi mechi mmoja na wao kupoteza watashushwa chini.

Katika msimamo huo, Mtibwa Sugar ipo nyuma yao ikiwa na alama 27 huku zote zikishuka dimbani mara 25 hadi sasa wakati huu Alliance ikiifuata Ruvu Shooting keshokutwa, Jumatano.

Alisema kwa sasa hawataweza kuwalaumu wachezaji wao kwa matokeo ya mchezo dhidi ya Yanga zaidi ya kufanyia kazi upungufu wao kwa ajili ya kutafuta matokeo katika michezo iliyopo mbele yao.

"Matokeo hayakuwa upande wetu japo tulipata nafasi nyingi za wazi, tukashindwa kuzitumia, Yanga wamepata nafasi tano na kutumia vema mbili na kutuadhibu.

"Kiwango walichoonyesha wachezaji watu ni kizuri, hivyo tunajipanga katika mchezo dhidi ya Ruvu Shooting, tumejipanga kuondoka na alama muhimu katika mechi hiyo," alisema Wandiba.

Alisema kikubwa wanachokifanya ni kuongeza umakini kwa wachezaji wao hasa washambuliaji kuhakikisha wanafanikiwa malengo yao ya kufanya vizuri katika michezo iliyopo mbele yao ili kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo.

# Michezo

Jumatatu Machi 2, 2020

Nipashe




Solskjaer atangaza Rashford kurejea UKURASA 30




Waziri wa Maliasili na Utalii, Hamisi Kigwangalla (katikati 6571), akishiriki mbio za Tigo Marathon kilomita 21, zilizofanyika mjini Moshi mkoani Kilimanjaro jana chini ya bia ya Kilimanjaro. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Yanga yaitaja Simba ushindi kwa Alliance

## ●●● Eymael asema hesabu za kuwavaa Wekundu wa Msimbazi hao zinazidi kuitika, amtaja Nchimbi kuwa...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kufanikiwa kufuta mzimu wa sare nne mfululizo, Kocha Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael, amefurahia kuimarika kwa kikosi chake kabla ya kuivaa Simba Machi 8, mwaka huu katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Juzi Yanga iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 kwenye uwanja huo dhidi ya Alliance FC, shukrani kwa Ditram Nchimbi aliyetupia yote mawili katika mechi hiyo ya Ligi Kuu Bara baada ya kutokea benchi dakika ya 46 kuchukuwa nafasi ya Tariq Seif.**

Ushindi huo umekuja baada ya Yanga kutoka sare nne dhidi ya Mbeya City, Tanzania Prisons, Polisi Tanzania na Coastal Union, hivyo kufikisha pointi 44 ikiwa nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo baada ya kushuka dimbani mara 23 hadi sasa.

Akizungunza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Eymael alisema amefurahishwa kuona mabadiliko makubwa kwa wachezaji kuzidi kuimarika na kufuata maelekezo yake katika mchezo wao dhidi ya Alliance na kufanikiwa kupata alama zote tatu.

Alisema mabadiliko hayo yanampa matumaini makubwa kuelekea mechi ya 'dabi' dhidi ya Simba, licha ya kwamba bado wana mchezo mmoja kabla ya kukutana na mahasimu wao hao.

Mbelgiji huyo alisema kwa sasa anakiandaa kikosi chake kukutana na Mbao FC kesho, Jumanne katika Uwanja wa Taifa na baada ya hapo hesabu atazielekeza dhidi ya Simba.

"Kwa sasa kiwango cha wachezaji kimeimarika na kitazidi kuimarika kuelekea katika mechi dhidi ya Simba, najua ni mechi ngumu ila tutahakikisha tunapambana na kupata matokeo mazuri katika mchezo huo," alisema Luc.

Alisema licha ya kuwapumzisha baadhi ya nyota wake, wameanza kufanya vema huku akihakikisha anawaongeza mbinu ili wawe bora zaidi.

Kuhusu Nchimbi, Eymael alisema amefurahishwa kwa namna alivyoweza kufuata maelekezo yake na kwenda kuipa timu ushindi huo walikuwa wakiusubiri kwa muda sasa.

"Nchimbi amenifurahisha, nimemwingiza kipindi cha pili akafuata maelekezo niliyompa akafunga mabao mawili hiyo ni burudani kwa mashabiki wetu," alisema.

Aidha, alisema kuna makosa madogomadogo ameyaona na kwamba ataendelea kuyafanyia kazi kabla ya kukutana na Simba. Kwa upande wake Nchimbi akizungumzia namna alivyofanikiwa kubadili matokeo dhidi ya Alliance juzi, alisema kocha alimtaka kutazama mchezo na kwenda kutumia makosa ya wapinzani ili kuipa timu yake ushindi.

"Kocha aliniambia kwamba ninapaswa nitazame upungufu wa wenzangu na nikafunge ili kuipa timu ushindi na mwisho wa siku ndicho kilichotokea," alisema Nchimbi.

Ushindi huo, umeifanya Yanga kuiacha Alliance nje ndani kufuatia mzunguko wa kwanza katika Uwanja wa CCM Kirumba kushinda kwa mabao 2-1 kabla ya juzi kuibugiza 2-0.

# Tanzania U-17 kidedea kufuzu Kombe la Dunia

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya Wanawake chini ya umri wa miaka 17, imetumia vizuri dimba lake la nyumbani baada ya kuifumua Uganda kwa mabao 2-1 katika mchezo wa kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia U-17 zitakazofanyika Julai mwaka huu nchini India.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana, Uganda walikuwa wa kwanza kuliona lango la Tanzania katika dakika ya tano kipindi cha kwanza, shukrani kwa Fauzia Najjemba aliyeunganisha nyavuni pasi ndefu kutoka kwa Margret Kunihira.

Bao hilo lilidumu hadi dakika ya 28 kufuatia Tanzania kusawazisha kupitia kwa mshambuliaji wake Aisha Masaka aliyepiga shuti kali na mpira kumshinda kipa baada ya kazi nzuri iliyofanywa na Irene Kisisa.

Tanzania ingeweza kuwa mbele kwa mabao 2-1 katika dakika ya 85, baada ya Bira Nadunga kumchezea madhambi Masaka ndani ya eneo la hatari na mwamuzi, Ema Paulo Novo kutoka Msumbiji kuamuru litengwe tuta, lakini Masaka alishindwa kulenga goli baada ya mkwaju wake kupita pembeni ya lango la Uganda.

Hata hivyo, katika dakika ya 88, Masaka alifuta makosa yake ya kukosa penalti baada ya kuifungia Tanzania bao la ushindi kufuatia kuitendea haki pasi ya Christer Mabanza.

Kwa matokeo hayo, Tanzania sasa inahitaji sare ama ushindi wowote watakaporudiana Machi 14, mwaka huu nchini Uganda ili kusonga mbele. Na kama ikifanikiwa kusonga mbele itakutana na mshindi wa jumla kati ya Ghana na Liberia.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >